# KISWAHILI

## KWA VYUO VYA UALIMU (TTC)

## KITABU CHA MWANAFUNZI

### MWAKA WA KWANZA

### MCHEPUO WA ELIMU YA LUGHA

© 2020 Bodi ya Elimu Rwanda

Haki zote zimehifadhiwa.

Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Elimu Rwanda.

Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Elimu Rwanda wakati yaliyomo yamenukuliwa.

## YALIYOMO

VIFUPISHO ........................................................................................ xiii

Dibaji .................................................................................................xiv

SHUKRANI ......................................................................................... xvi

UTANGULIZI .........................................................................................1

MADA YA 1: MATUMIZI YA KISWAHILI SHULENI .........................................3

SOMO LA 1: TARATIBU ZA SHULENI ......................................................4

1.1. Kusoma na ufahamu: Shule ya Icyerekezo ..........................................4

1.2. Msamiati kuhusu mazingira ya shule ...............................................6

1.3. Sarufi: Matumizi ya umoja na wingi wa majina ya ngeli ya LI-YA .......7

1.4. Matumizi ya lugha: Shughuli za Wafanyakazi Shuleni ......................8

1.5. Kusikiliza na kuzungumza .................................................................9

1.6. Kuandika ...............................................................................................9

SOMO LA 2: USAFI SHULENI ........................................................................ 11

2.1. Kusoma na ufahamu: Usafi wa mazingira ya shule yetu .................. 12

2.2. Matumizi ya msamiati ...................................................................... 14

2.3. Sarufi: Ngeli ya LI – YA na vivumishi vya kumiliki ............................ 15

2.4. Matumizi ya lugha ............................................................................. 16

2.5. Kusikiliza na kuzungumza ................................................................ 16

2.6. Kuandika ............................................................................................ 16

SOMO LA 3: VIONGOZI WETU SHULENI ........................................................ 16

3.1. Kusoma na ufahamu: Viongozi wa shule na wajibu wao ................. 16

3.2. Msamiati kuhusu mazingira ya shule .............................................. 18

3.3. Sarufi: Matumizi ya umoja na wingi wa majina ya ngeli ya li-ya ..... 18

3.4. Matumizi ya lugha: Vyeo vya viongozi shuleni ................................ 20
3.5. Kusikiliza na Kuzungumza ........................................................ 21
3.6. Kuandika ......................................................................... 21
SOMO LA 4 : RATIBA YA WIKI YA MWANAFUNZI ................................... 21
4.1. Kusoma na ufahamu: Ratiba ya shughuli za kila siku katika Shule ya Gasozi ..... 22
4.2. Matumizi ya msamiati ............................................................ 23
4.3. Sarufi: Matumizi ya vivumishi vya kuonyesha vya ngeli ya LI-YA 23
4.4. Matumizi ya lugha: Shughuli za kila siku za mwanafunzi ............... 24
4.5. Kusikiliza na Kuzungumza ........................................................ 24
4.6. Kuandika ......................................................................... 24
MADA YA 2: MSAMIATI KUHUSU MAZINGIRA YA NYUMBANI ................ 25
SOMO LA 5: MAZINGIRA YA NYUMBANI ............................................. 25
5.1. Kusoma na ufahamu: Makao ya Gakuba ........................................ 26
5.2. Matumizi ya msamiati ............................................................ 28
5.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya LI-YA. ............................................ 29
5.4. Matumizi ya lugha ................................................................ 30
5.5. Kusikiliza na kuzungumza ........................................................ 31
5.6. Kuandika ......................................................................... 31
SOMO LA 6: MSAMIATI KUHUSU WATU WANAOPATIKANA NYUMBANI ... 31
6.1. Kusoma na ufahamu: Watu wa nyumbani ........................................ 32
6.2. Msamiati kuhusu watu wa nyumbani ............................................ 33
6.3. Sarufi: Matumizi ya vivumishi vya idadi katika ngeli ya LI-YA......... 34
6.4. Matumizi ya lugha ................................................................ 35
6.5. Kusikiliza na kuzungumza ........................................................ 36

6.6. Kuandika ........ 36

SOMO LA 7: UHUSIANO WA KIFAMILIA ........ 36

7.1. Kusoma na ufahamu: Familia ya Rutebuka ........ 37

7.2. Msamiati kuhusu uhusiano wa kifamilia ........ 40

7.3. Sarufi: Matumizi ya vivumishi vya kuuliza katika ngeli ya LI-YA .... 41

7.4. Matumizi ya lugha ........ 42

7.5. Kusikiliza na Kuzungumza ........ 42

7.6. Kuandika ........ 42

SOMO LA 8: VIFAA VYA NYUMBANI NA USAFI WAKE ........ 43

8.1. Kusoma na ufahamu: Vifaa vya nyumbani na usafi wake ........ 43

8.2. Msamiati ........ 45

8.3. Sarufi: Nomino za ngeli ya LI-YA na vivumishi vya kumiliki ........ 46

8.4. Matumizi ya lugha ........ 47

8.5. Kusikiliza na Kuzungumza ........ 47

8.6. Kuandika ........ 47

SOMO LA 9: MSAMIATI KUHUSU MIFUGO ........ 48

9.1. Kusoma na ufahamu: Kazi nzuri ya ufugaji. ........ 48

9.2. Msamiati kuhusu mifugo ........ 53

9.3. Sarufi: Ngeli ya LI –YA na Vivumishi vya kuonyesha. ........ 54

9.4. Matumizi ya lugha ........ 55

9.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano ........ 56

9.6. Kuandika ........ 56

MADA YA 3: MSAMIATI KATIKA MAZINGIRA YA HOSPITALI .................... 58
SOMO LA 10: SEHEMU ZA HOSPITALI ............................................ 59
10.1. Kusoma na ufahamu: Ziara yetu hospitalini .................................. 59
10.2. Matumizi ya msamiati kuhusu mazingira ya hospitali.................. 63
10.3. Sarufi: Matumizi ya kauli za vitenzi ............................................ 63
10.4. Matumizi ya lugha: Sehemu muhimu za hospitali ........................ 64
10.5. Kusikiliza na Kuzungumza.......................................................... 65
10.6. Kuandika .................................................................................. 66
SOMO LA 11: VIFAA VYA HOSPITALINI.............................................. 66
11.1. Kusoma na ufahamu: Vifaa vya hospitalini.................................. 67
11.2. Matumizi ya msamiati.................................................................. 70
11.3. Sarufi: Matumizi ya kauli za vitenzi ............................................ 71
11.4. Matumizi ya lugha: Vifaa vya hospitalini ..................................... 72
11.5. Kusikiliza na Kuzungumza.......................................................... 73
11.6. Kuandika .................................................................................. 74
SOMO LA 12: WAFANYAKAZI WA HOSPITALINI....................................... 74
12.1. Kusoma na ufahamu: Kazi nzuri ya udaktari ................................ 75
12.2. Matumizi ya msamiati kuhusu mazingira ya hospitali.................. 76
12.3. Sarufi: Matumizi ya kauli za vitenzi ............................................ 77
12.4. Matumizi ya lugha: Aina za kazi.................................................. 78
12.5. Kusikiliza na Kuzungumza.......................................................... 81
12.6. Kuandika .................................................................................. 81
SOMO LA 13: USAFI KATIKA MAZINGIRA YA HOSPITALINI..................... 82
13.1. Kusoma na ufahamu: Usafi ni ufunguo wa afya nzuri.................... 82

13.2. Matumizi ya msamiati ........ 85
13.3. Sarufi: Matumizi ya kauli ya kutendeshana ........ 86
13.4. Matumizi ya lugha: Msamiati kuhusu aina za magonjwa ........ 87
13.5. Kusikiliza na kuzungumza ........ 88
13.6. Kuandika ........ 88
SOMO LA 14: ADABU HOSPITALINI ........ 89
14.1. Kusoma na ufahamu: Utaratibu hospitalini ........ 89
14.2. Matumizi ya msamiati ........ 90
14.3. Sarufi: Matumizi ya kauli za vitenzi ........ 91
14.4. Matumizi ya lugha: Muhtasari kuhusu kauli za vitenzi ........ 92
14.5. Kusikiliza na kuzungumza ........ 94
14.6. Kuandika ........ 94
MADA YA 4: MSAMIATI KUHUSU MAENEO YA UTAWALA ........ 96
SOMO LA 15: WILAYA YETU ........ 96
15.1. Kusoma na ufahamu: Ofisi za kiutawala ........ 97
15.2. Matumizi ya msamiati ........ 99
15.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya U-ZI ........ 100
15.4. Matumizi ya lugha: Ngazi za utawala ........ 104
15.5. Kusikiliza na Kuzungumza ........ 105
15.6. Kuandika ........ 106
SOMO LA 16: MAKAZI YA WATU ........ 106
16.1. Kusoma na ufahamu: Makazi ya watu ........ 107
16.2. Msamiati kuhusu makazi ........ 108
16.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya U-ZI ........ 109

16.4. Matumizi ya lugha: Makazi ya watu ........................................... 110
16.5. Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano kuhusu makazi ............ 111
16.6. Kuandika: Utungaji wa insha kuhusu makazi ............................. 111
SOMO LA 17: SIKUKUU ZA KITAIFA .................................................... 112
17.1. Kusoma na ufahamu: Sikukuu za kitaifa ....................................... 112
17.2. Msamiati kuhusu sikukuu za kitaifa ............................................. 113
17.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya U-ZI na vivumishi vya sifa .............. 114
17.4. Matumizi ya lugha: Sikukuu za kitaifa.......................................... 115
17.5. Kusikiliza na kuzungumza: Sikukuu za kitaifa............................. 116
17.6. Kuandika ........................................................................................... 116
SOMO LA 18: AINA MBALIMBALI ZA VITAMBULISHO ................. 116
18.1. Kusoma na ufahamu: Ombi la vitambulisho................................ 117
18.2. Msamiati kuhusu aina ya vitambulisho........................................ 118
18.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya U-ZI na vivumishi vya kumiliki ....... 119
18.4. Matumizi ya lugha.............................................................................. 121
18.5. Kusikiliza na Kuzungumza............................................................... 122
18.6. Kuandika ........................................................................................... 122
MADA YA 5: KISWAHILI KATIKA SHUGHULI ZA KIBIASHARA ............... 124
SOMO LA 19: MAWASILIANO SOKONI ........................................... 124
19.1. Kusoma na ufahamu: Safari ya Niwemwiza na Kayigi sokoni..... 125
19.2. Matumizi ya msamiati......................................................................... 128
19.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya I-ZI ..................................................... 129
19.4. Matumizi ya lugha: Msamiati maalumu katika uwanja wa kibiashara ... 131
19.5. Kusikiliza na kuzungumza................................................................ 134

19.6. Kuandika ........ 134

SOMO LA 20: MAJADILIANO DUKANI ........ 134

20.1. Kusoma na ufahamu: Muuzaji na mteja ........ 134

20.2. Matumizi ya msamiati ........ 136

20.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya I-ZI na vivumishi vya a- unganifu ... 136

20.4. Matumizi ya lugha: Aina za bidhaa zinazopatikana sokoni ........ 137

20.5. Kusikiliza na kuzungumza ........ 138

20.6. Kuandika ........ 138

SOMO LA 21: MATUMIZI BORA YA MIZANI ........ 138

21.1. Kusoma na ufahamu: Matumizi bora ya mizani ........ 139

21.2. Matumizi ya msamiati ........ 141

21.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya I-ZI na vivumishi vya kurejesha ...... 142

21.4. Matumizi ya lugha: Matumizi ya mizani katika hesabu na aina za pesa... 143

21.5. Kusikiliza na kuzungumza ........ 148

21.6. Kuandika ........ 148

MADA YA 6: UIGIZAJI WA MAZUNGUMZO ........ 150

SOMO LA 22: KUIGIZA MAZUNGUMZO ........ 150

22.1. Kusoma na ufahamu: Mazungumzo kati ya mwalimu mkuu wa shule na mzazi ........ 151

22.2. Matumizi ya msamiati ........ 153

22.3. Sarufi: Matumizi ya “nini”, “nani” na “lini’ katika kuuliza maswali ... 154

22.4. Matumizi ya lugha: Mazungumzo na uigizaji wake ........ 155

22.5. Kusikiliza na kuzungumza ........ 156

22.6. Kuandika ........ 156

SOMO LA 23: UMUHIMU WA UIGIZAJI WA MAZUNGUMZO.......... 157
23.1. Kusoma na ufahamu: Tujivunie lugha yetu.................................... 157
23.2. Matumizi ya msamiati............................................................ 159
23.3. Sarufi: Matumizi ya "nini", "wapi" na "kwa nini' katika kuuliza maswali... 159
23.4. Matumizi ya lugha: Mazungumzo na uigizaji wake ...................... 161
23.5. Kusikiliza na kuzungumza.................................................... 161
23.6. Kuandika.......................................................................... 161
SOMO LA 24: VIFAA KATIKA UIGIZAJI WA MAZUNGUMZO ........ 162
24.1. Kusoma na ufahamu: Majukumu yetu katika uigizaji wa mazungumzo.. 162
24.2. Matumizi ya msamiati............................................................ 164
24.3. Sarufi: Matumizi ya "gani" na "-ngapi' katika kuuliza maswali.... 166
24.4. Matumizi ya lugha............................................................... 167
24.5. Kusikiliza na kuzungumza.................................................... 168
24.6. Kuandika.......................................................................... 168
MADA YA 7: UTUNGAJI WA INSHA.................................................... 170
SOMO LA 25: DHANA YA INSHA ..................................................... 170
25.1. Kusoma na ufahamu: Mchuano wa fainali .................................... 170
25.2. Matumizi ya msamiati kuhusu kifungu cha habari ...................... 172
25.3. Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa ............................................ 173
25.4. Matumizi ya Lugha: Dhana ya insha na utungaji wake................ 174
25.5. Kusikiliza na kuzungumza .................................................... 175
25.6. Kuandika: Utungaji wa insha ................................................. 176
SOMO LA 26: AINA ZA INSHA ........................................................ 176
26.1. Kusoma na ufahamu: Usafi wa mavazi yetu................................. 178

26.2. Msamiati kuhusu kifungu cha hatari ............ 180
26.3. Sarufi: Matumizi ya alama za vituo ............ 181
26.4. Matumizi ya lugha: Ainaza insha ............ 184
26.5. Kusikiliza na kuzungumza ............ 186
26.6. Kuandika ............ 186
SOMO LA 27: INSHA YA MASIMULIZI ............ 187
27.1. Kusoma na ufahamu: Mafanikio ya kudumu ............ 187
27.2. Matumizi ya msamiati kuhusu kifungu ............ 190
27.3. Sarufi: Matumizi ya alama za vituo ............ 191
27.4. Matumizi ya lugha: Sifa za inshe ya masimulizi ............ 193
27.5. Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano ............ 193
27.6. Kuandika: Utangazaji wa insha ya masimulizi ............ 193
SOMO LA 28: MWONGOZO WA KUTUNGA INSHA ............ 194
28.1. Kusoma na kufahamu: Siku yangu ya kwanza katika shule za mabweni ... 194
28.2. Matumizi ya msamiati ............ 197
28.3. Sarufi: matumizi ya alama za vituo ............ 198
28.4. Matumizi ya lugha: Taratibu za kutunga insha ............ 200
28.5. Kusikiliza na kuzungumza ............ 202
28.6. Kuandika: Utungaji wa insha ............ 202
MADA YA 8: DHIMA YA LUGHA YA KISWAHILI KATIKA JAMII ............ 204
SOMO LA 29: TUONGEE KISWAHILI SANIFU ............ 204
29.1. Kusoma na ufahamu: Kiswahili nchini Rwanda ............ 205
29.2. Matumizi ya msamiati ............ 206
29.3. Sarufi: Matumizi ya hali ya kuamuru ............ 206

29.4. Matumizi ya Lugha: Maana na umuhimu wa lugha katika jamii. 208
29.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika jamii... 208
29.6 Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari .................................. 209
SOMO LA 30: MAWASILIANO YETU. ............................................... 209
30.1. Kusoma na ufahamu: Ziara ya mjini .......................................... 209
30.2. Matumizi ya msamiati kuhusu mawasiliano yetu ........................ 211
30.3. Sarufi: Hali ya kuamuru ............................................................ 213
30.4. Matumizi ya lugha: Mawasiliano yetu ........................................ 215
30.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano ..................................... 217
30.6. Kuandika: Utangaji wa insha...................................................... 218
SOMO LA 31: UMUHIMU WA LUGHA............................................... 218
31.1. Kusoma na ufahamu: Umuhimu wa lugha .................................. 218
31.2. Msamiati kuhusu umuhimu wa lugha ......................................... 221
31.3. Sarufi: Matumizi ya hali ya kuamuru ......................................... 222
31.4. Matumizi ya lugha: Umuhimu wa lugha...................................... 224
31.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano ..................................... 225
31.6. Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari.................................. 225
MAREJEO ........................................................................................ 227

## VIFUPISHO

**n.k:** na kadhalika

**k.v:** kama vile

**tnbh:** tanbihi

**m.f:** mfano

**agh:** aghalabu

## Dibaji

Mwanafunzi mpendwa,

Bodi ya Elimu Rwanda inayo heshima kwa kutoa Kitabu cha Kiswahili cha wanafunzi wa mwaka wa kwanza mchepuo wa elimu ya lugha katika Vyuo vya Ualimu.

Kitabu hiki ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo .

Falsafa ya elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo katika kila ngazi ya elimu ili kumwezesha kumudu vizuri katika jamii na kumpa fursa ya kujipatia ajira.

Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza umuhimu wa kufungamanisha ujifunzaji na ufundishaji na zana pamoja na mitaala ili kuwezesha mchakato wa ujifunzaji. Mambo mengi huathiri yale ambayo wanafunzi wanafundishwa , namna nzuri ya kujifunza na uwezo waupatao. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahususi wa yaliyomo, ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo.

Tumezingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza ambao unakuwezesha kuendeleza mawazo yako na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti; yawe ya binafsi au katika makundi, kwa msaada wa wakufunzi ambao majukumu yao ni kufanikisha ufundishaji. Utapata stadi zinazofaa kukuwezesha kutumia yale uliyojifunza katika miktadha ya maisha halisi. Kwa kufanya hivyo, utaonyesha tofauti siyo tu katika maisha yako bali hata kwa taifa.

Hii inatofautiana na mfumo wa zamani kuhusu nadharia ya ujifunzaji iliyosisitiza mchakato wa kujifunza kama upataji wa maarifa kutoka kwa yule aliyemzidi maarifa na hasa akiwa ni mkufunzi.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi ambapo dhana aghalabu huanzishwa kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na upatikanaji chanya wa maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya kujifunza hujishughulisha na wanafunzi kwa kufanya mambo na kufikiri kuhusu yale wanayoyafanya na wanafarijika kuonyesha uzoefu wao halisi na maarifa katika mchakato wa ujifunzaji.

Katika mtazamo huu, ili uweze kutumia kitabu hiki kwa ufanisi, jukumu lako litakuwa:

- Kuendeleza maarifa na stadi kwa kufanya kazi au mazoezi yanayolenga kwenye mada zote husika. Kuwasiliana na kupeana taarifa sahihi pamoja na wanafunzi wengine kwa kupitia mawasilisho, mijadala, kazi katika makundi na mbinu nyingine za ufundishaji kama: michezo ya kuigiza, utafiti, uchunguzi na utafiti katika maktaba, kwenye mitandao na hata nje ya shule.
- Kushiriki na kuwajibika kuhusu ujifunzaji wako na kufanya utafiti, uchunguzi kwenye maandishi yaliyochapishwa / mtandaoni, wataalamu na kuwasilisha matokeo ya utafiti.
- Kuhakikisha ufanisi mzuri wa mchango wa kila mwanakundi katika kazi sahihi uliyopewa kupitia maelezo na majadiliano unapoongea hadharani.
- Kutoa hitimisho sahihi kuhusu matokeo ya utafiti uliotokana na mazoezi ya ujifunzaji.

Napenda kutoa shukrani kwa wale wote walioshiriki na kutoa mchango wa kuboresha kitabu hiki, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Elimu Rwanda (CTLR-REB) walioandaa mchakato wa kazi hii tokea ilipoanza.

Pongezi muhimu ziwaendee walimu kutoka shule tofauti kwa kuendeleza na kufanikisha kazi hii. Maoni au mawazo yoyote yanakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo yatakayofuata .

**Dkt. Irénée NDAYAMBAJE**

**Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Elimu Rwanda**

## SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki. Kitabu hiki kisingeliwezekana kufanikiwa bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki; jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati.

Shukrani zangu ziwaendee viongozi wa shule mbalimbali walioruhusu walimu wao kufanya kazi na Bodi ya Elimu Rwanda katika mradi wa ukamilishaji wa kitabu hiki. Napenda kutoa shukrani zaidi kwa walimu ambao juhudi zao na uandikikaji wa kitabu hiki ulikuwa wa thamani.

Mwishowe, shukrani ziwaendee wafanyakazi wote wa Bodi ya Elimu Rwanda (CTLR-REB) walioshiriki katika mchakato wa kufanikisha uandikaji wa kitabu hiki.

**Joan MURUNGI**

**Mkuu wa idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana (CTLR)**

## UTANGULIZI

Kiswahili ni lugha ambayo imepewa kipaumbele zaidi kutokana na umuhimu wake wa kutumiwa kama lugha rasmi miongoni mwa lugha nyingine zinazotumiwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Nchini Rwanda, lugha ya Kiswahili hufundishwa katika shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha tatu katika ngazi ya chini ya sekondari. Zaidi ya hayo, mbali na mchepuo wa lugha ambapo Kiswahili hufundishwa katika mchepuo wa Fasihi, Kinyarwanda na Kiswahili, lugha hii hufundishwa pia katika michepuo mingine. Kwa hiyo, lugha ya Kiswahili imepiga hatua kimatumizi nchini Rwanda, katika jamii mbalimbali barani Afrika na hata ulimwenguni. Nchi kama vile Marekani, Ujerumani na nchi nyingi za Ulaya, hufundisha Kiswahili na kukitumia katika mazingira tofauti.

Kitabu hiki kimeandikwa kwa kuwalenga wanafunzi wa mwaka wa kwanza katika vyuo vya ualimu nchini Rwanda.

Kila mada iliyojadiliwa katika kitabu hiki, imegawanywa katika masomo ambapo kila somo limegusia vipengele vifuatavyo:

- Kusoma na ufahamu
- Matumizi ya msamiati wa msingi
- Sarufi
- Matumizi ya lugha
- Kusikiliza na kuzungumza
- Kuandika.

Masomo yaliyopendekezwa katika kitabu hiki yamezingatia matakwa na mahitaji ya nchi ya Rwanda kwa sababu Kiswahili kinahitajika kutumiwa katika mawasiliano mapana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, mwanafunzi anatakiwa kujifunza hatua kwa hatua masomo yote yaliyopendekezwa ili aweze kujijengea na kujifungulia milango ya kujiendeleza na kuliendeleza taifa lake kwa ujumla.

Uwezo utakaopatikana kupitia masomo hayo, utamwezesha mwanafunzi kukabiliana na matatizo mbalimbali yanayojitokeza katika maisha yake ya kila siku: kutunza mazingira, elimu kuhusu uzalishaji mali au ujasiriamali, usawa wa jinsia, mafunzo kuhusu amani na maadili, mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari, mafunzo kuhusu desturi ya usanifishaji, elimu kuhusu ujinsia, elimu jumuishi.

Ni vyema mwanafunzi ajitahidi kufanya kazi zilizotolewa kwa kila somo. Vilevile, ni jambo muhimu kusoma kwa makini na kufanya uchunguzi wa mada zilizojadiliwa katika kitabu hiki. Kazi nyingi zilizopendekezwa zitamwezesha mwanafunzi kukuza uwezo wake katika kiwango cha utafiti, ushirikiano na utawala binafsi na stadi za maisha na kuendeleza ujifunzaji wa muda mrefu. Vilevile, kazi za mijadala ya kibinafsi na ya makundi zote zitasaidia kumjenga mwanafunzi kwa kumpa uwezo wa kuwasiliana na watu mbalimbali kwa kutumia Kiswahili fasaha.

Kazi za makundi zilizopendekezwa zitamsaidia mwanafunzi kuelewa nafasi yake katika kujenga desturi ya heshima kwa wengine, uvumilivu, upendo na amani, haki, umoja na mshikamano na demokrasia.

Ili kufanikisha ujifunzaji wake, ni vyema mwanafunzi akumbuke kwamba kitabu hiki kinafuata vitabu vingine vya Kiswahili ambavyo viliandaliwa kwa wanafunzi wa awamu ya kwanza ya shule za Sekondari nchini Rwanda. Kwa hiyo, mwanafunzi awe na ujuzi wa awali wa kutosha ambao utamwezesha kuelewa mada zilizotolewa katika kitabu hiki na kuhakikisha kwamba amepata uwezo wa kutosha wa kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano na shughuli mbalimbali za maisha.

# MADA YA 1

# MATUMIZI YA KISWAHILI SHULENI

**Uwezo mahususi wa mada:** Kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha na kuandika matini fupifupi kwa kusisitizia msamiati maalum unaotumiwa katika mazingira ya shuleni.

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kutumia kwa ufasaha msamiati unaotumiwa katika mazingira ya shule;
- Kueleza kuhusu wafanyakazi wanaopatikana shuleni;
- Kueleza kuhusu msamiati unaohusiana na shughuli zifanyikazo shuleni;
- Kutunga sentensi kwa kuzingatia matumizi ya umoja na wingi wa majina ya ngeli ya LI-YA.

## Kidokezo



Tazama mchoro huu na kueleza kinachofanyika hapa juu.

# SOMO LA 1: TARATIBU ZA SHULENI

## 1.1. Kusoma na ufahamu: Shule ya Icyerekezo

**Soma kifungu cha habari hapa chini kisha ujibu maswali yanayofuata**

Shule yetu inaitwa Shule ya Sekondari ya Icyerekezo. Shule hii inapatikana katika wilaya ya **Kicukiro** makao yake makuu yapo mjini Kigali. Shule hii ya Ikerekezo ina walimu ishirini na madarasa kumi na mawili pamoja na wafanyakazi wengine kumi ambao siyo walimu.

Inapokuwa kipindi cha muhula kuanza, jumuiya nzima ya shule huchukua muda wa saa mbili za mazungumzo kuelezea kuhusu taratibu za shule kwa ujumla kabla ya kuanza shughuli yoyote shuleni.

Mazungumzo haya huanzishwa na mkuu wa shule ambaye huanza kwa kuelezea kama ifuatavyo:

Shughuli za shule huanza saa mbili kila siku, inapofika saa nne huwa kuna mapumziko ya dakika ishirini. Baada ya hapo masomo huendelea hadi saa sita,ambapo kunakuwepo mapumziko ya saa moja kwa chakula cha mchana. Saa saba masomo yanaendelea hadi saa kumi.

Baada ya masomo, wanafunzi hufanya usafi binafsi kwa muda wa saa moja, kisha hujitayarisha kwa chakula cha jioni ambacho hupatikana saa moja na baadaye huendelea na masomo binafsi darasani hadi saa tatu ambao ni muda wa kwenda kulala.

Saa moja asubuhi ni muda wa kupata kifunguakinywa (staftahi) hadi saa moja na nusu huku wakijiandaa kuanza masomo. Utaratibu huu unaanzia Jumatatu hadi Ijumaa.

Shule hii ina madarasa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita. Ina mikondo miwili yaani mchepuo wa lugha na mchepuo wa sayansi.

Shule hii ina maabara mbili. Maabara ya kidato cha kwanza hadi cha tatu na maabara ya kidato cha nne hadi cha sita kwa kufanyia mazoezi ya vitendo kwenye masomo ya lugha na sayansi.

Idadi ya wanafunzi wote ni mia tano. Kuna ofisi ya naibu mkuu wa shule, mkuu wa taaluma ambaye anashughulika na taratibu za mafunzo ya wanafunzi ya kila siku, mkuu wa nidhamu na ofisi ya walimu kwa ujumla. Baada ya maelezo haya, mkuu wa shule alichukua fursa ya kuwatambulisha walimu na wafanya kazi wengine.

Mara baada ya mkuu wa shule kumaliza kuwatambulisha wafanyakazi wote wa shule, alitoa fursa kwa wanafunzi kuuliza maswali huku akianzia kidato cha kwanza ambao ndio waliokuwa wageni muhula huo.

Mwanafunzi wa kidato cha kwanza alipewa fursa ya kuuliza swali na kuanza kama ifuatavyo: Mimi naitwa Revocatus Kabayiza; mwanafunzi wa kidato cha kwanza. Swali langu ni hili: “Mmetuelezea kuwa kufanya usafi binafsi shuleni ni kuanzia saa kumi. Je, mbona hamkutuelezea shughuli za siku ya Jumamosi na Jumapili ?”

Mkuu wa shule alimshukuru kwa swali zuri, kisha akaendelea kuwaelezea kuwa siku ya Jumamosi ni utawala binafsi, yaani wanafunzi hupata staftahi kama kawaida baada ya hapo ni kufanya usafi wa mazingira kwa muda wa saa moja. Wanafunzi hujigawa katika makundi ya kufanya usafi darasani, kwenye mabweni na kwenye mazingira ya shule.

Chakula cha mchana hupatikana saa za kawaida na siku ya Jumapili ni utawala binafsi shuleni, pale ambapo itaonekana kuwa kuna mwanafunzi mwenye matatizo siku za Jumamosi na Jumapili, ataweza kumwona mwalimu wa zamu kupitia viranja wenu pamoja na viongozi wa madarasa.

Baada ya maelezo mazuri haya, mkuu wa shule aliwatakia kila la heri na fanaka kwa kuanza muhula mpya wa masomo. Wanafunzi walionyesha furaha yao kwa kumpigia makofi mkuu wa shule wakionyesha walivyofurahia mazumgumzo yake. Baadaye, mkutano ulimalizika na shughuli za shule ziliendelea kama kawaida.

## Kazi ya 1

**Maswali ya Ufahamu**

1. Ni wahusika gani wanaozungumziwa katika kifungu hiki?
2. Mkuu wa shule alikuwa na lengo lipi kwa kufanya mkutano na wanafunzi?
3. Wanafunzi hao walikuwa katika kiwango gani cha elimu?
4. Nini maana ya mkuu wa taaluma?
5. Unadhani wanafunzi hawa wamefurahia mazungumzo waliyopewa na mkuu wa shule ? Eleza maoni yako.
6. Kifungu hiki cha habari kinazungumzia kuhusu:
   a. Maabara ya shule ya Icyerekezo.
   b. Utaratibu wa shule ya sekondari ya Icyerekezo.
   c. Ziara ya wanafunzi wa Shule jirani.
   d. Masomo ya Shule.

7. Ofisi ya Taaluma hujishughulisha na:

a. Wafanyakazi wote shuleni.

b. Wapishi shuleni.

c. Masomo na kumbukumbu za kila siku za wanafunzi.

d. Mwalimu wa zamu, viranja na viongozi wa madaras.

8. Maabara ni sehemu ambayo walimu na wanafunzi hufanyia:

a. Mchezo wa mpira wa miguu.

b. Mazoezi ya chemshabongo.

c. Sehemu ya kufanyia mazoezi ya sayansi kwa vitendo.

d. Sehemu ya kufanyia mikutano.

9. Ofisi ya walimu ni:

a. Eneo la burudani na starehe.

b. Mahali pa kuzungumzia na kupigia porojo.

c. Sehemu ya kufanyia kazi na kutayarisha masomo ya wanafunzi.

d. Hakuna shughuli yoyote ifanyikayo huko.

## 1.2. Msamiati kuhusu mazingira ya shule

### Kazi ya 2

**Baada ya kusoma kifungu cha habari cha hapo juu,oanisha msamiati ulio katika sehemu A na maelezo yake katika sehemu B.**

| | |
|---|---|
| 1. Maabara<br>2. Mkuu wa shule<br>3. Afisa wa taaluma<br>4. Mratibu wa nidhamu<br>5. Kiranja<br>6. Wapishi | a. Mwalimu anayehusika na masomo ya kila siku shuleni pamoja na utunzaji wa vyeti na alamaza za wanafunzi.<br>b. Kiongozi wa shule.<br>c. Kiongozi wa wanafunzi.<br>d. Sehemu ya kufanyia utafiti. |

| | |
|---|---|
| 7. Mwalimu wa zamu<br>8. Elimu ya juu au chuo kikuu | e. Mwalimu anayeshughulikia mienendo na nidhamu ya wanafunzi.<br>f. Hushughulikia shughuli zote za wanafunzi na maisha yao ya kila siku.<br>g. Hushughulikia maandalizi ya chakula cha wanafunzi.<br>h. Sehemu ya kuendelea na masomo ya chuo kikuu. |

## 1.3. Sarufi: Matumizi ya umoja na wingi wa majina ya ngeli ya LI-YA

**Kazi ya 3:**

**Chunguza sentensi zilizo katika sehemu A na sehemu B na kueleza mabadiliko yanayojitokeza.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| Yai hili lilikuwa zuri. | Mayai haya yalikuwa mazuri. |
| Jani hili limepukutika. | Majani haya yamepukutika. |
| Jicho hili linaniuma. | Macho haya yananiuma. |
| Ini hili lilikuwa tamu. | Maini haya yalikuwa matamu. |
| Ua hili lilichanua. | Maua haya yalichanua. |

Mifano ya maneno yaliyomo katika ngeli ya LI-YA katika umoja na wingi:

| | Umoja | wingi |
|---|---|---|
| 1. | Kundi | Makundi |
| 2. | Shirika | Mashirika |
| 3. | Jani | Majani |
| 4. | Gari | Magari |
| 5. | Darasa | Madarasa |

***Tanbihi*** : Kuna majina ya ngeli hii yasiyokuwa na umoja yaani hubaki katika wingi kama vile:

*Maji, mate, maziwa (ya kunywewa), mateso, manukato, mazishi, matumizi, manufaa, masafa.*

Katika sentensi, majina ya ngeli hii hufuatwa na kitenzi chenye kiambishi awali **li-** katika umoja na **ya-** katika wingi.

**Mfano:**

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Shirika **li**liundwa. | Mashirika **ya**liundwa. |
| 2. | Koti **li**ngesafishwa. | Makoti **ya**ngesafishwa. |
| 3. | Chungwa **li**liangushwa. | Machungwa **ya**liangushwa. |

Majina mengi ya ngeli ya **li-ya** hufanya wingi wake kwa kiambishi awali **ma-** kama inavyoonekana kwenye mifano iliyotolewa hapa chini.

| | |
|---|---|
| Bega langu linaumwa. | Mabega yangu yanaumwa. |
| Ua linachanua. | Maua yanachanua. |
| Ini linaumwa. | Maini yanaumwa. |
| Jiko limechafuka. | Meko yamechafuka. |

**Kazi ya 4:**

**Tunga sentensi za umoja na za wingi kwa kutumia maneno haya: jaribio, swali, jino, jembe, juma, jengo**

## 1.4. Matumizi ya lugha: Shughuli za Wafanyakazi Shuleni

**Kazi ya 5:**

**Zungumzia kuhusu viongozi wote wa shule na wajibu wao.**

**Kazi ya 6:**

**Husisha sehemu A na sehemu B**

| **Sehemu A** | **Sehemu B** |
|---|---|
| 1. Ubao | a. Hutumiwa kuhifadhia vitabu vya shule. |
| 2. Kabati la shule | c. Hutumiwa kuchezea wanafunzi. |
| 3. Maktaba | d. Nyumba au Chumba mnamohifadhiwa vitabu ili watu waweze kuazima au kusomea vitabu humo. |
| 4. Madawati ya shule | e. Hutumiwa kukaliwa na wanafunzi darasani. |
| 5. Uwanja wa shule | f. Hutumiwa kuandikia maelezo mbalimbali ya wanafunzi. |

## 1.5. Kusikiliza na kuzungumza

**Kazi ya 7:**

**Itambulishe shule uliposomea katika kidato cha tatu**

## 1.6. Kuandika

**Kazi ya 8:**

**Buni mazungumzo kati ya Mkuu wa Shule na wanafunzi wawili.**

**Kazi ya 9:**

**Iangalie ratiba hii kisha panga vipindi vyako inavyostahili kulingana na ratiba yako ya kila siku.**


## RATIBA YA SHULE

| | Muda (saa) | Jumatatu | Jumanne | jumatano | Alhamisi | Ijumaa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1:20—2:00 | Utawala binafsi | | | | |
| 2 | 2:00 - 2:40 | Kipindi cha 2 cha somo la... | Kipindi cha 2 cha somo la... | Kipindi cha 2 cha somo la... | Kipindi cha 2 cha somo la... | Kipindi cha 2 cha somo la... |
| 3 | 2:40 -3 :20 | Kipindi cha 3 cha somo la... | Kipindi cha 3 cha somo la... | Kipindi cha3 cha somo la... | Kipindi Cha 3 cha somo la... | Kipindi Cha 3 cha somo la... |
| 4 | 3:20 - 4:00 | Kipindi cha 4 cha somo la... | Kipindi cha 4 cha somo la... | Kipindi cha 4 cha somo la... | Kipindi cha 4 cha somo la... | Kipindi cha 4 cha somo la... |
| | 4:00 – 4:20 | Mapumziko ya kati | | | | |
| 5 | 4:20 – 5:00 | Kipindi cha 5 cha somo la... | Kipindi cha 5 cha somo la... | Kipindi cha 5 cha somo la... | Kipindi cha 5 cha somo la... | Kipindi cha 5 cha somo la... |
| 6 | 5:00 – 5:40 | Kipindi cha6 cha somo la... | Kipindi cha 6 cha somo la... | Kipindi cha 6 cha somo la... | Kipindi cha 6 cha somo la... | Kipindi cha6 cha somo la... |
| 7 | 5:40 – 6:20 | Kipindi cha 7 cha somo la... | Kipindi cha 7 cha somo la... | Kipindi cha 7 cha somo la... | Kipindi cha 7 cha somo la... | Kipindi cha 7 cha somo la... |
| | **6:20 -7:40** | Mapumziko ya Chakula cha mchana | | | | |
| 8 | 7:40 - 8:20 | Kipindi cha 8 cha somo la... | Kipindi cha 8 cha somo la... | Kipindi cha 8 cha somo la... | Kipindi cha 8 cha somo la... | Kipindi cha 8 cha somo la... |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 9 | 8:20 - 9:00 | Kipindi cha 9 cha somo la... | Kipindi cha 9 cha somo la... | Kipindi cha 9 cha somo la... | Kipindi cha 9 cha somo la... | Kipindi cha 9<br><br>cha somo la... |
| 10 | 9:00 - 9:40 | Kipindi cha 10 cha somo la... | Kipindi cha 10 cha somo la... | Kipindi cha 10 cha somo la... | Kipindi cha 10 cha somo la... | Kipindi cha 10<br><br>cha somo la... |
| 11 | 9:40-10:20 | Kipindi cha 11 cha somo la... | Kipindi cha 11 cha somo la... | Kipindi cha 11 cha somo la... | Kipindi cha 11 cha somo la... | Kipindi cha 11<br><br>cha somo la... |
| 12 | 10:20-11:00 | Utawala binafsi | | | | |

## SOMO LA 2: USAFI SHULENI


### Kidokezo



### Kazi ya 1:

**Tazama mchoro hapo juu kisha uzungumzie unayoyaona.**

## 2.1. Kusoma na ufahamu: Usafi wa mazingira ya shule yetu




**Soma kifungu cha habari hapa chini kisha ujibu maswali yanayofuata**

Usafi shuleni ni shughuli au kazi moja muhimu inayofanyika shuleni. Usafi wa shule na vifaa vya shule ni njia ya kuendeleza afya kwa kuzuia mawasiliano ya binadamu na athari za taka. Athari hizo zinaweza kuhusu mwili wa binadamu.

Uchafu unachangia pakubwa kuharibu maisha ya binadamu. Usafi shuleni ni jambo ambalo linafaa kutiliwa maanani na wanafunzi, walimu, viongozi wa shule na wafanyakazi wengine wa shule. Watu wa shuleni wachache wanafikiri kuwa usafi unahusu miili na sare tu wakisahau kuwa usafi huhusu kila kitu kinachopatikana na sehemu zote katika mazingira ya shule.

Wanafunzi ni lazima wawe safi. Sare humfanya mwanafunzi aonekane maridadi na apendeze. Mavazi ni hifadhi ya staha ya utu wa mtu. Mavazi hukusudia pia kuficha utupu wa mtu. Wanaposafisha sare zao, wanajiepusha na magonjwa yanayotokana na wadudu wanaoweza kuishi katika nguo chafu. Wadudu hawa ni kama chawa, viroboto na kadhalika. Isitoshe, usafi wa sare lazima uende sambamba na usafi wa mwili. Usafi wa mwili unahusiana na kuoga, kunyoa nywele, kupiga mswaki na kukata kucha.

Sehemu za shule zinazoshughulikiwa kusafishwa ni kama vile: darasani, nje ya darasa, bweni, bwalo, vyoo, chumba cha wasichana, ofisi za walimu na wakuu wa shule, viwanja vya michezo, n.k. Wanafunzi wanaposafisha sehemu zote hizo wanatumia vifaa kama vile: ndoo ya maji, sabuni za kawaida au sabuni za kemikali au dawa za kuulia wadudu wenye kuambukiza watu, deke, n.k.

Wanafunzi au wafanyakazi wengine wanakata nyasi zinazozunguka madarasa ili kuwafukuza mbu wanaosababisha ugonjwa wa malaria. Ni lazima kuhifadhi mazingira. Katika bustani, wanatumia jembe kwa kupalilia na panga kwa kukata nyasi. Wanafunzi au watu wengine wasitupe uchafu ovyoovyo. Taka zote zinazotokana na vitu vyote vilivyotumiwa zinafaa kutupwa mahali panapofaa kama vile pipa la taka au jalalani.

Wanafunzi wasisahau usafi wa vifaa vya shule kama vile: vitabu, madaftari, kalamu, kifutio, dawati, meza ya mwalimu, n.k. Wanafunzi wanaombwa kuwa na vitabu na madaftari yenye vifuniko safi. Inakatazwa kuharibu vifaa vya shule kwa kila mtu.

Shuleni, maji yote ya kunywa na ya matumizi mengine yatoke kwenye vyanzo salama au yachemshwe. Vyombo vya kubebea na kuhifadhi maji viwekwe safi ndani na nje na kufunikwa ili kuepuka uchafuzi wa maji. Wanafunzi wawe na tabia ya kunawa mikono kwa maji na sabuni kabla na baada ya chakula na baada ya kutoka chooni.

### Kazi ya 2:

**Maswali ya Ufahamu**

1. Usafi shuleni unasadia nini binadamu?
2. Usafi shuleni ni jambo ambalo linafaa kutiliwa maanani. Eleza.
3. Usafi shuleni unawahusu watu gani?
4. Watu wachache wa shule wanafikiri nini kuhusu usafi?
5. Kwa sababu gani wanafunzi wanaombwa kuvaa sare safi?
6. Faida gani ya kusafisha sare za wanafunzi?
7. Kuna umuhimu gani wa kukata nyasi zinazozunguka madarasa?
8. Tunatumiaje pipa za taka na jalala?
9. Wanafunzi wanatumia nini kusafisha bustani ?

## 2.2. Matumizi ya msamiati

### Kazi ya 3:

**Toa maana ya msamiati ufuatao na kuutumia katika sentensi sahihi**

1. Usafi
2. Uchafu
3. Athari
4. Maanani
5. Bweni
6. Bwalo
7. Mbu

### Kazi ya 4:

**Jaza sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo kutoka kifungu cha hapo juu:** (yachemshwe, kunawa, jalalani, kunyoa, mswaki, hifadhi, maridadi, unahusu, usafi, kuharibu)

1. ……… ni jambo ambalo linafaa kutiliwa maanani shuleni.
2. Watu wachache wa shuleni wanafikiri kuwa usafi ni…….mikono, kuoga na kuvaa sare safi.
3. Sare humfanya mwanafunzi aonekane ……………..na apendeze.
4. Mavazi ni …………..ya staha ya utu wa mtu.
5. Usafi wa mwili unahusiana na kuoga, …….. nywele, kupiga ………. na kukata kucha.
6. Taka zote zinazotokana na vitu vyote vilivyotumiwa, zinafaa kutupwa mahali panapofaa kama vile pipa la taka au....................
7. Wanafunzi wana tabia ya……….. mikono kwa maji na sabuni kabla na baada ya chakula.
8. Maji yote ya kunywa na ya matumizi mengine lazima yatoke kwenye vyanzo salama au ………………

## 2.3. Sarufi: Ngeli ya LI – YA na vivumishi vya kumiliki

### Kazi ya 5:

**Chunguza mifano ya sentensi hapa chini na ueleze aina za maneno yaliyopigiwa mstari.**

a. Jino **langu** linaniuma.

b. Gazeti **letu** lina habari nyingi.

c. Shamba **lako** limelimwa vizuri.

d. Dawati **lenu** linavunjika.

e. Soko **lao** linajaa watu.

**Maelezo muhimu**

Vivumishi vya kumiliki ni **-angu, -ako, -ake, -etu, -enu** na **-ao**. Vivumishi hivi katika ngeli ya **Li-Ya** huchukua kiambishi konsonanti **l-** katika umoja na **y-** katika wingi.

### Kazi ya 6:

**Andika sentensi zifuatazo katika umoja au wingi**

1. Jiji letu linapata wageni kutoka Kigali.
2. Ua langu linapamba mazingira.
3. Dirisha lao linafunguliwa ili hewa iingie.
4. Sikio langu lina shida ya kusikia.
5. Gari lenu linatereza siku hii.
6. Jino langu linaniuma.
7. Gazeti letu lina habari nyingi.
8. Shamba lako limelimwa vizuri.
9. Dawati lenu limevunjika.
10. Soko lao linajaa watu.

## 2.4. Matumizi ya lugha

**Kazi ya 7:**

**Mwambie mwenzako namna mnavyofanya usafi  shuleni kwako.**

## 2.5. Kusikiliza na kuzungumza

**Kazi ya 8:**

**Jadili kuhusu** "Uhifadhi wa vifaa vya shule"

## 2.6. Kuandika

**Kazi ya 7:**

**Tunga kifungu cha habari kwa kutumia kichwa kifuatacho (maneno yasiyopungua mia moja): "Uchafu shuleni ni asili ya maradhi mengi"**

# SOMO LA 3: VIONGOZI WETU SHULENI



**Kazi ya 1:**

**Tazama mchoro hapo juu kisha uzungumzie yale unayoyaona.**

## 3.1. Kusoma na ufahamu: Viongozi wa shule na wajibu wao

**Soma kifungu cha habari hapo chini kisha jibu maswali yanayofuata**

Mimi ninaitwa Kwizera. Ninasoma kidato cha  nne. Shule yetu inaitwa shule ya Sekondari ya Gikondo.

Kayitare ni kiranja wa darasa letu. Yeye hutuwakilisha katika mikutano mingi ya shule. Katika mikutano na mkuu wa shule, yeye huuliza maswali mazuri kwa sababu yeye ni mwanafunzi hodari sana. Mimi ninaelewa vizuri masomo yote; Kiswahili, Kinyarwanda, Kiingereza, Hisabati, Jiografia, Historia na mengine kwani shule yetu ina viongozi wazuri.

Mkutubi hufanya kazi maktabani ambapo vitabu vyetu huhifadhiwa kwani. Shule yetu ina vitabu vingi. Mwalimu wa taaluma kila asubuhi, hutukagua ikiwa tumevaa sare. Yeye pia hutushauri kupenda masomo yetu, kusaidiana na kufanya kazi kwa bidii. Yeye hupanga masomo ya kila muhula. Mwishoni mwa kila muhula, sisi hufanya mitihani. Mhasibu wa shule hupokea karo za wanafunzi. Mwalimu wa nidhamu huwaadhibu wanafunzi wanaofanya makosa: wanafunzi watukutu, wanafunzi wanaotoroka shule na wale wanaopiga kelele darasani.

Mwalimu mshauri wa wasichana, huchunguza nidhamu ya wasichana. Yeye hutatua shida zao shuleni, hutushauri kuwa na mwenendo mzuri, huchunguza wakati wa kuingia mabwenini na kadhalika. Mwalimu mshauri wa wavulana huchunguza nidhamu ya wavulana na kupanga michezo shuleni kwa kushirikiana na mwalimu mshauri wa wasichana.

Wakati wa chakula cha mchana na chakula cha jioni, walimu wa zamu huingia bwaloni kuchunguza chakula chetu na kutushauri kuheshimiana wakati wa kula. Mimi nawapenda sana viongozi wetu shuleni.

## Kazi ya 2:

### Maswali ya ufahamu

1. Kwizera anasomea wapi?
2. Yeye anasoma kidato gani?
3. Fafanua umuhimu wa maktaba kwa mwanafunzi.
4. Je, Kwizera anaelewa vizuri masomo yake? Eleza.
5. Viongozi wao ni wepi?
6. Eleza kazi zinazofanywa na mhasibu.
7. Mwishoni mwa kila muhula wanafunzi hufanya nini?
8. Nini wajibu wa kiranja?
9. Mkuu wa shule anaitwa nani na ana majukumu gani?
10. Walimu wa zamu huingia bwaloni kufanya nini?

## 3.2. Msamiati kuhusu mazingira ya shule

**Kazi ya 3:**

**Oanisha maneno ya kundi A na maana yake katika kundia B**

| | |
|---|---|
| 1. Shule | a. Kundi la watu wanaoishi mahali pamoja kama familia. |
| 2. Kaya | b. Mkusanyiko wa watu wanaoishi pamoja katika eneo moja la kijiografia. |
| 3. Jamii | c. Sehemu ya watu wengi kulikojengwa nyumba nyingi na kunakofanyika shughuli mbalimbali. |
| 4. Mji | d. Sehemu wanakopata maarifa na ufahamu. |
| 5. Ratiba | e. Orodha ya mpangilio wa namna mambo yatakavyofuatana katika shughuli fulani. |

## 3.3. Sarufi: Matumizi ya umoja na wingi wa majina ya ngeli ya li-ya

**Kazi ya 4:**

**Tazamasentensizifuatazonakuzungumziamabadilikoyanayojitokeza kutoka sehemu A kwenda sehemu B**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| Yai hili lilikuwa zuri. | Mayai haya yalikuwa mazuri. |
| Jani hili limepukutika. | Majani haya yamepukutika. |
| Jicho hili lanaumwa. | Macho haya yanaumwa. |
| Ini hili lilikuwa tamu. | Maini haya yalikuwa matamu. |
| Ua hili lilichanua. | Maua haya yalichanua. |

**TNBH:** Kuna majina ya ngeli hii yasiyokuwa na umoja kama vile :

Maji, mate, maziwa (ya kunywewa), mateso, manukato, mazishi, matumizi, manufaa, masafa.

Katika sentensi, majina ya ngeli hii hufuatwa na kitenzi chenye kiambishi awali li- katika umoja na ya- katika wingi.

**Mfano:**

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| 1. | Shirika **li**liundwa. | Mashirika yaliundwa. |
| 2. | Koti **li**ngesafishwa. | Makoti yangesafishwa. |
| 3. | Chungwa **li**liangushwa. | Machungwa yaliangushwa. |

**Maelezo muhimu**

Majina mengi ya ngeli ya **li-ya** hufanya wingi wake kwa kuongeza kiambishi awali **ma-** mwanzoni mwa neno.

### Kazi ya 5:

**Weka sentensi hizi kati wingi au umoja:**

a. Zoezi hili halieleweki.

b. Shamba la mjomba ni jipya.

c. Yai lililoharibika halifai kwa afya ya mwanadamu.

d. Gari lililoharibika halipendezi.

e. Matope yamechafua nguo zangu.

f. Jeshi limemshinda adui.

g. Juma la kazi limemalizika.

h. Magurudumu ya gari yanaviringika kasi.

i. Hekalu limejengwa vizuri.

j. Majamvi yaliliwa na panya.

## Kazi ya 6:

**Chunguza sentensi hizi kutoka sehemu A na sehemu B uziunganishe ili ziwe sentensi kamili**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Mhasibu wa shule | a. Hutunza barua ziingiazo shuleni pamoja na kumbukumbu nyingine zihusuzo shule. |
| 2. Shule yetu ina | b. hufanya mitihani. |
| 3. Mwishoni mwa kila muhula sisi | c. wavulana na wasichana. |
| 4.Karani wa shule | d. huchunguza nidhamu ya wavulana. |
| 5. Mwalimu mshauri wa wavulana | e. hukagua kama wanafunzi wamelipa ada ya shule. |

## 3.4. Matumizi ya lugha: Vyeo vya viongozi shuleni

## Kazi ya 7:

**Husisha maneno kutoka sehemu A kwenda sehemu B**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Kiranja wa darasa | a. makamu wa mkuu wa shule. |
| 2. Naibu mkuu wa shule | b. mwalimu anayehusika na shughuli za kila siku kuhusu darasa alilopewa. |
| 3. Mwalimu wa darasa | c. kiongozi wa wanafunzi darasani. |
| 4. Mwalimu wa chakula | d. mtaalamu wa hesabu za fedha. |
| 5. Mhasibu | e. mwalimu anayehusika na lishe ya wanafunzi shuleni. |

## 3.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Kazi ya 8:**


**Zungumzia kuhusu shule uliposomea kidako cha tatu.**

## 3.6. Kuandika

**Kazi ya 9:**

**Andika kuhusu umuhimu wa  kuwa na viongozi katika jumuia zetu**

# SOMO LA 4 : RATIBA YA WIKI YA MWANAFUNZI




**Kazi ya 1:**

**Tazama michoro hapo juu, tambua kazi zinazofanywa na utaje umuhimu wa kazi hizo**

## 4.1. Kusoma na ufahamu: Ratiba ya shughuli za kila siku katika Shule ya Gasozi

**Soma kifungu cha habari hapo chini kisha jibu maswali yanayofuata**

Gasimba ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza kwenye shule ya Gasozi. Yeye ni mwanafunzi mwenye bidii na hachelewi shuleni. Jumatatu, Gasimba huamka saa kumi na moja na nusu alfajiri na kuanza kujiandaa kwenda shuleni. Baadaye, yeye hupiga meno yake mswaki, huchana nywele na kuvaa sare yake.

Mamake Gasimba huamka mapema zaidi ili kumwandalia mwanawe kifunguakinywa. Gasimba hunywa chai kwa mkate kisha hubeba mkoba wake wenye madaftari na vitabu vyake kuelekea shuleni. Gasimba humuaga mamake na kuondoka. Gasimba hufika shuleni saa kumi na mbili na nusu na kuingia darasani na kuanza kusoma. Yeye huwatangulia wanafunzi wengine.

Saa mbili kasorobo kengele hulia na wanafunzi wote huenda kwenye gwaride ambapo wao husali na baadaye wakaimba wimbo wa taifa la Rwanda. Mwalimu mkuu huwahutubia wanafunzi kisha humpisha mwalimu wa zamu kuwapa wanafunzi matangazo muhimu.

Saa mbili kamili, somo la kwanza huanza. Baada ya vipindi viwili wanafunzi hupewa dakika ishirini za mapumziko. Chakula cha mchana huliwa saa saba kamili. Masomo huendelea kuanzia saa nane alasiri. Saa kumi na dakika ishirini masomo ya siku huwa yamekamilika. Wanafunzi wote huenda uwanjani kwa michezo mbalimbali kama kandanda, voliboli na kuruka kamba. Ifikapo saa kumi na moja na nusu wanafunzi wote huelekea nyumbani.

Gasimba afikapo nyumbani, yeye humsaidia mamake kufanya kazi za nyumbani. Baadaye, yeye hufanya kazi zake za ziada na za shuleni. Saa tatu na nusu usiku zifikapo huenda kulala.

Kila siku ya wiki huhusika na matukio haya ila siku ya Alhamisi jioni ambapo Gasimba hufanya mazoezi ya kuogelea katika bwawa la kuogelea nyumbani kwao. Ijumaa jioni, wanafunzi hushiriki katika mjadala kuhusu mada ambazo walimu wao huwa wamewachagulia. Jumamosi, Gasimba humsaidia mamake kufanya kazi za nyumbani. Jumapili, Gasimba huendelea na mapumziko kama kawaida. Baada ya kupumzika, Gasimba hujitayarisha kwa ajili ya kwenda shuleni Jumatatu.

**Kazi ya 2:**

**Maswali ya Ufahamu**

1. Gasimba anasomea katika shule gani?
2. Je, Gasimba yuko katika kidato kipi?
3. Gasimba hufanya nini anapoamka kabla ya kustaftahi?
4. Baina ya Gasimba na mamake, nani huamka mapema zaidi?
5. Gasimba hufanya nini afikapo shuleni kabla wanafunzi wengine wafike?
6. Gasimba na wanafunzi wenzake hufanya nini Alhamisi na Ijumaa jioni baada ya masomo yao?
7. Gasimba hufanya nini Jumamosi?
8. Taja shughuli za Gasimba za siku ya Jumapili?

## 4.2. Matumizi ya msamiati

**Kazi ya 3:**

**Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo:** (ratiba, kuogelea, mjadala, huchana nywele na mapumziko)

## 4.3. Sarufi: Matumizi ya vivumishi vya kuonyesha vya ngeli ya LI-YA

**Kazi ya 4:**

**Tazama sentensi zifuatazo na kuzungumzia mabadiliko yanayojitokeza kutoka sehemu A kwenda sehemu B**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Bega hili limepambwa nyota za kijeshi. | a. Mabega haya yamepambwa nyota za kijeshi. |
| 2. Gari hili ni jipya. | b. Magari haya ni mapya. |
| 3. Jengo hili ni la hospitali. | c. Majengo haya ni ya hospitali. |
| 4. Pazia hili ni Safi . | d. Mapazia haya ni safi. |

## 4.4. Matumizi ya lugha: Shughuli za kila siku za mwanafunzi

### Kazi ya 5:

Husisha sentensi kutoka sehemu A kwenda sehemu B na kuunda sentensi kamili

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Mwanafunzi huamka saa kumi na moja na nusu na | a. kisha huenda bafuni kuoga. |
| 2. Amina husali kwa dakika ishirini | b. kuanza kujiandaa kwenda shuleni. |
| 3. Gasimba hufika shuleni saa moja | c. huwasaidia wazazi kufanya kazi. |
| 4. Mwanafunzi afikapo nyumbani | d. walimu wao huwa wamewachagulia. |
| 5. Ijumaa jioni wanafunzi hushiriki katika mjadala kuhusu mada ambazo | e. akaingia darasani na kuanza kusoma. |

## 4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

### Kazi ya 6:

**Eleza kwa ufupi kuhusu shughuli uzifanyazo shuleni unakosomea.**

## 4.6. Kuandika

### Kazi ya 7:

**Andika kwa ufupi kuhusu maendeleo ya shule yako.**

### Tathmini ya mada

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja vitu angalau vitano ambavyo hupatikana katika mazingira ya shule yenu.
2. Zungumzia kuhusu shughuli tatu zinazofanyika shuleni kwenu.
3. Eleza majukumu ya wafanyakazi wanne wapatikanao shuleni.
4. Tunga sentensi kumi kwa kutumia ngeli ya LI-YA katika umoja na uwingi.
5. Eleza nafasi ya kila mwanafunzi katika harakati za kuzuia ueneaji wa magonjwa shuleni.

# MADA YA 2

# MSAMIATI KUHUSU MAZINGIRA YA NYUMBANI

**Uwezo mahususi wa mada:** Kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha na kuandika matini fupifupi kwa kutumia msamiati unaofaa katika mazingira ya nyumbani.

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kutumia msamiati uhusuo mazingira ya nyumbani, mifugo na vifaa vya nyumbani,
- Kuainisha watu wa nyumbani na uhusiano wa familia,
- Kutumia majina ya ngeli ya LI- YA na vivumishi  kwa ufasaha.

## Kidokezo

1. Taja watu wote wanawopatikana nyumbani kwenu.
2. Taja sehemu kuu za nyumba.
3. Orodhesha vifaa  na mifugo wanawopatikana nyumbani.

## SOMO LA 5: MAZINGIRA YA NYUMBANI




**Kazi ya 1:**

**Tazama mchoro hapo juu kisha jibu maswali yanayofuata:**

a. Unaona nini kwenye picha hii? Eleza.

b. Kuna uhusiano gani kati ya mchoro huo na kichwa cha habari cha hapa chini?

## 5.1. Kusoma na ufahamu: Makao ya Gakuba



Mimi na rafiki yangu Rurangwa tunazoea kutembea baada ya masomo ya jioni. Siku moja tulipata gari na kuelekea kijijini.Tulipofika kijiji ambapo mzee Gakuba anaishi tuliona nyumba yake na familia yake. Mzee Gakuba, mke wake na watoto wao wawili walikuwa wanasimama mbele ya nyumba yao katika bustani.Walikuwa wakizungumza.

Tulipigwa na bumbuazi kwa sababu kabla ya kuenda likizoni hapo palikuwa na nyumba ya msonge. Mapendekezo ya serikali ya Rwanda ni kuishi katika nyumba za kisasa. Nyumba hii ina sehemu kuu zifuatazo: sebule,vyumba vya kulala, chumba cha wageni, chumba cha vyombo, na jikoni. Nyumba hii inajengwa kwa mchanga, saruji, vyuma, nondo, milango, madirisha, mawe, matofali na mabati. Vifaa vyote hivi vinapatikana nchini Rwanda. Kwa kujenga nyumba hii kuna: msingi, kuta, zege, paa, madirisha, milango, sakafu, dari, bomba na kadhalika. Nyumba hii ina bustani na miti ya aina tofauti kama vile mti wa machungwa na mti wa maembe. Tulitazama nyumba hiyo kwa makini na kujiuliza mengi kuhusu mabadiliko ya muda mfupi.

Tulichunguza gharama za ujenzi wa nyumba yake! Na kujiuliza Je, gharama hizi zimetoka wapi? Gakuba na bibi yake, kwa ushirikiano wao walitumia fedha za mkopo kutoka benki. Gharama za nyumba ni thamani ambayo unapaswa kuilipa ili uweze kuipata nyumba hiyo unayoitaka! Sasa thamani unaweza kuilipa kwa njia ya pesa, nguvu ya kazi yako, nguvu ya akili na pesa. Ina maana kwamba bila kulipa gharama stahiki huwezi kupata thamani ya nyumba ile unayoitaka. Gharama hizi unaweza kuwalipa watu wengine wanaokufanyia kazi au wanaokuuzia bidhaa, lakini pia unaweza kuzilipa wewe mwenyewe kama muda na nguvu zako. Bila kulipa gharama stahiki huwezi kupata nyumba hiyo.

Mara moja, Rurangwa alianza kuniuliza: “ je, unaona tofauti kati ya nyumba za jadi na nyumba za kisasa?” Jibu langu lilikuwa hivi: “ kwanza ni vibaya kwa maisha ya mtu anayeishi katika nyumba za msonge kwa sababu usafi wa nyumba hizi si kazi rahisi. Nyingi zinajengwa kwa majani. Tena ni hatari sana kuishi katika nyumba ya msonge: Nyumba hii inaweza kuangukia watu, inaweza kuungua kwa sababu kunatumiwa majani kwa ujenzi wa nyumba hii, na kadhalika. Tunahifadhi mazingira wakati tunapojenga nyumba za kisasa kuliko ujenzi wa nyumba za jadi. Je, Rurangwa, unafahamu umuhimu wa kuhifadhi mazingira wakati tunapojenga nyumba?” Rurangwa anatoa jibu: “Hatuwezi kuorodhesha umuhimu wa mazingira kwa sababu bila mazingira viumbe vyote haviwezi kuishi. Kuna mashirika mengi nchini Rwanda yanayotetea uhifadhi wa mazingira. Bila mazingira hakuna maisha. Binadamu na wanyama hupumua hewa nzuri kutoka kwenye mazingira. Tunapata mvua kwa sababu mazingira yanahifadhiwa na kadhalika.”

Tulipomaliza matembezi yetu, tuliamua kuelezea wazazi wetu umuhimu wa kuishi katika nyumba nzuri kwa kutumia vifaa ambavyo vinapatikana nchini mwetu na kutumia fedha kutoka benki kwa njia ya mkopo. Na sisi kama wanafunzi tutaunda klabu zitakazofundisha watu umuhimu wa kuishi mahali pazuri na kuhifadhi mazingira.

### Kazi ya 2 :

**Maswali ya ufahamu**

1. Taja majina ya watu wote wanaotajwa katika kifungu hiki.
2. Familia ya Gakuba ina watu wangapi? Orodhesha watu hao.
3. Kwa kujenga nyumba yao, walitumia vifaa gani? Kutoka wapi?
4. Nyumba hii ilijengwa na nani? Toa maelezo.

5. Je, Mtu mwenye uwezo mdogo wa kiuchumi anaweza kuishi katika nyumba ya kisasa? Eleza.
6. Kwa sababu gani tunatakiwa kuheshimu mazingira wakati tunapojenga nyumba?
7. Kama mwanafunzi wa mwaka wa kwanza, msaada wako ni upi kwa kuhifadhi mazingira unamoishi?

## 5.2. Matumizi ya msamiati

### Kazi ya 3:

**Tumia maneno yafuatayo katika sentensi zako ukizingatia namna yalivyotumiwa katika kifungu cha habari ulichosoma**

1. Busitani
2. Bumbuazi
3. Mkopo
4. Kuhifadhi
5. Shirika
6. Kupumua
7. Kutetea
8. Klabu

### Kazi ya 4:

**Oanisha maneno yaliyomo katika sehemu A na yale yaliyomo katika sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Msingi | a. Sakafu ya juu ya nyumba iliyo baina ya paa na kuta za nyumba. |
| 2. Ukuta | b. Kifaa cha chuma , saruji au plastiki chenye uwazi ambacho aghalabu hufukiwa chini na kupitisha maji au mafuta. |
| 3. Zege | c. Mojawapo ya sehemu au pande za nyumba zinazosimama wima. |
| 4. Dari | d. Kitako cha nyumba ambapo nyumba hujengwa. |
| 5. Sakafu | e. Mchanganyiko mzito wa kokoto, mchanga, saruji na maji. |
| 6. Bomba | f. Eneo la chini aghalabu katika nyumba lakini pia hata nje ya nyumba ambalo hujengwa kwa mawe na mchanga uliochanganywa na saruji. |

## 5.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya LI-YA.

**Kazi ya 5:**

**Chunguza sentensi zifuatazo na kuandika viambishi nafsi vinavyopatikana katika vitenzi**

1. Kundi la wanamuziki liliwatumbuiza watu jana.
2. Mashirika haya yaliundwa na vijana mbalimbali.
3. Koti hilo limeshonwa na mshonaji hodari.
4. Makabati yalitengenezwa na maseremala.
5. Gari zuri lile lilitengenezwa nchini Rwanda

**Maelezo muhimu**

- Vitenzi vilivyomo katika sentensi hapo juu, vinatumia viambishi nafsi LI-YA
- Matumizi ya viambishi hivi LI-YA yanategemea nomino zilizotumiwa katika sentensi hizo.
- Nomino hizo zikiwa katika umoja kitenzi huchukua LI; zikiwa katika wingi kitenzi huchukua YA.
- Nomino zilizopendekezwa katika umoja huchukua wingi wake kwa kuongeza ma- kwa jina hilo:

**Mfano:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Kundi | makundi |
| 2. | Shirika | mashirika |
| 3. | Jani | majani |
| 4. | Gari | magari |
| 5. | Darasa | madarasa |

**Tanbihi**: Kuna majina ya ngeli hii yasiyokuwa na umoja.

***Maji, mate, maziwa (ya kunywewa), mateso, mavi, manukato, mazishi, matumizi, manufaa, masafa.*** Katika sentensi, majina ya ngeli hii hufuatwa na kitenzi chenye kiambishi awali **li-** katika umoja na **ya-** katika wingi

**Mfano:**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Shirika **li**liundwa. | Mashirika yaliundwa. |
| 2. Koti **li**ngesafishwa. | Makoti yangesafishwa. |
| 3. Chungwa **li**liangushwa. | Machungwa yaliangushwa. |

## 5.4. Matumizi ya lugha

**Kazi ya 6:**

**Tunga sentensi sahihi kwa kutumia nomino hizi katika umuja na wingi kisha ueleze kile ulichokigundua**

**Umoja** **Wingi**

1. Kabati ..........................................................
2. Koti ..............................................................
3. Bega .............................................................
4. Goti ..............................................................
5. Panga ..........................................................
6. Janga ...........................................................
7. Jangwa ........................................................
8. Jina ...............................................................
9. Jibu ...............................................................
10. Jembe…………………………………………

**Kazi ya 7:**

**Andika sentensi zifuatazo katika umoja au wingi.**

1. Mimi nina lengo la kupambana na jangwa.
2. Wewe utaondoa jani kavu hilo.
3. Majani yalikauka.
4. Shavu linaniuma.
5. Kijana mrefu alibeba kasha kwenye bega.
6. Debe hilo linavuja kwa sababu limetoboka.
7. Watoto watano walilazwa hospitalini kwa sababu ya matatizo ya mapafu.

8. Madaftari yanapaswa kuhifadhiwa vizuri.
9. Tarumbeta lilitumiwa wakati wa burudani.
10. Shirika la reli liliagiza garimoshi kubwa.

## 5.5. Kusikiliza na kuzungumza

**Kazi ya 8:**

**Simulia mbele ya darasa muhtasari wa kifungu " Makao ya Gakuba."**

## 5.6. Kuandika


**Kazi ya 9:**


**Tunga kifungu cha mistari 12 kuhusu ujenzi wa nyumba ya wazazi wako.**


# SOMO LA 6: MSAMIATI KUHUSU WATU WANAOPATIKANA NYUMBANI


**Kazi ya 1:**

**Chunguza michoro hii kisha ujadili unachoona kwenye michoro hii.**









## 6.1. Kusoma na ufahamu: Watu wa nyumbani



Familia ni jamaa ya watu wanaoishi pamoja yenye baba , mama na watoto. Katika utamaduni wetu kama Wanyarwanda, watu hawa wana majukumu tofauti katika familia.

Baba pamoja na mama wana majukumu ya kutafuta maendeleo ya familia yao. Baba kwa ushirikiano na mama wana wajibu wa kufanya juu chini ili familia yao iweze kupiga hatua kimaendeleo na kujitegemea kikamilifu. Kulinda usalama wa nyumbani ni mojawapo wa wajibu huo. Hapa mama na baba ndio walinzi wa kwanza wa utaratibu nyumbani ili familia yao iwe na amani kila wakati.

Kuwalea watoto wao, wazazi wana majukumu makubwa sana kwa watoto wao kama vile: kuwapenda, kuheshimu haki zote za mtoto na kukidhi mahitaji yao yote kama vile kuwalisha, kuwasomesha, kuwalipia karo za shule na kuwapeleka hospitalini wakati wanapoumwa, n.k.

Wazazi huwapa mawaidha mema na kuwafundisha mila na desturi za Wanyarwanda kama vile: uzalendo, ushirikiano, kuheshimiana, n.k. Wazazi pia huwasihi kuepukana na tabia za: ukatili, uongo, uovu, ulevi, uzembe, kupiga marufuku itikadi ya mauaji ya kimbari, na mienendo yote isiyofaa. Kwa upande wa watoto, nao wana majukumu ya kuwaheshimu wazazi wao, kutimiza mipango ya wazazi kama ilivyopendekezwa na kutoa mchango mwafaka wa maendeleo ya familia yao.

Nyumbani, wageni wa aina yote hukaribishwa. Miongoni mwa wageni hao ni kama babu, bibi, mjomba, shangazi, mpwa na shemeji. Wageni hawa wanalakiwa vizuri.

## Kazi ya 2:

**Maswali ya ufahamu**

1. Kwa maoni yako, eleza maana ya familia.
2. Kwa kawaida familia hujengwa namna gani?
3. Katika utamaduni wetu kama Wanyarwanda, baba na mama wanashirikiana vipi?
4. Je, mchango wa watoto ni upi katika familia?
5. Eleza mila na desturi ambazo wazazi wanafundisha watoto wao.

## 6.2. Msamiati kuhusu watu wa nyumbani

## Kazi ya 3:

**Baada ya kusoma kifungu cha habari, toa maana ya msamiati unaofuata, kisha utunge sentensi zenye maana kamili kwa kutumia msamiati huo.**

1. Majukumu
2. Ushirikiano
3. Usalama
4. Uzalendo
5. Mienendo

## Kazi ya 4:

**Oanisha maneno kutoka sehemu A na maana yake katika B**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Kukidhi | a. Hali ya kutokuwapo vita/hali ya kutokuwapo machafu yoyote. |
| 2. Amani | b. Kutimiza jambo au kitu kwa mwenye shida au kutosheleza. |
| 3. Mawaidha | c. Kuonyesha mtu kuwa unamthamini, fanyia mtu adabu. |
| 4. Kuheshimu | d. Kufanya kama ilivyotakiwa au kupangwa. |
| 5. Kutimiza | e. Maneno yenye mafunzo kuhusu mambo ya kutenda, ushauri, maonyo. |

## 6.3. Sarufi: Matumizi ya vivumishi vya idadi katika ngeli ya LI-YA

### Kazi ya 5:

**Chunguza sentensi zifuatazo, kisha ueleze muundo wa vivumishi vilivyotumiwa**

1. Jibu moja limepatikana.
2. Mawe sita yameanguka chini.
3. Matunda saba yameiva.
4. Madarasa tisa yanasafishwa.
5. Makoti kumi yatashonwa.

**Maelezo muhimu**

Katika matumizi ya ngeli ya **li-ya** na vivumishi vya idadi, idadi **mbili** ambayo hugeuka **-wili, tatu, nne, tano** pamoja na **nane** huchukua kiambishi **ma-** katika wingi. Vivumishi hivyo huwa **mawili, matatu, manne, matano** na **manane.**

Kinyume na matumizi ya ngeli ya **li-ya** na vivumishi vya idadi tulivyoona hapo juu, idadi, **sita**, **saba**, **tisa** na **kumi** havichukui kiambishi **ma-** katika wingi. Vivumishi hivyo hubaki vile vilivyo yaani, **sita**, **saba**, **tisa**, na **kumi**.

Nomino za ngeli ya **"li-ya"** huweza kutumiwa na vivumishi vya idadi ya jumla /isiyo kamili / isiyo dhahiri:

**Kwa mfano:**

Matendo <u>mengi</u> mazuri yamefanywa na watu hawa.

### Kazi ya 6:

**Andika sentensi zifuatazo kwa kutumia vivumishi vilivyomo ndani ya mabano**.

1. Mawe .................... yamewekwa kando ya barabara (tatu).
2. Madirisha .......................... yamefunguliwa (tano).
3. Meno ...................... yameng'oka (mbili).
4. Matunda ...................... yameiva (nane).

5. Makundi ................................ ya wanafunzi yameshiriki vilivyo (nne).
6. Madarasa ............................ yamejengwa (tatu).
7. Taja mambo .............. yanayozingatiwa katika kazi ya fasihi (tatu).
8. Makoti ...................... yameuzwa na mfanyabiashara huyu (tano).

**Kazi ya 7:**

**Chunguza vivumishi vya idadi isiyo dhahiri vya ngeli ya "li-ya" vifuatavyo kisha utunge sentensi zenye vivumshi hivyo.**

1. Machache
2. Mengi
3. Kadhaa
4. Tele
5. Kidogo

## 6.4. Matumizi ya lugha

**Kazi ya 8:**

**Kamilisha tungo zifuatazo kwa kutumia vivumishi vya idadi: toka moja hadi arubaini (Andika kwa maneno)**

1. Kanuni za Mungu ni ........................
2. Mwaka una miezi ............................
3. Ni rahisi kujua kwamba wiki moja ina siku .....................
4. Watu wa zamani walipika kwa kuweka chungu juu ya mafiga ...........................
5. Wanyarwanda huwapa majina watoto wao kwenye siku ya .......... .........................
6. Nchi ya Rwanda ina majimbo/ mikoa................ na mji wa Kigali.
7. Nchi yetu inapakana na nchi.......................
8. Dunia ina mabara...........................
9. Rwanda ina milima ya volkano.................
10. Katika mchezo wa soka, timu moja huwa na wachezaji.................. uwanjani.
11. Siku moja ina saa..........................

## 6.5. Kusikiliza na kuzungumza

**Kazi ya 9:**

Soma kifungu cha habari hapo juu “watu wa nyumbani” baadaye utoe muhtasari kimazungumzo.

**Kazi ya 10:**

Kwa njia ya mazungumzo, zungumzia wanafunzi wenzako ushirikiano uliopo baina ya watu wa familia yenu.

## 6.6. Kuandika

**Kazi ya 11:**

Buni, kwa kuandika, mazungumzo ya watu nyumbani wakishirikiana katika kazi fulani unayoitaka.


# SOMO LA 7: UHUSIANO WA KIFAMILIA

**Kazi ya 1:**


Tazama mchoro huu. Unaona nini kwenye mchoro huu?




## 7.1. Kusoma na ufahamu: Familia ya Rutebuka




**Picha ya 1: Rutebuka na Nyiranzage pamoja na watoto wao**




**Picha ya 2: Matabaro na Mukabutera (ni mume na mke) na mtoto wao Rubangura**




**Picha ya 3: Butera na Nyiratabaro wazazi wa Rubaduka.**

Bi. Nyiranzage aliolewa na Bw. Rutebuka. Sasa, Bi Nyiranzage anaitwa bibi Rutebuka. Wengine humwita Bi. Nyiranzage. Bwana Rutebuka ni mume wa bibi Nyiranzage. Bibi Nyiranzage na bwana Rutebuka, ni mke na mume. Bwana na bibi Rutebuka walizaa watoto wawili tu. Kifunguamimba wao ni mwanamume. Jina lake ni Matabaro. Mtoto wa pili ni mwanamke. Yeye anaitwa Nyiratabaro. Kwa upande mwingine Rutabagisha ambaye ni jirani yao amemuoa Nyiramavugo; hivyo wote huitana mume na mke. Bw. Rutabagisha na Nyiramavugo nao walizaa watoto wawili tu, mmoja wa kike anayeitwa Mukabutera ndiye aliyetangulia kuzaliwa na mwingine wa kiume Butera alifuata baadaye. Wototo wa familia hizi mbili husomea kwenye Chuo cha Ualimu cha Gacuba II.

Watoto wote ni wanafunzi wa shule za sekondari. Vifunguamimba husoma katika mwaka wa tatu katika chuo cha Ualimu cha Gacuba II. Ilhali vifungamimba husoma katika mwaka wa pili.

Baada ya muda mfupi, majirani hawa walikata shauri ya kushirikiana kimasomo. Vifunguamimba walitangulia kushirikiana na kusaidiana kati yao na hata kuwasaidia wadogo wao kimasomo na kuwahimiza kuwaiga. Walikuwa wakishika nafasi ya kwanza kwa kila muhula wa masomo. Baada ya kuona matunda ya kushirikiana kimasomo, wote waliamua kuwasaidia wanafunzi wenzao waliokuwa wakishindwa shuleni wakifanya marudio nao. Jambo hili lilishamiri sana na kujulikana shuleni kote. Ilitokea Mkurugenzi wa shule akapata habari hii na kuwakabidhi zawadi ya kusoma mwaka mzima bila kulipa ada ya shule.

Jambo hili liliwafurahisha wazazi na kuwapongeza watoto wao kwa zawadi nono. Shuleni, walimu wote walikuwa wanatumia mfano wao ili kuwahimiza wanafunzi wengine kuwaiga.

Mwishowe, wanafunzi hawa walimaliza masomo yao na kuachia shule yao makumbusho ya milele. Walianza maisha mapya wakawa walimu mashuhuri. Baada ya miaka miwili, Matabaro na Mukabutera walifunga ndoa na kuzaa mtoto anayeitwa Rubangura. Punde si punde, Butera na Nyiratabaro walioana wakazaa mtoto anayeitwa Rubaduka. Familia hizi ziliendelea kuishi pamoja na kushirikiana katika shughuli zote za nyumbani.

## Kazi ya 2:

**Maswali ya ufahamu:**

1. Taja uhusiano uliopo baina ya Butera na Mukabutera.
2. Bi. Nyiramavugo atamwitaje Mukabutera?
3. Bw. Rutebuka atamwitaje Matabaro?
4. Jaza mapengo kwa neno faafu:
   a. Bw. Rutebuka ni …………… wa Bi. Nyiranzage.
   b. Mukagatera ni ………….. yake Butera.
   c. Rutebuka ni ………….. yao Matabaro na Nyiratabaro.
5. Nyiramavugo atamwitaje mke wa Butera?

## Kazi ya 3:

**Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia msamiati wa uhusiano wa kifamilia unaofaa.**

1. Mama ya mama yangu anaitwa………………………
2. Ndugu wa kike wa baba yangu anaitwa ………………
3. Baba ya mume wangu anaitwa …………………………
4. Mtoto wa mtoto wangu anaitwa…………………………
5. Baba ya baba yangu anaitwa ……………………………..
6. Mtoto wa mjukuu wako anaitwa …………………………
7. Mama ya mke wako anaitwa ……………………………..
8. Mwanamke aliyeolewa na babako, na ambaye si mama yako wa damu anaitwa ……………………………………………………
9. Mtoto wa kwanza kuzaliwa anaitwa ……………………………
10. Mtoto wa mwisho kuzaliwa anaitwa…………………………

**Maelezo muhimu kuhusu uhusiano wa kifamilia**

- **Mjomba**: Mvulana aliyezaliwa na dada yako au kaka ya mama yako.
- **Shangazi**: Msichana aliyezaliwa pamoja na baba yako au ndugu wa kike wa baba yako.
- **Mpwa**: Mtoto wa dada yako.

- **Binamu**: Mtoto wa mjomba wako au wa shangazi yako.
- **Shemeji**: Ni ndugu zote wa mkeo au ndugu za kiume wa mumeo.
- **Wifi**: Jina wanaloitana dada zako na mkeo.
- **Mkaza mjomba**: Mke wa mjomba wako.
- **Mkaza mwana:** Mke wa mtoto wako.
- **Mavyaa**: Jina linalotumiwa katika kuitana baina ya mke na mama mkwe wake.
- **Kifunguamimba**: Mtoto wa kwanza kuzaliwa.
- **Kitindamimba:**Mtoto wa mwisho kuzaliwa.
- **Mapacha**: Watoto wawili waliozaliwa siku moja kutokana na mimba moja.
- **Baba wa kambo**: Mwanaume aliyeoa mamako na ambaye si baba yako wa damu.
- **Mama wa kambo**: Mwanamke aliyeolewa na babako, na ambaye si mama yako wa damu.
- **Kitukuu**: Mtoto wa mjukuu.
- **Kilembwe**: Mtoto wa kitukuu.
- **Kilembwekeza/Kinying'inya**: Mtoto wa kilembwe.
- **Kitojo**: Mtoto wa kilembwekeza.

## 7.2. Msamiati kuhusu uhusiano wa kifamilia

**Kazi ya 4:**

**Eleza maneno yalopigiwa mistari katika sentensi hizi:**

1. Watoto wanaheshimu <u>**wazazi**</u> wao.
2. Tunampokea <u>**nyanya**</u> yetu nyumbani.
3. <u>**Kifunguamimba**</u> kutoka familia ya mjomba wetu anahifadhi mazingira.
4. <u>**Baba wa kambo**</u> wa Juma anamsadia mtoto mwenzake mwenye matatizo ya kutembea.
5. <u>**Binamu**</u> yenu anaunda shirika la kutetea watoto wenye matatizo.

## 7.3. Sarufi: Matumizi ya vivumishi vya kuuliza katika ngeli ya LI-YA

### Kazi ya 5:

**Chunguza sentensi zifuatazo kisha ueleze muundo wa vivumishi vilivyotumiwa.**

1. Jengo lipi ni kubwa?
2. Mapapai yapi yameiva?
3. Tukupe magunia mangapi?
4. Mashirika gani yanasaidia wakulima?
5. Wewe unataka nikupe jembe lipi?

**Maelezo muhimu kuhusu vivumishi viulizi**

Vivumishi viulizi hutumika kuuliza swali kuhusu nomino. Vivumishi hivi vinapotumiwa katika sentensi ni sharti sentensi hiyo ikamilishwe kwa alama ya kiulizi. Vivumishi viulizi ni vitatu:**-pi?, -ngapi?** na **-gani?** Vivumishi viulizi **-ngapi?** na **-pi?** huchukua viambishi vya ngeli lakini kiulizi "gani" hakichukui kiambishi chochote cha ngeli.

**Kwa mfano:**

1. Gari **lipi** linatembea?
2. Magari **yapi** yanatembea?
3. Je, nyumba yako ina madirisha **mangapi**?
4. Unapenda shirika **gani?** –
5. Unapenda mashirika **gani?**

### Kazi ya 6:

**Tumia vivumishi viulizi vilivyomo mabanoni ili kujaza sentensi zifuatazo:**

1. Jibu .............. limeishapatikana? (-pi)
2. Mawe ................. yamewekwa kando ya barabara? (-ngapi)
3. Madirisha .............. yamefunguliwa? (gani)
4. Meno ................ yameng'oka? (-pi)
5. Tunda ................ limeiva? (gani)

**Kazi ya 7:**

**Andika sentensi zifuatazo katika umoja ama wingi.**

1. Jengo lipi ni kubwa?
2. Mapapai yapi yameiva?
3. Tukupe magunia yapi?
4. Mashirika gani yanasaidia wakulima?
5. Wewe unataka nikupe jembe lipi?

## 7.4. Matumizi ya lugha

**Kazi ya 8:**

**Soma maelezo hapo juu kuhusu uhusiano wa kifamilia kisha umwambie mwenzako hali halisi ya kila mtu katika familia yako binafsi.**

## 7.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Kazi ya 9:**

**Baada ya kusoma maelezo kuhusu uhusiano wa kifamilia, zungumzia darasa ukoo wako.**

## 7.6. Kuandika

**Kazi ya 10:**

**Tunga mazungumzo kuhusu**

“ uhusiano wa kifamilia” ( angalau misitari 15)

## SOMO LA 8: VIFAA VYA NYUMBANI NA USAFI WAKE

**Kazi ya 1:**

**Orodhesha vifaa mnavyotumia nyumbani kwenu mnapofanya usafi.**

### 8.1. Kusoma na ufahamu: Vifaa vya nyumbani na usafi wake



Usafi wa nyumbani na vifaa vyake ni njia ya kuendeleza afya kwa kuzuia maradhi yanayotokana na athari za taka kwa binadamu. Athari hizo zinaweza kuhusu miili yetu.

Usafi wa nyumbani ni jambo ambalo linafaa kutiliwa maanani na kila mtu, kwani uchafu unachangia pakubwa kuharibu maisha ya binadamu. Jambo la kushangaza ni kwamba watu wengi wanafikiri kuwa usafi unahusu miili na mavazi tu, wakisahau kuwa usafi huhusu kila kitu kinachopatikana katika mazingira wanamoishi.

Tunapozungumzia usafi wa nyumbani, watu wengi huelewa shughuli muhimu zinazostahili kufanywa katika kusafisha vyumba vya nyumbani na kutengeneza bustani zinazozunguka nyumba hiyo. Lakini, ni lazima kujua kwamba usafi huchunguzwa kupitia vifaa vya nyumbani vinavyotumiwa kama vile: sahani, vikombe, vijiko, sufuria,vijiko, nguo, meza, kabati, runinga, redio,na kadhalika. Tena inafaa kusafisha sehemu zote za nyumba kama vile vyumba vya kula, sebule, jikoni, chooni, bila ya kusahau bustani.

Kabla ya kufanya usafi wa vifaa na sehemu za nyumba, sisi wenyewe tunaombwa kuwa na usafi ipasavyo. Kama vile: Kunawa mikono kwa maji

na sabuni hupunguza kwa kiasi kikubwa maambukizo ya ugonjwa wa kuhara. Wazazi na walezi wengine wanapaswa kunawa mikono kwa sabuni kila baada ya kumhudumia mtoto mchanga au mtoto mdogo aliyejisaidia, kumpeleka mtoto msalani, kutoka msalani wao wenyewe, kabla ya kuandaa chakula, kabla ya kulisha watoto wadogo na baada ya kuondoa takataka.

Wazazi na walezi wengine wanapaswa kuwajengea watoto tabia ya kunawa mikono kwa maji safi na sabuni kabla ya chakula na baada ya kutoka msalani. Kinyesi cha wanyama na binadamu kisiruhusiwe kukaa ndani ya nyumba, njiani, kwenye vyanzo vya maji na katika maeneo ya kuchezea watoto. Matumizi ya vyoo pamoja na tabia ya usafi, hasa unawaji wa mikono kwa sabuni ni mambo muhimu kwa afya ya jamii. Hutoa kinga kwa watoto na kwa kaya kwa gharama nafuu pamoja na kuwapatia watoto haki yao ya kuwa na afya njema na lishe bora.

Tunaposafisha nyumba tunatumia maji, sabuni za kawaida, na sabuni za majimaji au dawa za kuulia wadudu wenye kuambukiza watu magonjwa mbalimbali.Tunawaonya watu wasitupe uchafu ovyoovyo. Taka ambazo zinaweza kusababisha matatizo ya afya ni kinyesi cha binadamu na cha wanyama, taka ngumu, maji machafu, taka za viwandani, na za kilimo, n.k. Taka zote zinazotokana na vitu vyote vilivyotumiwa zinafaa kutupwa mahali panapofaa kama vile jalalani au zikachomwa kupitia njia zinazokubaliwa. Nyasi nazo zinazozunguka nyumba zetu zinafaa kufyekwa ili kuwafukuza mbu wanaosambaza ugonjwa wa malaria.

Maji yote ya kunywa na ya matumizi mengine yatoke kwenye vyanzo salama na yachemshwe baadaye au yanyunyiziwe dawa ya kuulia vijidudu. Vyombo vya kuwekea na kuhifadhia maji vitunzwe vizuri ndani na nje na kufunikwa ili kuepukana na uchafu wa maji. Ni lazima iwepo mikakati rahisi ya kusafisha maji yawe safi nyumbani kama vile kuyachemsha, kunyunyizia dawa ya maji (klorini) ili kuua vijidudu. Vyakula vibichi au mabaki ya vyakula vilivyopikwa yanaweza kuwa hatari. Vyakula vibichi visafishwe kwa maji safi kabla ya kupikwa. Chakula kilichopikwa kiliwe kikiwa moto na kiporo kipashwe moto vizuri kabla ya kuliwa. Chakula, vyombo na eneo la kutayarishia chakula halina budi kuwa safi na mbali na wanyama.

Chakula kihifadhiwe kwenye vyombo vilivyofunikwa.

Upungufu wa usafi wa mazingira ni sababu kuu ya maradhi kote duniani. Uboreshaji wa mazingira una manufaa makubwa kwa afya ya watu katika kaya na katika jamii.

## Kazi ya 2:

**Maswali ya ufahamu**

1. Ni sehemu zipi za nyumba ambazo huhitaji usafi?
2. Taja vifaa vya nyumbani vilivyotajwa katika kifungu hiki.
3. Kwa sababu gani watoto wanapaswa kuepukana na uchafu?
4. Tunatumia nini katika kufanya usafi wa nyumbani?
5. Wazazi au walezi wengine wanafundisha watoto wao nini kuhusu usafi?
6. Ni umuhimu gani wa kuwa na maji safi?
7. Ni dosari zipi za upungufu wa usafi kwa binadamu?

# 8.2. Msamiati

## Kazi ya 3:

**Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. Athari
2. Maanani
3. Kuhara
4. Kinga
5. Takataka
6. Kaya

## Kazi ya 4:

**Baada ya kusoma kifungu cha habari hapo juu, kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yafuatayo:** *runinga, redio, kijiko, sufuria, meza, malaria, usafi, tabia, sabuni, linafaa, vifaa.*

1. Mama anapika chakula ndani ya………………
2. Tunaposoma kiswahili nyumbani tunaandikia kwenye………..
3. Nyanya yangu anatumia………….. wakati mimi ninatumia uma.
4. Tunasikiliza habari za mpira kwenye………………
5. Wanafunzi hupenda kutazama filamu kwenye………..
6. Usafi nyumbani ni jambo ambalo ……….kutiliwa maanani.
7. Watu wengi wanafikiri kuwa ……..unahusu miili na mavazi tu.

8. Usafi nyumbani huonekana kupitia .......... vinavyotumiwa nyumbani.
9. Kunawa mikono kwa maji na ...........hupunguza kwa kiasi kikubwa magonjwa.
10. Wazazi na walezi wengine wanapaswa kuwazoeza watoto .......... ya kunawa mikono kwa maji safi.
11. Nyasi nazo zinazozunguka nyumba zetu zinafaa kukatwa ili kuwafukuza mbu wanaosababisha ugonjwa wa.............

## 8.3. Sarufi: Nomino za ngeli ya LI-YA na vivumishi vya kumiliki

**Kazi ya 5:**

**Chunguza mifano ya sentensi hapa chini, kisha ueleze aina za maneno yaliyopigiwa mstari.**

1. Koti **langu** limechafuka.
2. Shirika **lako** linajulikana sana.
3. Gari **lake** ni la kifahari.
4. Jumba **letu** linapendeza

**Maelezo muhimu kuhusu matumizi ya nomino za ngeli ya LI-Ya na vivumishi vya kumiliki**

Vivumishi vya kumiliki ni **-angu, -ako, -ake, -etu, -enu** na **-ao.** Vivumishi hivi katika ngeli ya **Li-Ya** huchukua kiambishi konsonanti **l-** katika umoja na **y-** katika wingi.

**Kazi ya 6:**

**Andika wingi wa sentensi za hapa chini.**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Jembe langu limepotea. | ------------------------------------------ |
| 2. Janga kubwa limesababisha maafa. | --------------------------------- |
| 3. Jaribio la leo limesahihishwa. | ------------------------------------------ |
| 4. Jeshi lao lina askari wengi. | ------------------------------------------ |
| 5. Jeraha lake lina uchafu sana. | ------------------------------------------ |
| 6. Jambo hili liliwafurahisha wengi. | --------------------------------------- |
| 7. Jicho lake linaona mbali sana. | ----------------------------------------- |
| 8. Jiwe langu lina thamani kubwa. | ----------------------------------------- |

9. Jino lako limeng'oka? -----------------------------------------

10. Jiko langu limeharibika. -----------------------------------------

## 8.4. Matumizi ya lugha

### Kazi ya 7:

**Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili jadilini kuhusu "Umuhimu wa usafi  na madhara ya kutokuwa na usafi."**

### Kazi ya 8:

**Eleza umuhimu wa vifaa hivi vya usafi:**

1. Bafu
2. Sabuni
3. Deki
4. Ufagio
5. Taulo

## 8.5. Kusikiliza na Kuzungumza

### Kazi ya 9:


**Mwambie mwenzako namna mnavyofanya usafi  nyumbani kwenu na usafi wa vifaa vya nyumbani.**

## 8.6. Kuandika

### Kazi ya 10:

**Tunga kifungu cha habari kwa kutumia kichwa kifuatacho (maneno yasiyopungua mia moja): "Uchafu ni asili ya maradhi mengi."**


## SOMO LA 9: MSAMIATI KUHUSU MIFUGO



**Kazi ya 1:**

**Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Kumbushaneni majina ya mifugo mbalimbali mnayoyajua.**

### 9.1. Kusoma na ufahamu: Kazi nzuri ya ufugaji.



Huyu ni Ikirezi. Ikirezi ni mfugaji wa nyuki. Ikirezi anarina asali. Baada ya kurina, yeye husafisha asali yake na kuiuza. Asali hiyo hutumiwa kama chakula au hutengenezewa dawa.



Huyu ni Gabiro. Gabiro anakata sufu. Sufu ya kondoo hutumiwa kutengenezea nyuzi za kufumia nguo.



Huyu ni Ituze. Ituze anakama ng'ombe. Kabla ya kukama, aliosha chuchu kwa maji vuguvugu na kuzikausha kwa kitambaa safi. Anatumia mkebe safi kuwekea maziwa. Ituze  huwapandisha madume kwa mitamba au mpira.



Hili ni josho. Ng'ombe hawa wanaogeshwa kwa dawa ndani ya josho. Wafugaji huosha mifugo katika josho ili kuwakinga dhidi ya kupe. Dawa huua viroboto wanaoishi kwenye ngozi za mifugo.



Hawa ni Mudenge na Gatera. Mudenge anawalisha kuku kwa mahindi. Pia, huwapa kuku mtama, ugali, wadudu na vyakula vinavyopatikana kwa urahisi. Wakati mwingine, yeye huwapa kuku chakula maalumu kilichotengenezewa katika viwanda. Mudenge anawafuga kuku wa mayai na wa nyama. Yeye huuza baadhi ya mayai ili kujipatia riziki. Mudenge, pia, huwaatamisha baadhi ya kuku wake ili apate vifaranga wa kuuza na kufuga.

Gatera, naye, anawalisha ng'ombe kwa nyasi. Gatera anawafuga ng'ombe wake ndani kwa ndani. Anawapa lishe, maji na dawa humo humo zizini. Gatera hukata pembe za ng'ombe wake. Ng'ombe hukatwa pembe ili kumzuia kumdhuru mtu au kuharibu vitu.



Huyu ni Kaliza. Kaliza anapenda kuchunga farasi. Anawachunga farasi penye maji safi na nyasi nyingi. Kulisha mifugo ni shughuli muhimu ya ufugaji. Mifugo wanapolishwa vizuri hukua kwa haraka, huwa na afya nzuri na hutupatia mapato mazuri.



Kaliza anafagia zizi la ng'ombe. Mfugaji bora husafisha makao ya mifugo na vyombo vyao vya kulia, kunywea na kulalia. Mifugo wanaolala katika mahali safi na kulia katika vyombo safi huwa na afya njema.



Daktari wa mifugo anamtibu kuku kwa kumdunga sindano. Kutibu mifugo ni muhimu kwa mfugaji. Ni vizuri kutambua dalili ya ugonjwa ili watibiwe mapema.

**Kazi ya 2:**

**Maswali ya ufahamu**

1. Andika majina yote ya mifugo yaliyotajwa hapo juu.
2. Asali ina umuhimu gani kwa maisha ya binadamu?
3. Kwa sababu gani tunakata sufu ya kondoo?
4. Kabla ya kukama ng'ombe, tunaombwa kufanya nini kwanza?
5. Chagua mifugo watano katika vifungu vya habari hapo juu kisha utaje umuhimu wao kwa binadamu.
6. Kwa maoni yako, ufugaji unaleta matunda gani kwa maendeleo ya nchi?

## 9.2. Msamiati kuhusu mifugo

**Kazi ya 3:**

**Baada ya kusoma kifungu cha habari hiki, toa maana ya msamiati unaofuata:**

- kurina
- kukata sufu
- kukama
- kupandisha madume kwa mtamba
- kufuga ng'ombe ndani kwa ndani
- kuwapeleka ng'ombe katika josho
- kuatamisha kuku
- kuchunga
- kukata pembe

## Kazi ya 4:

**Oanisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Asali | a. Manyoya ya kondoo yatumikayo kutengeneza nyuzi. |
| 2. Sufu | b. Kitu ambacho mtu anaweza kuwa nacho baada ya kufanya kazi au biashara. |
| 3. Kufuma | c. Kuunda kitambaa kwa kupitisha nyuzi ndefu juu na chini kwa kutumia sindano au mashine. |
| 4. Chuchu | d. Mlo bora wenye virutubisho vya kujenga mwili kama vile : madini , protini, …. |
| 5. Josho | e. Dimbwi maalumu lililotiwa dawa ya kuogeshea wanyama ili kuwakinga na kupe. |
| 6. Lishe | f. Sehemu ya ziwa la binadamu au mnyama ambayo hukamwa. |
| 7. Pato | g. Kitu kiowevu kitamu ambacho hutengenezwa na nyuki. |

## 9.3. Sarufi: Ngeli ya LI –YA na Vivumishi vya kuonyesha.

## Kazi ya 5:

**Tazama sentensi zifuatazo na kujadili mabadiliko ya kisarufi yanayojitokeza.**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Gari hili ni jipya | a. Magari haya ni mapya. |
| 2. Tunda hilo limeoza. | b. Matunda hayo yameoza. |
| 3. Kundi lile ni chipukizi. | c. Makundi yale ni chipukizi. |

**Maelezo muhimu**

Vivumshi vya kuonyesha **hili, hilo, lile** hufuata nomino katika umoja.

Vivumishi vya kuonyesha **haya, hayo**, **yale** hufuata nomino katika wingi.

### Kazi ya 6:

**Chagua neno sahihi katika mabano na kujaza pengo.**

1. Debe ………….. lilitoboka (hii, haya, hili, hiyi).
2. Jambazi ……….liliadhibiwa (yule, hii, lile, hiyo).
3. Tafadhali kunja majamvi………..(ayo, hizo, hayo, halo).
4. Anakuomba umnunulie machungwa ………….(hizo, hayo, yayo).
5. Jahazi …….ni kubwa (lili, hile, jile, lile).

### Kazi ya 7:


**Sahihisha sentensi zifuatazo:**

1. Kabati kale kalivunjwa na wezi.
2. Maji haya alimwagwa ovyo sakafuni.
3. Alipotaka kujenga nyumba alitafuta majiwe makubwa.
4. Mafuta haya haamwagwi ziwani kwa sababu anaweza kuua samaki.
5. Maboga haya yana manufaa nyingi kwa mwili wako.

## 9.4. Matumizi ya lugha

### Kazi ya 8:

**Husisha majina haya na mifugo wanaopatikana hapo chini: mbuzi, mbwa, kuku, paka, na sungura.**



## 9.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

**Kazi ya 9:**

**Zungumzia wanafunzi jinsi mnavyofanya ufugaji wengine namna gani nyumbani kwenu au kwa babu yako mnavyofanya ufugaji.**

## 9.6. Kuandika

**Kazi ya 10:**

**Tunga kifungu kifupi cha maneno yasiyozidi 100 kuhusu "Umuhimu wa ufugaji nchini Rwanda."**

## Tathmini ya mada

1. **Tumia maneno yafuatayo ya ngeli ya LI-YA na vivumishi vya kumiliki au vya kuonyesha katika sentensi sahihi katika umoja.**
   a. Azimio
   b. Ini
   c. Jiko
   d. Ua
   e. Shamba
2. **Tumia sentensi za hapo juu katika wingi.**
3. **Jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno: baba, wifi, mama, shangazi, mjomba, mjukuu, binamu, mpwa, mapacha, baba wa kambo.**
   a. Mke wa baba yako ni ………………………………….. yako.
   b. Mume wa mama yako utamuita……………………… yako.
   c. Mtoto wa mjomba au shangazi yako ni……………..
   d. Mtoto wa mtoto wako utamuita…………..
   e. Bwana ya mama yako ambaye si baba yako utamuita……..
   f. Dada ya baba yako utamuita………………………………
   g. Kaka ya mama yako utamuita……………………………..
   h. Mke wa ndugu yako utamuita…………………………….
   i. Watoto wawili waliozaliwa siku moja na mama mmoja tutawaita……..
   j. Mtoto wa dada yako utamuita………

4. **Andika umuhimu wa vifaa vya nyumbani vifuatavyo:**

| Kifaa | Umuhimu |
|---|---|
| Sufuria | |
| Kikombe | |
| Kabati | |
| Sabuni | |
| Kiti | |

5. **Tunga insha ndogo ya maneno yasiyozidi 100 kuhusu "Umuhimu wa kuishi katika nyumba ya kisiasa kwa maisha ya binadamu"**

MADA YA 3

# MSAMIATI KATIKA MAZINGIRA YA HOSPITALI

**Uwezo mahususi katika mada hii:**

Kuzungumza na kuandika kwa ufasaha matini fupifupi kwa kutumia msamiati unaofaa katika mazingira ya hospitalini.


**Malengo ya Ujifunzaji:**

- Kutumia kwa ufasaha msamiati maalum wa mazingira ya hospitali katika mawasiliano;
- Kueleza vifaa vya hospitalini na umuhimu wake,
- Kubainisha wafanyakazi wa hospitalini na majukumu yao,
- Kusikiliza kwa makini na kusoma kwa ufasaha kifungu cha habari kinachohusika,
- Kunyambua vitenzi kwa kuzingatia kauli mbalimbali.

## Kidokezo

1. Hospitali ni nini?
2. Orodhesha angalau hospitali tatu muhimu zinazojulikana nchini Rwanda.
3. Taja vifaa vitano vinavyotumiwa hospitalini na kueleza umuhimu wake.
4. Bainisha wafanyakazi angalau wanne wapatikanao hospitalini na kuainisha kazi au majukumu yao.

## SOMO LA 10: SEHEMU ZA HOSPITALI




**Kazi ya 1:**

**Tazama kwa makini mchoro hapa juu. Zungumzia vitu muhimu unavyoona vyenye uhusiano na hospitali.**

### 10.1. Kusoma na ufahamu: Ziara yetu hospitalini



*Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Maadili wamefanya ziara kwenye hospitali moja wilayani Huye. Shabaha yao ni kuielewa vyema hospitali. Wamekaribishwa na mpokezi wageni ambaye amewaongoza kwa Daktari Mkuu.*

**Daktari**: Hamjambo vijana!

**Vijana**: Hatujambo Daktari!

**Aminata**: Jina langu ni Aminata na mimi ndimi kiranja wa darasa letu. Hawa ni wanafunzi wenzangu.

Tumefurahia fursa hii ya kuitembelea hospitali yenu kwa ajili ya kuyaelewa vyema mazingira ya hospitali.

**Daktari**: Asante sana kwa nia yenu. Kwa hiyo, karibuni nyote!

Mimi ni Birashoboka, Daktari Mkuu wa hospitali hii. Na huyu ni muuguzi wetu, jina lake Veneranda.

Nifuateni sasa niwatembeze sehemu mbalimbali za hospitali.

**Muuguzi**: Tuanzie kwenye sehemu ambapo mmekaribishiwa na kupata kiti. Sehemu hiyo huitwa **pambajio**. Ni sehemu ya kuwapokelea wagonjwa.

**Pascal:** Samahani Daktari! Sisi siyo wagonjwa, msije mkatudunga sindano!

**Daktari:** Hahaaaa! Usiwe na wasiwasi kijana! Tafadhali tuendelee. Sehemu hii ni **chumba cha matibabu ya dharura**, yaani chumba cha kuwatibia wagonjwa wanaohitaji matibabu ya haraka sana kama vile majeruhi wa ajali.

**Muuguzi:** Samahani Daktari! Ni vizuri kuelewa kwamba chumba cha dharura ni tofauti na **wodi** kwani wodi ni chumba cha kushughulikia maradhi ambayo si ya kawaida kama vile maradhi ambayo yamezuka ghafla na bado hayaeleweki vizuri.

**Daktari:** Asante sana Muuguzi! Kama nyongeza, kuna wodi nyingine ambayo ni sehemu ya **kuwalaza wagonjwa** wanaoendelea na matibabu.

**Samilla:** Samahani Daktari! Kwenye mlango ule nimesoma neno maabara. Je, nini maana ya neno hili?

**Daktari:** Vizuri sana! **Maabara** ni chumba cha kufanyia uchunguzi wa magonjwa. Kwa kuwa hatuna muda wa kutosha wa kuizunguka hospitali yote, inafaa kusimamia hapa na kumwomba Muuguzi awaelezee sehemu nyingine za hospitali.

**Muuguzi:** Asante sana Daktari! Kuna **chumba cha kuhifadhia** dawa; kuna **kungawi,** yaani chumba cha kujifungulia kwa kina mama wajawazito; **chumba cha upasuaji**; chumba cha **uangalizi maalum** ambacho ni chumba cha matibabu ya kiwango cha juu sana. Hususan chumba hiki hutumiwa kwa wagonjwa walio katika hali mahututi.

**Daktari:** Chumba hiki huwa na mitambo na mashine za hali ya juu sana za kumsaidia mgonjwa.

**Muuguzi:** Chumba cha mwisho ni **ufuoni** au **makafani** ambacho hutumiwa kuhifadhia maiti.

**Jado:** Asante sana kwa maelezo haya. Ningependa sasa mtuelezee kuhusu vifaa muhimu vinavyotumiwa humu.

## Kazi ya 2:

**Maswali ya ufahamu**

***a. Soma kifungu cha habari hapa juu na kujibu maswali ya ufahamu yafuatayo*:**

1. Habari hii imetokea wapi?
2. Ni lengo gani la wanafunzi kuitembelea hospitali?
3. Ni watu gani wanaozungumziwa katika kifungu cha habari hiki?
4. Ni sehemu zipi za hospitali zilizotajwa?
5. Aminata alikuwa na wajibu gani?

***b. Chagua jibu lililo sahihi kuliko mengine***

1. Kifungu hiki cha habari kinazungumzia:

a. Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Maadili na Daktari.

b. Vifaa na wafanyakazi wa hospitali wilayani Huye.

c. Ziara ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Maadili kwenye hospitali moja wilayani Huye.

d. Mazungumzo kati ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Maadili kuhusu uchaguzi wa mchepuo wa udaktari.

2. Walipofika hospitalini, wanafunzi walikaribishwa na

a. Muuguzi.

b. daktari mkuu.

c. nesi.

d. mpokeaji.

3. wanafunzi walitembezwa sehemu za hospitali na

a. daktari mkuu.

b. muuguzi pamoja na daktari mkuu.

c. mpokezi.

d. majibu yote ni sahihi.

4. Wanafunzi walielezewa vyumba vingapi ?

a. vyumba tisa.

b. vyumba vitatu.

c. vyumba kumi.

d. vyumba vitano.

e. hakuna jibu sahihi.

5. Kungawi ni chumba cha:

a. kuwapasulia wajawazito.

b. kuzalia wajawazito.

c. kununulia dawa.

d. kulalia wagonjwa.

## 10.2. Matumizi ya msamiati kuhusu mazingira ya hospitali

### Kazi ya 3:

**Kwa kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu au njia nyingine tofauti, toa maana ya msamiati ufuatao na kuutungia sentensi sahihi.**

1. Kudunga
2. Matibabu
3. Mgonjwa
4. Hali mahututi
5. Kupenyeza
6. Kuhifadhi
7. Uchafu
8. Mjamzito
9. Kujifungua
10. Dharura

### Kazi ya 4:

**Oanisha maneno katika sehemu A na maana zake kutoka sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Kungawi | a. chumba cha kuhifadhia dawa. |
| 2. Pambajio | b. chumba cha kuhifadhia maiti. |
| 3. Chumba cha dawa | c. chumba cha kujifungulia kwa kina mama wajawazito. |
| 4. Maabara | d. chumba cha kuwapokelea wagonjwa. |
| 5. Makafani | e. chumba cha kufanyia uchunguzi wa magonjwa. |

## 10.3. Sarufi: Matumizi ya kauli za vitenzi

### Kazi ya 5:

**Soma sentensi zifuatazo na kutofautisha viambishi vilivyokolea**

Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Maadili walikuwa wanapend**ana** sana. Waliand**a** mpango wa kumwandik**ia** Daktari Mkuu wa Hospitali kwa ajili ya kuitembel**ea** hospitali yake.

**Maelezo muhimu**

Viambishi vilivyokolea ni viambishi vya mnyambuliko wa vitenzi.

Mnyambuliko wa vitenzi ni jinsi vitenzi vinavyobadilika kulingana na kauli/hali mbalimbali.

Hapo juu, kauli za vitenzi zilizotumiwa ni tatu kama ifuatavyo:

i. Kauli ya kutenda.
ii. Kauli ya kutendana.
iii. Kauli ya kutendea.

**Yafuatayo ni maelezo kwa kila aina ya kauli:**

1. Kauli ya Kutenda - kitendo katika hali yake ya kawaida (bila kunyambuliwa).
2. Kauli ya Kutendana - unamfanya mtu kitendo, naye anakufanya vivyo hivyo.
3. Kauli ya Kutendea - kufanya kitendo kwa niaba (au kwa ajili) ya mtu mwingine.

**Kazi ya 6:**

**Onyesha mnyambuliko wa vitenzi ulivyochagua kisha uviweke katika hali ya kutendea na kutendeana.**

**Kazi ya 7:**

**Tunga sentensi ambazo vitenzi vyake vinabeba kauli ya kutenda, kutendea na kutendana**

**Kazi ya 8:**

**Andika vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendea kwa kuzingatia mabadiliko ya kimaana.**

1. Tumeandika barua kwa ajili ya rafiki zetu.
2. Wazazi walifanya mema kwa niaba ya watoto wao
3. Baba yake ameweka pesa kwenye akaunti kwa manufaa ya mtoto wake.

## 10.4. Matumizi ya lugha: Sehemu muhimu za hospitali

**Maelezo muhimu kuhusu sehemu muhimu za hospitali**

Hospitali ni mahali pa kutibia wagonjwa. Kuna hospitali kubwa na nyingine ndogo. Hospitali ndogo huitwa dispensali au zahanati.

Hospitali ina sehemu muhimu zifuatazo:

1. Pambajio: Sehemu ya kuwapokelea wagonjwa.
2. Wodi: Sehemu ya kuwalaza wagonjwa wanapoendelea kupokea matibabu.
3. Kungawi: Chumba cha kujifungulia kwa waja wazito.
4. Chumba cha upasuaji: Chumba cha kufanyiwa upasuaji wa wagonjwa.
5. Wodi wa matibabu maalum: Chumba cha kushughulikia maradhi ambayo si ya kawaida k.m. maradhi ambayo yamezuka ghafla na bado hayaeleweki vizuri.
6. Chumba cha matibabu ya dharura: Chumba cha kuwatibia wale wanaohitaji matibabu ya haraka sana k.m. waathiriwa wa ajali.
7. Chumba cha matibabu ya kina: Chumba cha matibabu ya kiwango cha juu sana. Hususan hutumiwa kwa wale walio katika hali mahututi. Chumba hiki huwa na mitambo na mashine za hali ya juu za kumsaidia mgonjwa.
8. Maabara: Chumba cha kufanyia utafiti.
9. Chumba cha dawa: Chumba cha kuhifadhia dawa zitolewazo kwa wagonjwa.
10. Ufuoni/makafani: Mahali pa kuhifadhia maiti.

## 10.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Kazi ya 10:**

**Sikiliza taarifa ya habari moja kutoka redio au runinga juu ya mambo ya afya. Isimulie mbele ya darasa.**

**Kazi ya 11:**

**Kwa ushirikiano na wenzako, igiza mazungumzo hapo juu**

**Kazi ya 12:**

**Fikiria zahanati au hospitali moja uliyoitembelea, kisha zungumzia chumba kimoja ambamo uliingia na sababu za kuitembelea.**

## 10.6. Kuandika

**Kazi ya 13:**

**Chora hospitali moja na kuonyesha sehemu zake angalau nne na kueleza umuhimu wake**

## SOMO LA 11: VIFAA VYA HOSPITALINI









**Kazi ya 1:**

Tazama kwa makini mchoro hapa juu. Zungumzia vitu muhimu unavyoona vyenye uhusiano na hospitali.

## 11.1. Kusoma na ufahamu: Vifaa vya hospitalini



**Daktari:** Kabla ya kutembelea vyumba vyote ambamo mmepatikana vifaa mbalimbali, tazameni picha hizi za vifaa vipatikanavyo hospitalini. Picha hii ni ya eksrei au uyoka ambayo ni mashine ya kutazamia viungo vya ndani ya mwili.

**Muuguzi:** Hii ni machela, yaani kigari au kitanda cha kubebea wagonjwa.

**Aminata:** Tafadhali Muuguzi. Je, naweza kuwasaidia? Picha inayofuata ninajua jina lake.

**Muuguzi:** Vizuri sana! Kushirikiana katika kazi zote ni jambo muhimu sana. Fursa ni yako kiongozi wa darasa.

**Aminata:** Ile ni **mikroskopu au hadubini**. Inatumiwa kuangalia vijidudu vidogo sana ambavyo haviwezi kuonekana kwa macho tu.

**Daktari**: Hongera Aminata! Tuendelee. Hii ni **dipfriza** ambayo ni chombo cha kuhifadhia dawa katika kipimo cha baridi kali sana.

**Muuguzi**: Jiko lile hutumiwa kuchemshia vyombo ili kuulia vijidudu na bakteria.

Kifaa hiki chenye umbo sawa na soksi kinaitwa **glovu.** Kinavaliwa mkononi kumkinga muuguzi dhidi ya uchafu au kuambukizwa na maradhi.

**Daktari**: Vifaa hivi ninadhani vinafahamika kwa kila mtu. Vijana, nani ambaye anaweza kutuelezea?

**Bugingo**: Hizi ni **sindano**. Zinatumiwa kupenyezea dawa mwilini. Pembeni kuna makasi ambazo hutumiwa kwa kukatia vitu mbalimbali.

**Muuguzi**: Vijana, mpigieni makofi! **Bendeji** hii ni kitambaa cha kufungia jeraha au kidonda kisichafuliwe.

Na hii ni **plasta** ambayo ni kitambaa kigumu sana cha kufungia sehemu ya mwili iliyovunjika.

**Daktari**: Mwishoni, **koleo** hii husaidia kama kifaa cha kushikia vitu vinavyotumiwa na daktari.

## Kazi ya 2:

**Maswali ya ufahamu**

**a. Soma kifungu cha habari hapa juu na kujibu maswali ya ufahamu yafuatayo:**

1. Mazungumzo haya yametokea wapi?
2. Ni madhumuni gani ya wanafunzi kuitembelea sehemu hii?
3. Ni wahusika gani waliowasiliana?
4. Baadhi ya vifaa vilivyoonyeshwa, ni kifaa kipi ambacho kingeweza kuwatia hofu wanafunzi?
5. Daktari ametumia mbinu gani ya kuonyesha na kuelezea vifaa?

**b. Chagua jibu lililo sahihi kuliko mengine**

1. Kifungu hiki cha habari kinazungumzia:

a. Vifaa vitumiwavyo hospitalini

b. Daktari na wanafunzi

c. Ziara ya wanafunzi hospitalini

d. Hakuna jibu sahihi

2. Katika maelezo yake, Daktari ameungwa mkono na

a. muuguzi

b. kiongozi wa darasa

c. wanafunzi

d. muuguzi pamoja na wanafunzi wawili.

3. Dipfriza ni mojawapo ya:

a. Wafanyakazi wa hospitalini

b. Dawa za hospitalini

c. Sehemu za hospitali

d. Vifaa vya hospitalini.

4. Machela inatumiwa kubeba

a. Dawa za wagonjwa

b. Walemavu

c. Vifaa vya hospitalini

d. Wagonjwa hospitalini.

5. Daktari au Muuguzi anatumia bendeji

a. Kumfunga kamba mgonjwa

b. Kufungia kidonda

c. Kufungia sehemu iliyovunjika

d. Kumwezesha mgonjwa kutembeatembea.

## 11.2. Matumizi ya msamiati

### Kazi ya 3:

**Kwa kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu au njia nyingine tofauti, toa maana ya msamiati ufuatao na kuutungia sentensi sahihi.**

i. Vidudu
ii. Bakteria
iii. Kuhifadhi
iv. Jeraha
v. Kidonda

### Kazi ya 4:

**Jaza nafasi iliyoachwa wazi kwa kutafuta msamiati unaofaa kwenye upande wa maneno na maana kwenye upande wa maelezo**

| Maneno | Maelezo |
|---|---|
| | Mchanganyiko wa vitu vinavyotokana na mafuta na aina mojawapo ya magadi na ambayo hutumiwa kwa kufulia, kuogea au kusafisha vitu. |
| Machela | |
| | Kifaa kinachotengenezwa kwa madini, aghalabu ya chuma, chenye visu viwili vilivyounganishwa kwa msumari mdogo na tundu mbili za kuingizia vidole, kinachotumiwa kukatia kitu k.v. nguo au nywele. |
| | Kitu kama gome gumu kilichotengenezwa kwa unga maalumu na kitambaa kinachofungwa sehemu ya mwili iliyovunjika ili kushikanisha mifupa iliyovunjika. |

### Kazi ya 5:

**Kamilisha sentensi zifuatazo ili zilete maana kamili kwa kutumia msamiati huu: eksirei, plasta, sindano, kuhifadhia baadhi ya dawa.**

1. Kitambaa kigumu sana cha kufungia sehemu iliyovunjika huitwa......................................................
2. Dipfriza ni chombo..................................
3. ........................ni kifaa cha kupenyezea dawa mwilini.
4. ..................ni mashine ya kuonea viungo vya ndani ya mwili.

## 11.3. Sarufi: Matumizi ya kauli za vitenzi

**Kazi ya 6:**

**Soma sentensi zifuatazo na kutofautisha viambishi vilivyokolea**

Baada ya mpango kukamil**ika**, walifik**isha** hoja zao kwa Mkuu wa shule ambaye aliridh**ika** na nia hiyo ya wanafunzi wake.

Baadaye, walitum**iwa** barua na Daktari Mkuu wa hospitali ya kuwakubalia ziara yao.

**Maelezo muhimu**

Kauli za vitenzi zilizotumiwa katika sentensi hapo juu ni zifuatazo:

i. Kauli ya kutendeka
ii. Kauli ya kutendesha
iii. Kauli ya kutendewa

**Yafuatayo ni maelezo kwa kila aina ya kauli:**

1. Kauli ya Kutendeka - kitendo kukamilika au kuwa katika hali timilifu.
2. Kauli ya Kutendewa - kitendo kufanywa kwa niaba yako au kwa ajili yako.
3. Kauli ya Kutendesha - kumfanya mtu atende jambo fulani.

**Kazi ya 7:**

**Onyesha mnyambuliko wa vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendeka na kutendewa**

Vitenzi ni kunywa, kuzaa, kupenda, kutaja na kujenga.

**Kazi ya 8:**

**Tunga sentensi 3 ambazo vitenzi vyake vinabeba kauli ya kutendeka, kutendesha na kutendewa**

**Kazi ya 9:**

**Soma kisa kifuatacho na kuweka vitenzi husika katika hali ya kutendewa**


Baba alimpatia mtoto wake elimu kuhusu uhifadhi wa mazingira, uzalishajimali pamoja na usawa wa kijinsia. Alimwelezea pia faida za kupiga marufuku uvivu, ulevi pamoja na ukatili. Alimtungia hadithi za kumwongoza na kumwelekeza katika njia nzuri za kimaisha. Baadaye, alimpelekea wajibu wa kuzitetea haki za binadamu na kuishi kwa amani na watu wote mahali popote atakapokuwepo.

## 11.4. Matumizi ya lugha: Vifaa vya hospitalini

**Kazi ya 10:**

**Taja majina ya vifaa vifuatavyo na kueleza umuhimu wa kila kifaa.**












**Kazi ya 11:**

**Tafuta vifaa vingine vinavyotumiwa hospitalini na kueleza umuhimu wake.**

**Maelezo muhimu**

Hospitali hutumia vifaa mbalimbali wakati wa kuhudumia wagonjwa. Baadhi ya vifaa hivyo ni hivi vifuatavyo:

1. Eksrei/uyoka: mashine ya kuonea viungo vya ndani ya mwili.
2. Machela: kigari au kitanda cha kubebea wagonjwa.
3. Mikroskopu/hadubini: kifaa kitumiwacho kuangalia vitu vidogo.
4. Dipfriza: chombo cha kuhifadhia baadhi ya dawa zinazohitaji kuhifadhiwa katika kiwango cha baridi sana.
5. Jiko: chombo cha kuchemshia vyombo ili kuulia viini na bakteria.
6. Glovu: kitu kama soksi kitengenezwacho kwa mpira na huwekwa mkononi kukingia uchafu.
7. Sindano: kifaa cha kupenyezea dawa mwilini.
8. Sirinji: kifaa chenye umbo la bomba ambapo madaktari na wauguzi huchopeka sindano ili kumdunga mgonjwa au kufyonza sampuli ya damu.
9. Makasi: kifaa ambacho hutumiwa kwa kukatia
10. Bendeji: kitambaa cha kufungia jeraha au kidonda
11. Plasta: kitambaa kigumu sana cha kufungia sehemu iliyovunjika
12. Koleo: kifaa cha kushikia vitu vinavyotumiwa na daktari.

## 11.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Kazi ya 12:**

**Kwa ushirikiano na wenzako, igiza mazungumzo yanayohusu vifaa vya hospitalini.**

**Kazi ya 13:**

**Itembelee zahanati au hospitali moja, kisha uzungumzie vifaa ulivyowahi kuviona.**

### Kazi ya 14:

**Simulia hisia ulizokuwa nazo au ulizosikia kutoka mtu mwingine kuhusu siku yako au yake ya kwanza kudungwa sindano hospitalini.**

## 11.6. Kuandika

### Kazi ya 15:

**Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kuongozwa na muktadha wa vifaa vya hospitalini**

a. Nilipokuwa bado mtoto nilikuwa na woga wa kuenda hospitalini kwa sababu...................................

b. Inasemekana leo kuwa Hospitali ya Roi Faisal ni maarufu sana kwa sababu..................................

c. Hospitali au zahanati nyingi hushindwa kutoa huduma bora kwa sababu ya................................

d. Sindano hospitalini hutumiwa mara moja kwa mgonjwa kwa ajili ya ............................................

## SOMO LA 12: WAFANYAKAZI WA HOSPITALINI



### Kazi ya 1:

**Tazama kwa makini mchoro hapo juu kisha uzungumzie vitu muhimu unavyoviona**

## 12.1. Kusoma na ufahamu: Kazi nzuri ya udaktari



***Wanafunzi wameendelea na matembezi yao hospitalini. Sasa ni wakati wa kuongea na wafanyakazi.***

**Muuguzi:** Shukrani Daktari, ningependa tuelekee sehemu ambapo tutawapata wafanyakazi mbalimbali ili niwaelezee kazi zao. Daktari au tabibu mnayemwona hapa ndiye anayewatibu wagonjwa. Mimi ni Muuguzi au nesi. Kazi yangu ni kumsaidia daktari katika kazi yake.

**Mkunga:** Jina langu ni Liberata. Mimi ni Mkunga. Kazi yangu ni kutoa huduma kwa wajawazito wakati wa kujifungua.

**Mhazigi:** Ninaitwa Jean Paul. Mimi ni mhazigi. Wajibu wangu ni kuwashughulikia waliovunjika viungo kama vile miguu au mikono.

**Msaidizi:** Ninaitwa Francoise, Msaidizi katika maabara. Mimi hutoa huduma kwa wagonjwa.

**Karani:** Jina langu ni Shema, Karani wa hospitali. Jukumu langu ni kufanya rekodi za wagonjwa.

**Mfamasia:** Mimi ni mfamasia na jina langu Pascasie. Kazi yangu ni kuziweka dawa na kuzitoa kwa wagonjwa.

**Daktari wa meno**: Byiringiro Charles, daktari wa meno. Jukumu langu ni kuwashughulikia wagonjwa walio na matatizo ya meno.

**Aminata:** Kwa mujibu wa wanafunzi wenzangu, tumenufaika zaidi kutokana na safari hii. Kwa kweli, tungeliitembelea hospitali hii mwaka jana, tungelijua haya yote tayari. Wahenga walisema kwamba asiyefika kwa mfalme hudanganywa mengi. Tumebahatika kufika hapa na mengi tumeyaelewa.

**Mireille**: Sisi sote tumeridhika na maelezo tuliyopewa. Kwa upande wetu, tunaahidi kuwaunga mkono kama iwezekanavyo kwa kuchagua mchepuo wa udaktari ili kuwahudumia wagonjwa hospitalini.

**Daktari:** Asanteni sana vijana. Kwa heri ya kuonana, tunawatakia kila la kheri!

**Aminata:** Asante sana Daktari pamoja na Muuguzi, na sisi tunawatakia kazi njema!

**Kazi ya 2:**

**Soma kifungu cha habari hapo juu na kujibu maswali ya ufahamu yafuatayo:**

1. Ni watu gani wanaozungumziwa katika mazungumzo haya?
2. Matembezi haya yamekuwa na lengo lipi?
3. Jadili faida pamoja na hasara kutoka ziara ya wanafunzi iliyozungumziwa.
4. Wanafunzi wameridhika na ziara yao. Je, unakubaliana na ukweli huu? Eleza msimamo wako.

## 12.2. Matumizi ya msamiati kuhusu mazingira ya hospitali

**Kazi ya 3:**

**Kwa kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu au njia nyingine tofauti, toa maana ya msamiati ufuatao na kutungia sanifu sentensi sahihi.**

a. Kutibu
b. Jukumu
c. Mujibu
d. Wahenga
e. kuahidi

## Kazi ya 4:

**Oanisha maneno katika sehemu A na maana zake kutoka sehemu B.**

| **Sehemu A** | **Sehemu B** |
|---|---|
| 1. Dobi | a. anayewatibu wagonjwa. |
| 2. Tabibu | b. anayewasaidia wajawazito kujifungua. |
| 3. Mkunga | c. anayeshughulikia waliovunjika viungo. |
| 4. Karani | d. anayepokea pesa kutoka huduma mbalimbali. |
| 5. Mhazigi | e. anayeshughulikia vipimo vya afya. |
| 6. Mfamasia | f. anayeweka rekodi za wagonjwa. |
| 7. Maabara fundi | g. anayeweka dawa na kuzitoa kwa wagonjwa. |
| 8. Muuguzi au nesi | h. afuaye nguo na kuzipiga pasi. |
| 9.Afisa wa usalama | i. anayemsaidia mganga kuwatibu wagonjwa. |
| 10. Keshia | j. achunguzaye mwendo wa wanaoingia na kutoka. |

## Kazi ya 5:

**Husisha wafanyakazi wafuatao na vifaa wanavyotumia**

| | |
|---|---|
| 1. Dobi | a.plasta |
| 2. Daktari | b. kompyuta/tarakilishi |
| 3. Karani | c. beseni pamoja na sabuni |
| 4. mfamasia | d. stethoskopu |
| 5. mhazigi | e. Kikombe cha dawa |

# 12.3. Sarufi: Matumizi ya kauli za vitenzi

## Kazi ya 6:

**Soma sentensi zifuatazo na kutofautisha viambishi vilivyokolea**

Walipowasili hospitalini walikaribi**shwa** na kupokel**ewa** vizuri. Waliele**zewa** mambo mengi sana na kuonge**zewa** ujasiri wa kuchagua mchepuo wa udaktari. Waliahidi kwamba kazi yao itafany**wa** kwa bidii.

**Maelezo muhimu**

Viambishi vilivyopigiwa mstari vinaonyesha kauli ya kutendwa ambayo huathirika moja kwa moja na kitendo

### Kazi ya 7:

**Andika vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendewa kwa kuzingatia mabadiliko ya kimaana.**

1. Wezi wameniiba pesa zangu.
2. Tulimzaa mtoto wa kike miaka sita iliyopita.
3. Dawa imewaua nzi wengi kutoka chooni.
4. Kampuni ilimfikisha meneja wake mahakamani kwa sababu ya uporaji mali.
5. Tumekula chakula kitamu kwa wingi.
6. Tulivua samaki wengi kutoka ziwa Kivu.
7. Si vizuri kunywea pombe hospitalini.
8. Wilaya itatengeneza barabara za lami nyingi.
9. Dobi amefua nguo za aina mbalimbali.

## 12.4. Matumizi ya lugha: Aina za kazi

### Kazi ya 8:

**Katika jozi, jadilini kuhusu kazi za watu mbalimbali mnazozijua.**

**Maelezo muhimu**

Zipo kazi za aina nyingi duniani. Kazi hizi hutofautiana kulingana na ujuzi, elimu na tajiriba ya kiwango cha juu.

Ifuatayo ni baadhi ya mifano mbalimbali ya kazi:

**Mhasibu**: Mtaalamu wa kuweka hesabu ya fedha.

**Mhandisi/injinia**: Mjuzi wa kutengeneza, kuhudumia na kuunda mitambo.

**Tarishi/Katikiro:** Anayehudumu ofisini kwa kutumwa kupeleka habari au ujumbe.

**Bawabu:** Alindaye mlangoni.

**Topasi/chura:** Asafishaye choo.

**Tabibu/daktari/mganga:** Mwenye ujuzi wa kutibu.

**Muuguzi/mualisaji:** Ahudumiaye wagonjwa.

**Msarifu:** Anayesimamia na kuidhinisha matumizi mazuri ya fedha katika shirika.

**Dereva:** Aendeshaye vyombo vya nchi kavu k.v. gari.

**Nahodha:** Aendeshaye na kuongoza vyombo vya majini k.v. meli.

**Rubani/Mwanahewa:** Aendeshaye na kuongoza vyombo vya angani k.v.ndege.

**Utingo/taniboi:** Mpakiaji na mpakuaji wa mizigo katika gari.

**Hamali/mpagazi/mchukuzi:** Abebaye mizigo kwa malipo.

**Malenga:** Mtunzi stadi wa mashairi na nyimbo.

**Manju:** Stadi wa kutunga na kuimba nyimbo katika ngoma.

**Kuli:** Apakiaye na kupakua shehena za forodhani.

**Dobi:** Afuaye na kupiga nguo za watu pasi kwa malipo

**Sogora:** Fundi wa kupiga ngoma

**Saisi:** Atunzaye wanyama wanaopandwa k.v. punda na farasi.

**Msajili:** Awekaye orodha ya kazi, vitu au viumbe.

**Mkalimani/mtarijumani:** Afasiriaye lugha moja hadi nyingine.

**Sonara:** Atengenezaye mapambo kwa kutumia madini**.**

**Kinyozi:** Anyoaye nywele.

**Msusi/msosi:** Asukaye watu nywele.

**Ngariba:** Mtu anayefanya kazi ya kutahiri katika jando.

**Mkunga:** Awasaidiaye wajawazito kujifungua**.**

**Kungwi:** Afundishaye mwari wa kike au kiume.

**Mshenga:** Atumwaye kupeleka habari za ndoa (posa).

**Refa:** Mwamuzi katika mchezo k.v. soka

**Kasisi:** Kiongozi wa kidini katika madhehebu fulani ya kikristo

**Imamu:** Kiongozi wa kidini katika madhehebu fulani ya kiislamu**.**

**Hakimu:** Aamuaye kesi katika mahakama.

**Kadhi:** Hakimu wa kiislamu

**Mwekezaji:** Anayeweka mali au pesa katika mradi au biashara.

**Meneja:** Msimamizi au kiongozi katika kampuni au shirika.

**Karani:** Afanyaye kazi ya kuandika k.m. barua na majarida.

**Kocha:** Mwalimu wa mchezo k.v. soka, voliboli, n.k.

**Mkutubi:** Ahifadhiye vitabu maktabani na kuviazima kwa wasomaji.

**Mnajimu:** Mwenye elimu ya nyota. Hutabiri mambo.

**Mpigaramli:** Abashiriaye kwa kupiga bao**.**

**Mwajiri:** Aandikaye mtu kwa kazi ya malipo au mshahara.

**Mzegazega:** Achotaye maji na kuyauza**.**

**Dalali:** Auzaye bidhaa katika mnada (soko la kushindania bei)

**Manamba:** Mfanyakazi wa muda katika shamba kubwa.

**Mnyapara:** Msimamizi wa kazi.

**Mhazili:** Sekretari - Atunzaye barua na majarida na kuandika kwa mashine ofisini.

**Mhadhiri:** Mwalimu katika chuo kikuu.

**Mwashi:** Fundi wa kujenga nyumba.

**Mhunzi:** Afuaye vitu vya madini ya chuma au bati.

**Seremala :** Atengenezaye samani za mbao au miti.

**Mfinyanzi:** Atengenezaye vyombo vya udongo k.m. vyungu.

**Mvuvi:** Afanyaye kazi ya kuvua samaki.

**Mwanaanga:** Afanyaye utafiti wa hali ya anga**.**

**Mkabidhi:** Mtu atunzaye mali kwa ajili ya mwingine

**Diwani:** Anayewakilisha watu wake katika serikali za wilaya

**Mzoataka:** Anayeokota takataka

**Kaimu:** Anayeshikilia cheo au wadhifa fulani kwa muda**.**

## 12.5. Kusikiliza na Kuzungumza

### Kazi ya 9:

**Kwa kushirikiana na wenzako,buni na uigize mazungumzo kuhusu kazi za ufundi mbalimbali.**

### Kazi ya 10:

**Itembelee zahanati au hospitali moja, kisha zungumzia wafanyakazi uliowaona hapo.**

### Kazi ya 11:

**"Daktari ni muhimu sana kuliko mwalimu". Jadili na wenzako kauli hii.**

## 12.6. Kuandika

### Kazi ya 12:

**Kamilisha sentensi hizi kulingana na ujuzi wako**

a. Ili uwe na cheti cha udaktari, unapaswa kuwa na weledi katika mchepuo wa..............................

b. Baada ya kuhitimu masomo ya.............................. mtu huweza kupatiwa cheti cha urubani

c. Hakimu ni mfanyakazi ambaye alihitimu masomo ya..................

d. Kasisi huwa ameyazingatia masomo ya .......................

e. Keshia huteuliwa baada ya masomo ya...................................

f. Katibu ni lazima awe na stadi katika elimu ya........................

# SOMO LA 13: USAFI KATIKA MAZINGIRA YA HOSPITALINI



**Kazi ya 1:**

Tazama mchoro huu kwa makini na kuzungumzia unachoona.

## 13.1. Kusoma na ufahamu: Usafi ni ufunguo wa afya nzuri



*Daktari Mkuu pamoja na Muuguzi kutoka hospitali moja wilayani Gatsibo wamepata fursa ya kuwatolea wagonjwa maonyo kuhusu umuhimu wa usafi katika maeneo ya hospitali na mahali pengine.*

***Daktari***: Hamjambo wote!

***Wagonjwa***: Hatujambo Daktari!

***Daktari***: Haya! Kabla ya kuwatolea huduma mbalimbali, ningetaka tuongee kidogo kuhusu usafi hapa hospitalini.

Nani anayeweza kutuelezea kwa nini usafi hospitalini ni muhimu sana?

**Mgonjwa wa 1:** Usafi hospitalini ni lazima utiliwe maanani kwa sababu pasipokuwa na usafi afya ya wagonjwa pamoja na wafanyakazi wa hospitalini huwa katika hali mbaya sana.

**Daktari:** Vizuri sana! Nani mwingine ambaye anaweza kutaja mahali ambapo usafi unastahili kuliko pengine?

***Mgonjwa wa 2:*** Mahali muhimu pakushughulikia mno ni kama vile vyooni, vyumbani pamoja na nje ya hospitali.

***Muuguzi:*** Asante sana! Je, mnafikiri nini kwa mtu ambaye anakuja hospitalini bila usafi wa mwili pamoja na mavazi yake?

***Mgonjwa wa 3***: Kwa ukweli, watu kama hao wapo lakini tabia hiyo ni ya kuepuka sana.

***Daktari***: Ndiyo. Lakini ni lazima kujua kwamba usafi hospitalini huchunguzwa kupitia vifaa vyote vinavyotumiwa, dawa zinazotunzwa na kupewa wagonjwa, mahali pa kutolea huduma tofauti bila kusahau usafi wa mwili na nguo kwa wafanyakazi wa hospitalini.

***Muuguzi***: Sasa, nani ambaye anaweza kueleza hasara inayotokana na ukosefu wa usafi kwa ujumla?

***Mgonjwa wa 4***: Si hospitalini tu, ukosefu wa usafi mahali popote huweza kuambukiza magonjwa kadhaa kama vile ugonjwa wa kipindupindu, kuhara, minyoo, n.k.

***Daktari***: Asante sana! Basi, nani wa kueleza njia au jinsi magonjwa hayo yanavyosambazwa?

***Mgonjwa wa 5***: Kwa mfano, kama vyoo havisafishwi vizuri, nzi huweza kujitafutia makazi humo. Wadudu hawa wanapogusa

kinyesi cha mgonjwa na kutua kwenye chakula cha watu wazima vilelevile huwaambukiza ugonjwa wa kipindupindu au kuhara. Lakini na matumizi ya maji machafu huweza kuwa chanzo cha magonjwa haya.

***Muuguzi***: Je, hakuna ugonjwa mwingine unaosababishwa na ukosefu wa usafi kwenu nyumbani?

***Mgonjwa wa 6***: Taka zikitupwa mahali pasipofaa, madimbwi pamoja na vichaka karibu na nyumba huwakaribisha mbu ambao husababisha ugonjwa wa malaria.

***Daktari***: Asante sana kwa mchango wenu. Kumbukeni kwamba usafi ni ufunguo wa afya njema. Inatubidi kuushughulikia mahali popote kwa ajili ya kuboresha maisha yetu mema.

## Kazi ya 2:

**Maswali ya Ufahamu**

**Chagua jibu sahihi kuliko mengine**

1. Tunatakiwa kuwa na usafi mahali popote kwa sababu

   a. usafi ni mzuri

   b. usafi wa mwili hulinda magonjwa

   c. penye ukosefu wa usafi maisha ya binadamu pamoja na ya mazingira yake huathirika vibaya.

   d. Mbu huweza kujificha katika vichaka na kuambukiza ugonjwa wa malaria.

2. Ugonjwa wa kipindupindu au kuhara husababishwa na

   a. nzi

   b. uchafu kutoka kinyesi unaosambazwa na nzi pamoja na matumizi ya maji machafu

   c. chakula kichafu na ambacho hakikuiva vizuri

   d. ukosefu wa vyoo safi na vya kutosha.

3. Taka zote ni lazima
   a. zichomwe
   b. zitupwe shambani
   c. zitupwe jalalani baada ya kutofautisha zinazooza na zisizooza
   d. zihifadhiwe katika mashimo mbali na nyumba.
4. Inastahili kuvaa glovu na bwelasuti wakati wa
   a. kula
   b. kupiga deki
   c. kuingia hospitalini
   d. kufanya usafi kwa ajili ya kujikinga na uchafu.
5. Usafi hospitalini ni jukumu la
   a. wagonjwa
   b. wagonjwa, wafanyakazi wa hospitali pamoja na yeyote anayekwenda hapo
   c. wafanyakazi wa hospitali
   d. hakuna jibu sahihi.

## 13.2. Matumizi ya msamiati

**Kazi ya 3:**

**Eleza maana ya maneno yafuatayo:**

1. Madimbwi
2. Kupiga deki
3. Huduma
4. Kuambukiza
5. Kipindupindu
6. Kichaka
7. Minyoo
8. Bwelasuti

**Kazi ya 4:**

**Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia choo, kuhara, deki, kutiliwa maanani, taka.**

1. .....................ni kifaa chenye majimaji kinachotumiwa kuosha sakafu ili kuondoa uchafu.
2. Baada ya kujisaidia ni lazima umwage maji katika...................................................................................
3. Matumizi ya maji machafu yanaweza kuwa chanzo cha kuambukizwa ugonjwa wa....................................
4. Kila jamii inalazimishwa kuwa na jalala la kutupia...................................................
5. Usafi ni jambo la..........................mahali popote.

## 13.3. Sarufi: Matumizi ya kauli ya kutendeshana

**Kazi ya 5:**

**Soma sentensi zifuatazo na kueleza maana ya kitenzi baada ya kuongezewa viambishi vilivyopigiwa mstari.**

1. Martha na Peter wanaelimishana mambo ya kujitegemea.
2. Walikaribishana na kutoa hoja zao.
3. Si vuzuri kugombanishana watu.

**Maelezo muhimu**

Kauli ya Kutendeshana - mtu anakufanya utende jambo fulani, nawe unamfanya atende jambo hilo hilo.

**Kazi ya 6:**

**Weka vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendeshana**

a. Wamepikiana chakula kitamu.

b. Tumefanyana mambo mema ya kuieleza jamii yetu.

c. Wamelimiana shamba la maharage.

d. Mmechora michoro inayoeleza wazi usawa wa kijinsia.

## 13.4. Matumizi ya lugha: Msamiati kuhusu aina za magonjwa

**Kazi ya 7:**

**Zungumzia aina mbalimbali za magonjwa yanayoweza kuhatarisha maisha ya binadamu**

**Maelezo ya kuzingatia**

**a. Maana ya ugonjwa**

Ugonjwa ni hali au kitu kinachomfanya mtu, mnyama au mmea kuwa katika afya duni. Pia ugunjwa huitwa maradhi, uele, ukongo. Kuna maradhi chungu nzima yanayoweza kumwathiri mtu. Mengine yana tiba mengine hayana. Mengine yanaambukizwa.

Maradhi ya kuambukiza ni yale yanayoenea kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine.

**b. Aina za maradhi**

Kuna aina mbalimbali za ugonjwa au maradhi. Ifuatayo ni miongoni mwa mifano.

**Saratani/kansa:** ugonjwa usio na tiba kwa sasa. Ni ukuaji usio wa kawaida wa seli katika mwili.

**Malale:** ugonjwa wa usingizi unaoambukizwa na mbung'o.

**Homa ya matumbo:** taifodi

**Kwashakoo/ukosandisha:** uele wa watoto unaosababishwa na uhaba wa chakula hususan protini.

**Surua/shurua/firangi/ukambi:** ugonjwa wa watoto unaofanya ngozi kuwa na vipele. Hatua za kwanza huwa ni homa kali.

**Mafua/bombo:** maradhi ya kuambukiza yanayosababisha mgonjwa kuumwa na koo na kichwa. Mgonjwa hutokwa na kamasi na kuwa na homa**.**

**Kaputula:** uele wa kuhara. Tumbo la kuendesha.

**Baridi yabisi:** maumivu ya mifupa au viungo yanayosababishwa na baridi shadidi.

**Ukoma:** uele wa kuambukiza wa mabatomabato ambao unaharibu mishipa ya fahamu na kukata viungo vya mwili.

**Matumbwitumbwi / machibwichibwi:** ugonjwa wa kuvimba mashavu hadi chini ya taya hususan kwa watoto

**Kisunzi/kizunguzungu / masua / gumbizi:** uele wa kuhisi kichwa kikizunguka.

**Kipwepwe:** ugonjwa wa ngozi unaosababisha madoa mekundu unaodaiwa kuletwa na chawa.

**Ndui:** ugonjwa unaosababisha pele nyingi zenye majimaji na usaha.

**Kororo:** uele wa kuvimba kooni.

**Ngiri:** ugonjwa wa kukazana kwa mishipa iliyo sehemu za chini ya kitovu.

**Zongo:** ugonjwa wa kuvimba tumbo kwa watoto wadogo.

**Vimbizi:** hali ya kutoweza kupata pumzi kutokana na chakula kutosagika tumboni.

**Mbalanga / barasi:** uele unaobadilisha rangi ya ngozi na kuwa na mabaka au matone.

**Rovu:** ugonjwa wa kuvimba tezi kwenye shingo.

**Tetekuwanga / galagala / tetemaji:** ugonjwa wa pele na homa kali wa kuambukizwa

## 13.5. Kusikiliza na kuzungumza

**Kazi ya 8:**

**Igiza mazungumzo hapo juu kati ya Daktari na wagonjwa.**

**Kazi ya 9:**

**"Usafi ni ufunguo wa afya njema." Jadili kauli hii.**

## 13.6. Kuandika

**Kazi ya 10:**

**Tunga sentensi nne kwa kutumia vitenzi kama vile kuondoa, safisha, kunawa, kuambukiza.**

## SOMO LA 14: ADABU HOSPITALINI

**Kazi ya 1:**

**Eleza adabu inayotakiwa hospitalini na utoe sababu za adabu hiyo.**

### 14.1. Kusoma na ufahamu: Utaratibu hospitalini

***Yafuatayo ni mazungumzo mbele ya darasa ya wanafunzi walioitembelea hospitali ya Girubuzima***

**Mwalimu:** Hamjambo vijana!

**Wanafunzi:** Hatujambo mwalimu!

**Mwalimu:** Kuna kundi la wanafunzi waliopewa kazi ya nyumbani kwenda kuitembelea hospitali moja.

Nawaomba wafike mbele ya darasa na kutusimulia juu ya ziara yao.

**Kiongozi wa kundi**: Asante sana mwalimu kwa fursa hii. Kazi tuliyoshughulikia ilikuwa inahusu mwenendo hospitalini.

Tuliitembelea hospitali moja inayoitwa Girubuzima. Ningetaka niwashirikishe wenzangu katika masimulizi haya.

**Mwanafunzi wa kwanza:** Tulipoingia katika maeneo ya hospitali, tuliwakuta watu wamekaa kimya mbele ya ofisi tofauti kwa ajili ya kutaka kuhudumiwa.

**Mwanafunzi wa pili:** Kwenye ukuta wa hospitali palikuwa pameandikwa maonyo au maadili mbalimbali kuhusu utaratibu unaofaa hospitalini kama ifuatavyo:

**Mwanafunzi wa tatu:** Hapa ni eneo la Hospitali. Inakatazwa kutenda yafuatayo:

Kuvuta sigara.

**Mwanafunzi wa nne:** Kuchafua majengo ya hospitali na mazingira yake.

**Mwanafunzi wa tano**: Kujisaidia pasipofaa.

**Mwanafunzi wa sita:** Kutema mate hadharani.

**Mwanafunzi wa saba**: Kupiga kelele.

**Mwanafunzi wa nane**: Kuharibu vifaa vya hospitalini kama vile kuvunja vioo, viti, mlango, n.k.

**Mwanafunzi wa tisa**: Kutumia pombe pamoja na dawa za kulevya.

**Mwanafunzi wa kumi**: Kuonyesha tabia ya ukatili, ugomvi, chuki pamoja na ubaguzi.

**Kiongozi wa kundi:** Hii ndiyo miiko ya kupiga marufuku ndani ya hospitali tuliyoorodheshewa.

**Mwalimu:** Asante sana kwa kazi hii! Darasa, pigieni makofi kundi hili.

## Maswali ya Ufahamu

### Kazi ya 2:

**Jibu maswali yafuatayo**

1. Habari hii imetokea wapi?
2. Ni mbinu gani ya ufundishaji na ujifunzaji inayozungumziwa?
3. Kwa nini maonyo yale yalitolewa hospitalini?
4. Ni wahusika wangapi wanaojitokeza?
5. Unadhani maonyo yale yalitolewa na nani?

## 14.2. Matumizi ya msamiati

### Kazi ya 3:

**Oanisha msamiati kutoka sehemu A na maana yake katika sehemu B**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Onyo | A. Kitu anachozuiwa mtu kufanya kama vile kuiba, kudharau, kutukana, ubakaji, n.k. |
| 2. Kukataza | B. Hali ya upendeleo katika kuwahudumia watu. |

| | |
|---|---|
| 3. Mwiko | C. Kuwa na mzozo au fujo, ghasia, vita, chokochoko, shari, mgogoro. |
| 4. Kujisaidia | D. Maelezo au maagizo ya kukataza mtu asifanye jambo fulani ambalo huenda likamdhuru. |
| 5. Dawa ya kulevya | E. Bidhaa aina ya vidonge, bangi, kokaine, au vinywaji mbalimbali ambavyo haviruhusiwi kutumiwa kisheria kutokana na athari yake mbaya sana kwa maisha ya binadamu pamoja na usalama wa jamii. |
| 6. Ukatili | F. Hali ya kuwa na roho mbaya, kukosa upendo. |
| 7. Ugomvi | G. Kulifanya jambo ambalo limekatazwa na mamlaka fulani lisifanyike. |
| 8. Chuki | H. Kuzuia au kumwambia mtu asifanye jambo fulani. |
| 9. Ubaguzi | I. Kwenda mahali k.m.chooni kwa haja ndogo au kubwa. |
| 10. Kupiga marufuku | J. Hali ya kukosa kuwa na huruma, udhalimu, uovu. |

## 14.3. Sarufi: Matumizi ya kauli za vitenzi

**Kazi ya 4:**

**Soma sentensi zifuatazo na kueleza maana ya kitenzi baada ya kuongezewa viambishi**

1. Mama na shangazi wamepikiana chakula kitamu sana.
2. Kagina na Amina waliimbiana nyimbo za kuvutia.
3. Mimi na binamu yangu tulitembeleana mwishoni mwa mwaka uliopita.

**Maelezo muhimu**

Viambishi vilivyopigiwa mstari vinaonyesha kauli ya kutendeana yaani unafanya kitendo kwa niaba ya mtu, naye anafanya kitendo hicho kwa niaba yako.

## 14.4. Matumizi ya lugha: Muhtasari kuhusu kauli za vitenzi

**Kazi ya 5:**

**Unganisha kauli za vitenzi vifuatavyo: fanya, lima, piga, cheza, lipa, penda, omba, dunga katika jedwali moja na kutoa mifano husika kwa kila kauli.**

1. Kauli ya Kutenda: Kitendo katika hali yake ya kawaida (bila kunyambuliwa)
2. Kauli ya Kutendea: Kufanya kitendo kwa niaba(au kwa ajili) ya mtu mwingine
3. Kauli ya Kutendana: Unamfanya mtu kitendo, naye anakufanya vivyo hivyo
4. Kauli ya Kutendeana: Unafanya kitendo kwa niaba ya mtu, naye anafanya kitendo hicho kwa niaba yako.
5. Kauli ya Kutendwa: Kuathirika moja kwa moja na kitendo
6. Kauli ya Kutendewa : Kitendo kufanywa kwa niaba yako au kwa ajili yako.
7. Kauli ya Kutendeka: Kitendo kukamilika au kuwa katika hali timilifu
8. Kauli ya Kutendesha : Kumfanya mtu atende jambo fulani
9. Kauli ya Kutendeshana: Mtu anakufanya utende jambo fulani, nawe unamfanya atende jambo lilo hilo

**Mifano ya kauli mbalimbali Katika Jedwali**

| TENDA | TENDEA | TENDANA | TENDEANA | TENDWA | TENDEWA | TENDEKA | TENDESHA | TENDESHANA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Imba | imbia | imbana | imbwa | imbwa | imbiwa | imbika | imbisha | Imbishana |
| abudu | abudia | abudiana | abudiana | abudiwa | abudiwa | abudika | abudisha | abudishana |
| Pika | pikia | pikana | pikiana | pikwa | pikiwa | pikika | pikisha | pikishana |
| Tembea | tembelea | tembeleana | tembeleana | tembelewa | tembelewa | tembeleka | tembeza | tembezana |
| Lia | lilia | ? | liliana | ? | liliwa | lika | liza | Lizana |
| penda | pendea | pendana | pendeana | pendwa | pendewa | pendeka | pendeza | pendezana |
| Kula | lia | lana | liana | liwa | liwa | lika | lisha | lishana |
| Dunga | dungia | dungana | dungiana | dungwa | dungiwa | dungika | dungisha | dungishana |

## 14.5. Kusikiliza na kuzungumza

**Kazi ya 6:**

**Simulia mbele ya darasa muhtasari wa mazungumzo hapo juu baina ya mwalimu na wanafunzi**

**Kazi ya 7:**

**Kwa ushirikiano na wenzako, igiza mazungumzo hayo.**

## 14.6. Kuandika

**Kazi ya 8:**

**Buni mazungumzo mafupimafupi baina ya mwanafunzi na mzazi wake kuhusu umuhimu wa usafi na uandike maneno yasiyopungua 100.**

**Tathmini ya mada**

1. Taja vifaa angalau vinne vya hospitalini na kueleza umuhimu wake
2. Baadhi ya sehemu muhimu za hospitali, chagua tatu na kueleza umuhimu wake.
3. Kamilisha sentensi zifuatazo:
   i. Kazi ya muuguzi ni..........................................................
   ii. Karani hospitalini hushughulikia..............................................
   iii. Tabibu ni mfanyakazi wa hospitalini anaye...............................
   iv. Mfanyakazi wa hospitalini anayeshughulikia waliovunjika viungo vya mwili huitwa................
   v. Anayetoa huduma kwa wajawazito wakati wa kujifungua huitwa............................................
4. Jadili hasara zinazoweza kujitokeza kwa sababu ya ukosefu wa usafi.
5. Zungumzia kasoro angalau tano ambazo zinachukuliwa kama mwiko hospitalini.

6. Weka vitenzi vinavyopatikana katika sentensi zifuatazo katika hali ya kutendwa.

   a. Tumesafisha vyumba, vyoo pamoja na jikoni kwa ajili ya kujilinda uchafu.

   b. Jana wageni walikula chakula kwa wingi.

   c. Si vizuri kupiga kelele hospitalini.

   d. Tunakunywa maji baada ya kuchemka.

   e. Sisi huvaa tai shingoni.

# MADA YA 4

# MSAMIATI KUHUSU MAENEO YA UTAWALA

**Uwezo mahususi :** Kuzungumza na kuandika kwa ufasaha matini fupifupi kwa kutumia msamiati unaofaa katika maeneo ya utawala.


**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kutoa msamiati utumiwao katika maeneo ya utawala, ngazi za utawala na viongozi wakuu wa kiserikali,
- kutaja aina za vitambulisho vinavvotumiwa na sikukuu za kitaifa,
- Kuainisha makazi ya watu mbalimbali,
- Kutumia kwa usahihi vivumishi vya majina ya ngeli ya U-ZI,
- Kuzungumza na kuandika kwa ufasaha Kiswahili kwa kutumia msamiati kuhusu utawala.

### Kidokezo

- Katika mazingira unamoishi kuna viongozi wa aina gani?
- Je, tarehe ya 1 Februari inakukumbusha nini kila mwaka?
- Taja aina tatu za vitambulisho unavyovijua.

## SOMO LA 15: WILAYA YETU



**Kazi ya 1:**

Jengo hili linakuonyesha nini?

## 15.1. Kusoma na ufahamu: Ofisi za kiutawala

**Soma mazungumzo yaliyo hapa chini baina ya Abayo, Baba, Gloriose na Anezerwe.**

(*Abayo alikubaliana na babake kwenda kuwashawishi rafiki zake ili waambatane kumpokea rais wa jamhuri katika ziara yake wilayani kwao)*

**Abayo:** Shikamoo baba!

**Baba:** Marahaba mwanangu. U safi leo kabisa!

**Abayo:** Ndiyo, leo tutampokea rais wetu wa jamhuri hapa kwetu.

**Baba:** Hilo ni jambo muhimu sana. Kila mtu ataenda kumpokea.

**Abayo:** Unajua atazuru miundombinu kadhaa wilayani humu kama vile: kuanzisha mradi wa umwagiliaji, kuzindua mradi wa ukarabati wa nyumba kwa familia zilizokumbwa na mvua kali na ukarabati wa barabara ya lami.

**Baba:** Nenda uwajulishe rafiki zako Gloriose na Anezerwe ili wasikose kuhudhuria.

**Abayo:** Kweli kabisa! Ebu niende.

**Baba:** Haya, safari njema.

**Abayo:** Hamjambo rafiki zangu.

**Gloriose:** Hatujambo sana! Karibu kwetu.

**Abayo:** Ningetaka kuwakumbusha ziara ya rais wa jamhuri katika wilaya yetu. Sherehe za kumpokea zinatarajiwa kufanyika kwenye uwanja wa michezo Ituze.

**Gloriose:** Uwanja huo unapatikana wapi?

**Abayo:** Unapatikana katika kijiji cha Kinini, kata ya Gitabi, tarafa ya Bwiza, wilaya Bikombe, mkoa wa Mashariki.

**Anezerwe:** Haaa! Nyinyi mmeisha kuwa wanasiasa! Hayo yote mimi siyajui.

**Abayo**: Ni kusema kwamba hujui hata wilaya yetu pamoja na mkoa?

**Gloriose:** Tafadhali, acha Abayo aendelee na habari yake ya ziara ya rais.

**Abayo:** Nimekuja kuwaalika ili msije mkakosa bahati ya kuwaangalia viongozi mbalimbali.

**Anezerwe**: Kweli? Viongozi wepi? Jamaa, tupatie mfano.

**Abayo:** Mawaziri mbalimbali akiwemo wa elimu, wabunge na maseneta, gavana wa mkoa wetu, wakuu wa wilaya mbalimbali, viongozi wa tarafa, wakuu wa jeshi na polisi kwenye ngazi mbalimbali, n.k.

**Gloriose:** Ehee! Viongozi wanapaswa kuweko ili wananchi wakiuliza swali lo lote watoe mchango wao katika kujibu au kumfafanulia rais.

**Anezerwe:** Hii ndiyo fursa yangu kuuliza swali kiongozi wa tarafa aliyetunyang'anya mabati yetu ya kutujengea nyumba baada ya dhoruba kali kuiangusha nyumba yetu.

**Gloriose:** Rais wetu ni mzuri atawauliza viongozi walichokifanya ili tusiteswe namna hii.

**Abayo:** Jamani! Naona saa za kuenda zimefika. Twende tufike mapema ili umati wa watu usitukataze kumwona rais.

**Anezerwe**: Eeeh!Twende. Asante sana Abayo kutujulisha.

Gloriose: Mienendo bora ya wananchi ni kujiendeleza, uzalendo na ushikamano, n.k.

**Abayo:** vizuri, twende.

**Kazi ya 2:**

**Maswali ya ufahamu**

**A. Baada ya kusoma mazungumzo hapo juu, jibu maswali yafuatayo:**

1. Ni wahusika gani wanaozungumza?
2. Kwa sababu gani Abayo aliamua kwenda nyumbani kwao Gloriose na Anezerwe?
3. Sherehe zinatarajiwa kufanyika wapi?
4. Raia wamealikwa kuwapokea viongozi gani?
5. Eleza miundombinu zilizotajwa katika kifungu cha habari.
6. Andika baadhi ya mienendo bora uliyoisoma katika mazungumzo.

**B. Jaza sentensi zifuatazo kwa kutegemea mazungumzo hapo juu**

i. ……….. ndiye alikwenda kuwaarifu………………ziara ya……………………..

ii. Ziara hii inatarajiwa kuhudhuriwa na viongozi kadhaa kama vile………………..

iii. Lengo kuu la ziara hii ni kuanzisha miradi ya kimaendeleo kama vile……………..

## 15.2. Matumizi ya msamiati

### Kazi ya 3:

**Fafanua msamiati ufuatao:**

Rais

Mbunge

Waziri

Umwagiliaji

Dhoruba

Miundombinu

### Kazi ya 4:

**Oanisha msamiati wa sehemu A na viongozi katika sehemu B**

| **Sehemu A** | **Sehemu B** |
|---|---|
| 1. Kijiji | a. Gavana |
| 2. Jeshi | b. Mbunge |
| 3. Jamhuri | c. Katibu mtendaji wa kata |
| 4. Kata | d. Meya |
| 5. Mkoa/jimbo | e. Mkuu wa kijiji |
| 6. Bunge | f. Katibu mtendaji wa Tarafa |
| 7. Wilaya | g. Waziri |
| 8. Tarafa | h. Kanali |
| 9. Wizara | i. Rais |

## Kazi ya 5

a. Jaza  akili ramani ifuatayo.





b. Taja majina yote ya wilaya za Rwanda.

## 15.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya U-ZI

## Kazi ya 6:

**Tazama sentensi zifuatazo zilizo katika sehemu A na sehemu B na kueleza mabadiliko ya kisarufi yanayojitokeza.**

| A | B |
|---|---|
| Ufagio wangu umevunjika  | Fagio zangu zimevunjika  |
| Ufunguo huu ni mrefu  | Funguo hizi ni ndefu  |
| Wembe ule si mzuri  | Nyembe zile si nzuri  |
| Uwineza atanunua uzi wa bluu  | Uwineza atanunua nyuzi za bluu  |

**Maelezo ya kuzingatia**

Ngeli hii inajumuisha nomino za vitu visivyo na uhai ambazo zinajigawa katika makundi matano yafuatayo:

1. Nomino ambazo umoja huanza kwa u- na wingi Ø-.

Kwa mfano: unywele, ukuta, ufagio, ufunguo, unyasi, utepe, utosi, ukoo, upote, upenu, upondo, upongoo, upanga, upepeo, n.k.

2. Nomino ambazo umoja huanza kwa u- na wingi wake huanza kwa ny-

Kwa mfano: uta, ufa, uwanja, uso, uwayo, uzi, uwalio, ugwe.

3. Nomino ambazo umoja huanza kwa w- na wingi huanza kwa ny-

Kwa mfano: waraka, wakati, wembe, wimbo, wayo, waya, wavu, wanja, wanda, wadhifa, waadhi.

4. Nomino ambazo umoja huanza kwa u- na wingi huanza kwa nd-

Kwa mfano: ulimi, uele.

5. Nomino ambazo umoja huanza kwa u- na wingi huanza kwa mb-

Kwa mfano: ubao, ubavu, ubati, ubale.

**Mifano zaidi katika sentensi:**

**Umoja:**

1. Ukuta huu umebomolewa na Umutoni.
2. Ufunguo wake utafungua vizuri.
3. Ukurasa wenyewe si mrefu.
4. Ukucha ule umechorwa na Nikuze.
5. Uso wa Solange ni mzuri

**Wingi:**

1. Kuta hizi zimebomolewa na Umutoni
2. Funguo zao zitafungua vizuri
3. Kurasa zenyewe si ndefu
4. Kucha zile zimechorwa na Nikuze
5. Nyuso za solange ni nzuri

## Kazi ya 7:

**Jaza jedwali hili kwa kuweka sentensi zilizomo katika umoja au wingi**

| | SENTENSI KATIKA UMOJA | SENTENSI KATIKA WINGI |
|---|---|---|
| 1 | | Kurasa hizi zimeandikwa na Yusufu. |
| 2 | Utepe unatumiwa kupima urefu wa vitu au watu. | |
| 3 | | Nyaya hizi zinatumiwa katika kazi za umeme. |
| 4 | Wembe wangu utakata nguo zote. | |
| 5 | | Nyaadhi hizi ni za mnyama gani? |

### Vivumishi katika ngeli ya U-ZI

1. **Vivumishi vya kuonyesha**

**Mfano:**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Wimbo huu unapendeza. | Nyimbo hizi zinapendeza. |
| Uzi huu umetoka wapi? | Nyuzi hizi zimetoka wapi? |
| Ukurasa huo umeandikwa vizuri. | Kurasa hizo zimeandikwa vizuri. |
| Utepe ule umenunuliwa leo. | Tepe zile zimenunuliwa leo. |

**Maelezo:**

Maneno ule,zile,hizo na huo ni vivumishi vya kuonyesha katika ngeli ya U-ZI, kwa sababu vinaonyesha jina au nomino fulani. Katika umoja: huu,huo na ule hutumiwa na hizi,hizo,zile hutumiwa katika wingi.

## Kazi ya 8:

**Jaza sentensi hizi kwa kutumia jibu sahihi kutoka mabanoni.**

1. Ufito ……………utakatwa upya.(huyu,huu,hii).
2. Fizi ……….zilijeruhiwa kutokana na ajali ya baiskeli (hio,huo,hizo).
3. Ufunguo…………unaweza kufungua nyumba yangu (ule,ile,zile).
4. Mwanafunzi ataandika ukurasa………… vizuri(hio,huo,hizo).
5. Nyufa ……………. zitazibwa na mwashi hodari (huu,hizi,hii).

2. **vivumishi vya pekee**

**Kazi ya 9:**

**Soma kifungu cha habari kifuatacho na kueleza matumizi ya maneno yaliyopigiwa mstari**

Bwana Kamali ni Mwalimu kwenye shule ya Mahoro. Siku moja akiwa njiani kuelekea shuleni alipoteza funguo zake pamoja na ufunguo wenyewe wa gari lake.

Kwa bahati nzuri funguo zile zote zilipatikana na kumwezesha kufika shuleni. Alipofikapo aliwapa wanafunzi wake kazi ya kuandika kurasa kumi za insha. Binti mmoja aitwaye Tamari aliandika ukurasa mmoja tu. Kwenye ukurasa wenyewe alichora picha za wanyama wenye kucha ndefu. Kucha zenyewe zilikuwa chafu mno. Mwalimu alimwonyesha mfano mzuri wa kufuata. Kwa hiyo, binti alikubali mfano wa mwalimu. Uso wa mwalimu ulionekana kuwa na furaha vilevile na uso huo wa binti Tamari ukaonyesha furaha tele.

**Maelezo**

Maneno wenyewe na zenyewe ni vivumishi vya pekee vyenye dhana kurejesha katika ngeli ya U-ZI, kwa sababu vina uaminifu wa kulirejea lile jina linalowakilishwa.Katika umoja wenyewe hutumiwa na zenyewe ikatumiwa katika wingi.

| **Mfano:** | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| | Uzi wenyewe | Nyuzi zenyewe |
| | Ukurasa wenyewe | Kurasa zenyewe |

Mifano katika sentensi

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Uso **wenyewe** umeharibika. | Nyuso **zenyewe** zimeharibika. |
| Ufagio **wenyewe** umepotea. | Fagio **zenyewe** zimepotea. |

## 15.4. Matumizi ya lugha: Ngazi za utawala

**Kazi ya 10:**

**Jadili maswali yafuatayo:**

a. Maeneo ya utawala nchini Rwanda yanaonekana katika muundo gani?

b. Panga viongozi wa utawala nchini Rwanda kulingana na ngazi zao

**Maelezo muhimu**

**1. Muundo wa ngazi za utawala nchini Rwanda**

Kijiji

kata

Tarafa

Wilaya

Mkoa

Taifa/nchi

**2. Ngazi za viongozi**

Mkuu wa kijiji

Katibu mtendaji wa kata

Katibu mtendaji wa tarafa

Meya/mkuu wa wilaya

Gavana

Viongozi wakuu wa taifa (Rais, waziri mkuu, mawaziri,wabunge, maseneta)

Nchi ya Rwanda ina jumla ya Mikoa 5, Wilaya 30, Tarafa 416 na Kata 2 148 na Vijiji 14 837.

Mji wa Kigali huongozwa na Meya wa mji. Viongozi wengine wanaopatikana katika ngazi za utawala ni wale wanaosimamia ngazi za usalama kama vile jeshi na polisi pamoja na viongozi wa vyeo mbalimbali vya kiserikali. Maseneta, Wabunge, Makatibu katika wizara tofauti, wakuu wa jeshi, wakuu wa polisi,…….Wote hushirikiana ili kuliendeleza taifa na kumsaidia rais wa jamhuri kuyafikia majukumu yake.Hii inamaanisha kwamba viongozi wote wakitimiza majukumu yao, nchi itaweza kuendelea haraka na kuukuza uchumi wake.

### Kazi ya 11:

**Oanisha sehemu A na sehemu B**

| A (ngazi za utawala) | B (viongozi) |
|---|---|
| 1. Kijiji | a. Katibu mtendaji wa kata |
| 2. Kata | b. Mkuu wa wilaya/Meya |
| 3 .Tarafa | c. Mkuu wa mkoa au jimbo/ Gavana |
| 4.Wilaya | d. Katibu mtendaji wa tarafa |
| 5.Mkoa/jimbo | e. Mkuu wa kijiji |

### Kazi ya 12:

**Kamilisha sentensi zifuatazo:**

1. Karongi ni mojawapo ya …………………...zinazounda ……………. wa Magharibi.
2. ……………………….wa jamhuri ya Rwanda alihutubia raia wote.
3. Nishati, umeme, ukarabati wa barabara ni baadhi ya …………………
4. Gavana ni kiongozi mkuu wa ………………………………………….
5. a.Idadi fulani ya kata inaunda ………………………………………..

   b. Jamhuri ya Rwanda inaongozwa na ……………………………

   c. Rwanda imegawanyika katika mikoa ifuatayo:…………………

## 15.5. Kusikiliza na Kuzungumza

### Kazi ya 13:

**Igiza na wenzako mazungumzo kuhusu kifungu cha habari kilichosomwa awali** “Ofisi za kiutawala.”

### Kazi ya 14:

**Iandae ziara kwenye kituo cha utawala kilichoko karibu yako na kusimulia mbele ya darasa kuhusu ziara yako.**

**Kazi ya 15:**

**Jitambulishe kwa mwenzako kwa kuzingatia maeneo ya utawala unamoishi pamoja na viongozi wake.**

## 15.6. Kuandika

**Kazi ya 16:**


**Tunga mazungumzo kati ya raia mmoja na kiongozi wilayani juu ya huduma ya kuomba kitambulisho fulani.**

**Kazi ya 17:**

**Tunga kifungu cha habari kifupi kwa kutumia msamiati ufuatao:**

a. Mkoa
b. Jamhuri
c. Kata
d. Wilaya

# SOMO LA 16: MAKAZI YA WATU



**Kazi ya 1:**

**Chunguza mchoro huu, kisha ueleze ikiwa unayoyaona yanahusiana na makazi ya watu**

## 16.1. Kusoma na ufahamu: Makazi ya watu

**Makazi** ni eneo au mazingira ambayo ni makao ya mnyama au mmea fulani au aina nyingine ya viumbe hai. Ni mazingira ya asili ambapo kiumbe huishi, au mazingira ambayo yanazunguka idadi ya jamii. Kuhusu makazi ya bianadamu, haya ni mazingira ambayo binadamu huishi na kuingiliana. Kwa mfano, nyumba ni makazi ya binadamu, ambapo binadamu hulala na kula. Haya yanaweza kuwa mjini au vijijini. Makazi ya mjini ni aina ya makazi ambayo watu wanajenga nyumba zao mijini, karibu na wenzao wengi. Mji wenye wakaaji wengi ni mji mkuu wa Kigali na miji kama Musanze, Huye, Rubavu, Rusizi, Muhanga na Nyagatare inayosaidia jiji la Kigali. Miji hii yote ina miundombinu mbalimbali kama vile umeme, maji safi, viwanda kadhaa, hospitali, barabara za lami, n.k.

Makazi ya vijijini ni aina ya makazi ambayo watu hujenga nyumba zao sehemu za vijijini. Asilimia kubwa ya Wanyarwanda huishi sehemu hii lakini serikali inaendelea kuwapa miundombinu tofauti kama inavyofanyia miji.

Nchini kwetu, serikali imewakataza raia kujenga na kuishi katika maeneo hatari kama vile vinamasini, mabondeni, milimani na sehemu nyingine zote zinazoweza kuhatarisha maisha yao. Serikali imetoa mchango mkubwa kulitatua tatizo hili kwa kuhamisha raia wote waliokuwa katika maeneo haya ya hatari ikiwapatia maeneo mazuri pia salama na kuwajengea nyumba bora vilevile. Hii inalenga wale wanaoishi katika mabonde chini ya milima mirefu kuepuka mmomonyoko wa ardhi na watu waliokuwa wamejenga kando ya mito na maziwa.

**Kazi ya 2:**

**Maswali ya ufahamu**

1. Taja aina za makazi bora kwa binadamu?
2. Eleza maeneo yasiyokubaliwa kuishi nchini Rwanda.
3. Serikali ya Rwanda ilifanya nini kuwaokoa waliokuwa wanaishi katika maeneo ya hatari?
4. Taja miundombinu ambayo serikali ilifikisha vijijini ili kusaidia raia kuishi vema.
5. Je, mmomonyoko wa ardhi husababishwa na nini?
6. Je, ungependa kuishi wapi kati ya mjini na kijijini? Kwa nini?

7. Jibu “**NDIYO** au **HAPANA**” kwa sentensi zifuatazo:

a. Binadamu hukaa katika nyumba.

b. Mji wa Kigali ni mji wenye wakaaji wengi duniani.

c. Sehemu za vijijini nchini Rwanda zina miundombinu mbalimbali.

d. Nchini Rwanda raia wanaweza kujenga nyumba zao sehemu yoyote.

## 16.2. Msamiati kuhusu makazi

### Kazi ya 3:

Fafanua maneno yafuatayo:

a. Nyumba

b. Bondeni

c. Mmomonyoko wa ardhi:

d. Kinamasi

e. Mjini

### Kazi ya 4:

**Oanisha maneno katika kundi A na maana yake katika kundi B**

| | A: Maneno |
|---|---|
| 1 | Umeme |
| 2 | Ziwa |
| 3 | Raia |
| 4 | Mabonde |
| 5 | Jiji |

| B: Maana |
|---|
| Mtu aliye na haki za kisheria za kuwa mkazi katika nchi fulani. |
| Sura ya nchi iliyoko baina ya milima. |
| Mji mkubwa wenye watu wengi na miundombinu kadhaa. |
| Eneo kubwa lenye maji lililozungukwa na nchi kavu. |
| Nguvu ya vitu kama betri au jenereta inayopitia katika waya na kutoa moto au mwangaza. |

## 16.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya U-ZI

### Vivumishi vya idadi

**Kazi ya 5:**

**Tazama sentensi hizi na kujadili mabadiliko ya kisarufi yaliyojitokeza:**

Ufagio **mmoja** umetumiwa kwetu.

Ukurasa mmoja umeandikwa vizuri.

Kuta **mbili** zitajengwa lini?

Fagio **tatu** zimeletwa na wavulana.

Nyufa **chache** zimezibwa na Ishimwe.

**Maelezo**

Maneno mmoja, mbili, tatu, nne, chache,…. ni vivumishi vya idadi katika ngeli ya U-ZI, kwa sababu vinaonyesha idadi au hesabu ya vitu. Aina hii ya vivumishi tunaweza kuigawa katika makundi mawili:

- Vivumishi vya idadi vinavyoonyesha idadi kwa jumla.
- Vivumishi vya idadi vinavyoonyesha idadi kwa hesabu.

Vivumishi vya idadi vinavyoonyesha idadi kwa jumla. Mifano ya vivumishi vya idadi vya kundi la kwanza ni kama:

i. chache
ii. ingi
iii. maridhawa
iv. pungufu
v. haba
vi. kidogo, n.k.

- Vivumishi vya idadi vinavyoonyesha idadi dhahiri: ni vya idadi isiyo kikomo kwani vinahusu hesabu ya nambari kuanzia moja na kuendelea.

**Mfano:**

i. moja
ii. mbili
iii. tatu
iv. nne

v. kumi
vi. mia
vii. elfu
viii. milioni, n.k.

**Kazi ya 6:**

**Weka sentensi hizi katika umoja au wingi:**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| | Kuta mbili zimejengwa leo |
| Ufa mmoja utatibiwa kesho | |
| | Kucha chache za solange ni ndefu |

**Kazi ya 7:**

**Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia kivumishi kinachofaa mabanoni.**

a. Upondo ……………….. umewekwa ndani ya mtumbwi (moja, mmoja, mbili).

b. Petero aliandika kurasa…………………..(zitano,tano,moja).

c. Umutoni na Abayo walipokea fagio………………. Siku ile (nyingi, moja, wengi).

d. Mtoto aliwaandikia wazazi wake nyaraka…………..katika muhula wa tatu. (nyingi, zingi, lingi).

e. Wembe ……………ulimkata kidole (moja, mmoja, wumoja).

## 16.4. Matumizi ya lugha: Makazi ya watu

**Kazi ya 8:**

**Jadili maswali yafuatayo:**

a. Makazi ni muhimu sana kwa binadamu.

b. Serikali ya Rwanda iliwakataza raia kujenga na kuishi katika maeneo hatarishi.

**Maelezo muhimu**

Kama ilivyoandikwa katika kifungu cha habari, makazi ni eneo au mazingira ambayo ni makao ya mnyama au mmea fulani au aina nyingine ya viumbe hai. Ni mazingira ya asili ambapo kiumbe huishi, au mazingira ambayo yanazunguka idadi ya jamii. Binadamu anaweza kuishi katika nyumba kubwa au ndogo kulingana na uwezo wake. Nyumba hizi lazima ziwe safi ili kujiepusha na magonjwa yatokanayo na uchafu. Ghorofa ni aina ya nyumba pia ambayo familia moja au nyingi huweza kuishi.

## 16.5. Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano kuhusu makazi

**Kazi ya 9:**

**Zungumzia wenzako umuhimu wa kuishi katika maeneo yasiyo hatari.**

**Kazi ya 10:**

**Simulia wenzako kuhusu picha au video ulizoziona zinazohusu makazi nchini Rwanda hasa hasa mji wa Kigali.**

## 16.6. Kuandika: Utungaji wa insha kuhusu makazi

**Kazi ya 11:**

**Tunga insha yenye aya 3 (Maneno yasiyopungua mia moja) ukielezea umuhimu wa kuishi katika maeneo yasiyo hatari.**



## 17.1. Kusoma na ufahamu: Sikukuu za kitaifa

Mwaka jana Yusufu alikuja kututembelea kwenye sikukuu ya Krismasi. Alipofika nyumbani kwetu tulimpokea vizuri kwa chakula pamoja na vinywaji mbalimbali. Tulipomaliza sherehe zetu, mwalimu wetu aliingia ndani na kutuuliza sababu tulikuwa tunafurahi sana. Bila kukawia nilimwambia kuwa nchini Rwanda kuna sikukuu za kitaifa nyingi zinazosherehekewa na kwamba siku hiyo tulikuwa tukisherehekea Krismasi. Mwalimu alituomba kumfafanulia sikukuu nyingine za kitaifa zinazosherehekewa nchini Rwanda. Tulianza kukodoleana macho tukingoja mmoja kati yetu ajibu swali hilo. Mwalimu alipoona kuwa kimya kimetutawala alianza kutufafanulia sikukuu hizo ili mara nyingine tusije tukatatizika. Yusufu alimwambia kwamba hakukumbuka na habari. Mwalimu alianza kumfafanulia sikukuu hizo ili mara nyingine asije akaziuliza tena. "Tarehe ya 1 Januari kila mwaka ni sikukuu ya mwaka mpya, tarehe 1 Februari sikukuuu ya mashujaa, tarehe 7 Aprili kila mwaka ni kumbukumbu ya mauaji ya kimbari dhidi ya watutsi, siku ya kuwakumbuka jamii ya Wanyarwanda iliyoangamia mwaka 1994," alisema mwalimu. Nami niliongeza kuwa tarehe 1 Mei ni sikukuu ya kazi ulimwenguni, sikukuuu ya uhuru wa Rwanda ikasherehekewa kwenye tarehe 1 Julai na tarehe 4 Julai kila mwaka ikawa sikukuuu ya ukombozi wa Rwanda.

Yusufu alituomba kutosahau sikukuu za kidini kama vile Idi kwa waumini wa kiislamu, sikukuu ya Bikira Maria kwa wakatoliki, sikukuu ya pasaka katika mwezi Machi au Aprili, n.k.

Kitu kingine alichotuambia mwalimu ni kwamba sikukuu hizi huwapa viongozi fursa ya kukutana na wananchi, kuwajulisha mipango ya serikali, pia hupata fursa ya kupumzika na kuwatembelea jamii na marafiki.

## Kazi ya 1:

**Maswali ya ufahamu**

1. Yusufu alikuja kututembelea kwenye sikukuu ipi?
2. Nani aliingia baada ya chakula na kinywaji? Alisema nini?
3. Ni kwenye tarehe gani ulimwengu mzima husherehekea sikukuu ya kazi?
4. Andika majina matatu ya sikukuu za kidini zinazosherehekewa nchini Rwanda.
5. Ni kitu gani kinachowanufaisha viongozi kwenye sikukuu hizi?

## 17.2. Msamiati kuhusu sikukuu za kitaifa

## Kazi ya 2:

**Eleza maneno yafuatayo ukiyahusisha na kifungu hicho.Tumia kamusi ya Kiswahili Sanifu pale panapohitajika.**

1. Krismasi
2. Mashujaa
3. Kukomboa
4.Kimbari
5. Fursa

## Kazi ya 3:

**Jaza sentensi kwa kutumia msamiati huu: Uhuru, mashujaa, kimbari, makazi, kuikomboa, Krismasi, Idi.**

1. Katika mwezi wa Februari sisi husherehekea sikukuu ya …………… lakini ile ya ………….. wa taifa ni mwezi wa Julai.
2. Mauaji ya …………nchini Rwanda yaliacha watu wengi bila………………
3. Majeshi ya RPF Inkotanyi yaliwahi…………………..nchi ya Rwanda.
4. ……………………huanza kulingana na kalenda ya waislamu.
5. Kwenye sikukuu ya ………..wao walikula chakula kizuri sana.

## 17.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya U-ZI na vivumishi vya sifa

### Kazi ya 4:

**Tazama sentensi hizi na kueleza maneno yaliyopigiwa kistari:**

- Ufunguo mpya unafungua mlango vizuri.
- Funguo nzuri zinafungua milango vizuri.
- Ukurasa mbaya umeandikwa na Irakiza.
- Kurasa nyekundu zimeandikwa na Irakiza
- Mugabekazi ametuagizia ufagio mzito.
- Mugabekazi ametuagizia fagio nzito.

**Maelezo muhimu**

Vivumishi vya sifa ni vivumishi vinavyotaja tabia au namna vitu vilivyo au vinavyoonekana. Vivumishi vinavyoonyesha tabia hii ni kama hivi vifuatavyo:

i. -ema
ii. -pevu
iii. -nyamavu
iv. -pumbavu
v. -nyenyekevu
vi. -danganyifu
vii. -changamfu
viii. -ovu, n.k

Katika mfano hapo juu tunaona kuwa kuna vivumishi vya sifa vinavyoonyesha tabia hasa ya viumbe hai. Ifuatayo ni mifano ya vivumishi vya sifa vinavyoonyesha jinsi vitu vilivyo hai au vinavyoonekana:

i. -zuri
ii. -baya
iii. -gumu
iv. -zito
v. -nene
vi. -eusi
vii. -pya
viii. -kongwe, n.k

### Kazi ya 5:

**Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia kivumishi kinachofaa kutoka mabanoni.**

a. Ukucha wake ……………….. umekatwa na Ahirwe (mbaya, baya, mabaya).
b. Mbwa huyu ana nyayo……………… (msafi, safi, usafi).
c. Kalisa aliandika kurasa…………………..(refu, ndefu, urefu).
d. Ufunguo ………………. umepotea njiani (ndogo, mdogo, wadogo).

## Kazi ya 6:

**Andika sentensi mbili zenye vivumishi vya sifa vinavyoonyesha tabia na nyingine mbili za vivumishi vya sifa vinavyoonyesha jinsi vitu vilivyo au vinavyoonekana katika jedwali hili:**

| Vivumishi vya sifa vinavyoonyesha tabia | Vivumishi vya sifa vinavyoonyesha jinsi vitu vilivyo au vinavyoonekana |
|---|---|
| 1. | 1. |
| 2. | 2. |

## 17.4. Matumizi ya lugha: Sikukuu za kitaifa

## Kazi ya 7:

**Chagua maneno haya na kuyapanga katika kundi A au B**

Pasaka

Sikukuu ya mashujaa

Sikukuu ya ukombozi

Sikukuu ya kazi ulimwenguni

Krismasi

Sikukuu ya uhuru wa taifa

Sikukuu ya watakatifu wote

Idi

**Maelezo muhimu**

Sikukuu ni siku yenye shamrashamra ya kuadhimisha tukio fulani. *Hii ni* siku maalumu ya kukumbuka, kusheherekea au kufurahia jambo fulani. Kati ya sikukuu za umma kuna *sikukuu za kidini* na *sikukuu za kiserikali*.

| **Sikukuu za kiserikali** | **Sikukuu za kidini** |
|---|---|
| Sikukuu ya mashujaa | Krismasi |
| Sikukuu ya wafanyakazi | Pasaka |
| Sikukuu ya Uhuru wa taifa | Jumatatu ya majivu |
| Sikukuu ya Ukombozi wa taifa | Ijumaa takatifu |
| Sikukuu ya wanawake | Idi |
| Sikukuu ya mwalimu | Sikukuu ya Watakatifu wote |

## 17.5. Kusikiliza na kuzungumza: Sikukuu za kitaifa

**Kazi ya 8:**

**Jadili kuhusu sikukuu za kitaifa na kutoa matokeo yako hadharani.**

**Kazi ya 9:**

**Ukitumia sikukuu uliyoisherehekea siku moja au zaidi, zungumzia wenzako jinsi ilivyokuwa.**

## 17.6. Kuandika


**Kazi ya 10:**

**Tunga kifungu cha habari kuhusu sikukuu fulani uliyoisherehekea siku moja au zaidi kisha uonyeshe vile ulivyoona pale.**

# SOMO LA 18: AINA MBALIMBALI ZA VITAMBULISHO




Kitambulisho cha utaifa




Kitambulisho cha shule

## 18.1. Kusoma na ufahamu: Ombi la vitambulisho

*Uwera, Aline na Rwema walienda kwenye ofisi ya tarafa ili kutafta vitambulisho mbalimbali*

**Uwera:** Shikamoo Katibu Mtendaji!

**Katibu Mtendaji:** Marahaba bibi. Nikusaidie nini?

**Uwera:** Nimekuja hapa ili nipate cheti cha kuzaliwa.

**Katibu Mtendaji:** Karibu ofisini. Nipe kibali cha Katibu Mtendaji wa Kata.

**Uwera :** Hiki hapa Katibu.

**Katibu Mtendaji:** Naona wewe namaliza kukupa huduma yako. Mwambie mwingine aingie.

**Uwera:** Kwaheri. (Mwingine anayehitaji huduma aingie).

**Rwema:** Mimi nataka kadi ya uraia nimetimiza miaka kumi na sita.

**Katibu Mtendaji:** Ndiyo. Na wewe?

**Aline:** Nimekuja mniandikie kibali niende kwenye wilaya kutafuta pasipoti kwani nitaenda Marekani mwezi ujao.

**Katibu Mtendaji:** Barabara kabisa. Rwema, nenda ukamkute mtumishi wa mtandao Irembo atakusaidia haraka. Na wewe Aline mwambatane kwa sababu mna  shida sawa.

**Aline& Rwema**: Asante sana katibu. Nchi yetu imepiga hatua kiteknolojia.

**Katibu Mtendaji:** Asante kushukuru.

**Kazi ya 1:**

**Maswali ya ufahamu**

1. Mazungumzo haya yametokea wapi?
2. Kwa nini raia walitembelea ofisi ya katibu mtendaji wa tarafa?
3. Kiongozi yule aliwapokeaje raia?
4. Rwema aliambiwa kupata alichokitaka wapi?
5. Ni kwa nyanja gani Rwanda ina maendeleo?

## 18.2. Msamiati kuhusu aina ya vitambulisho

**Kazi ya 2:**

**Toa maana ya  msamiati huu na uutumie katika sentensi**

i. Cheti
ii. Ofisi
iii. Huduma
iv. Kibali
v. Kuambatana

**Kazi ya 3:**

**Jaza sentensi kwa kutumia msamiati ufuatao: pasipoti, huduma, ofisi, cheti**

i. Nilipoingia kazini ilinibidi nitafute………………cha kuzaliwa.
ii. Mujawase ataulizwa………………..kabla ya kuenda nchini Ujerumani.
iii. Katibu mtendaji wa tarafa anawapa raia …………….nzuri sana.
iv. ……………ya wilaya yetu inapatikana mbali na nyumba yangu.

## 18.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya U-ZI na vivumishi vya kumiliki

### Kazi ya 4:

**Tazama sentensi hizi na kujadili mabadiliko ya kisarufi yanayojitokeza.**

1. Wimbo wake unapendeza mno (umoja).
2. Nyimbo zoo zinapendeza mno (wingi).
3. Upinde wangu umevunjika (umoja).
4. Pinde zetu zimevunjika (wingi)

**Maelezo muhimu**

Majina ya ngeli ya U-ZI yametumiwa pamoja na vivumishi vya kumiliki. Vivumishi vya kumiliki ni maneno yanayoonyesha kitu ni cha nani, mtu fulani ni wa nani au kitu kina nini . Navyo ni sita: –angu, -etu -ako,-enu -ake,-ao

**Mifano zaidi**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Uso **wangu** ni mzuri sana. | Nyuso **zetu** ni nzuri sana |
| Ufunguo **wako** ni mchafu kabisa | Funguo **zenu** ni chafu kabisa |
| Ukuta **wake** utajengwa upya | Kuta **zao** zitajengwa upya |

### Kazi ya 5:

**Jaza sentensi hizi kwa kutumia vivumishi vya kumiliki vinavyofaa kulingana na kiambishi cha nafsi ambacho kimeandikwa katika mabano:**

1. Ukucha …………………umerefuka sana (yeye).
2. Uzi …………………..ni mweusi sana (Kagorora na mimi).
3. Kazeneza na Mwami waliibiwa funguo ………….zote (wao).
4. Usikose kupaka rangi ukuta ………..ule kwani umechafuka sana (wewe).

## Kazi ya 6:

**Soma kifungu hiki cha habari na kueleza matumizi ya maneno yaliyopigiwa kistari**

Habari gani Dusabe? Mbona umenunua kufuli lenye ufunguo mmoja? Bila shaka utalirudisha sokoni. "Funguo zipi baba?" Dusabe aliniuliza. "Funguo nyingine nimeziweka kabatini," Dusabe aliendelea kueleza. Baada ya maelezo yake nilifungua kabati na kuziona zote ndani. Nilikosa cha kusema na kumwambia maneno haya: Samahani binti yangu sitakusumbua tena nimeziona. Uwineza ndiye alikuwa amezichukua. Niliendelea kumwuliza, "umeleta wembe upi?" Tuliongea mengi na kumruhusu aende kula chakula cha mchana. Tokea siku hiyo, Dusabe na Uwineza ni wasichana wapole wenye ukweli.

**Maelezo muhimu:**

Vivumishi vya kuuliza hutumika kwa kuuliza swali. Badhi ya vivumishi viulizi huchukua viambishi vya ngeli wakati ambapo vingine havichukui viambishi hivyo vikitumiwa pamoja na nomino za ngeli ya U-ZI.

Kivumishi kinachochukua kiambishi ngeli ni:-pi? Wakati ambapo viulizi – ngapi? na gani? Havichukui viambishi vya ngeli.

**Mfano:**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Ukuta upi umejengwa ? | Kuta zipi zimejengwa ? |
| - | Kuta ngapi zimejengwa? |
| Ukuta gani umejengwa? | Kuta gani zimejengwa? |

## Kazi ya 7:

Uliza maswali matatu ukitumia vivumishi **–pi** au **gani** katika ngeliya U-ZI

## Kazi ya 8:

**Jaza sentensi hizi ukitumia kivumishi cha kuuliza kinachofaa.**

i. Uwineza alichukua funguo…………….?

ii. Mchana huo Dusabe aliambiwa habari…………..?

iii. Ni wembe…………….ambao binti yangu atauleta?

iv. Tumbili wanapenda kuparamia ukuta…………?

v. Karatasi …………..zilitengenezwa katika miti ya kwetu?

## 18.4. Matumizi ya lugha

**Kazi ya 9:**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Je, raia anaweza kupata vitambulisho vifuatavyo katika ngazi zipi za kiutawala?

   Pasipoti, cheti cha kuzaliwa, Cheti cha ndoa na leseni ya udereva.

2. Ikiwa kitambulisho fulani kimepotea au kimeibiwa, raia aliyekipoteza atafanya nini?
3. Je, kuna kosa lolote la utumiaji mbaya wa vitambulisho vya kitaifa? Eleza.

**Maelezo muhimu: Vitambulisho.**

Kitambulisho ni cheti au kadi, aghalabu yenye picha inayotumiwa kwa ajili ya kumtambulisha mtu na mahali pa kazi au mahali pengine ambapo kitu kama hicho kinahitajika. Baadhi ya vitambulisho hivyo ni kama:

1. Kitambulisho cha utaifa
2. Cheti cha kuzaliwa
3. Cheti cha elimu ya msingi,
4. Pasi ya kusafiria (Pasipoti)
5. Cheti cha elimu ya sekondari (kidato cha vi)
6. Leseni ya udereva
7. Kadi ya bima ya afya
8. Kadi ya mpigakura
9. Nambari ya mlipa kodi (Tin. No)
10. Cheti cha ndoa
11. Cheti cha kufariki

- Nchini Rwanda, idadi kubwa ya vitambulisho hupatikana kupitia mtandao rasmi wa kiteknolojia -IREMBO na kumwangalia kiongozi husika baadaye.

**UMUHIMU WA KITAMBULISHO**

**Vitambulisho vya Taifa ni msingi wa maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.**

1. Vitasaidia kuongeza wigo wa mapato ya Serikali
2. Vitasaidia kumtambua mhusika kwa urahisi anapohitaji huduma katika taasisi mbalimbali kama vile benki, taasisi za mikopo na huduma za afya.
3. Vitarahisisha kuwatambua wakwepaji wa kurejesha mikopo kutoka kwenye benki na asasi mbalimbali za fedha nchini.
4. Vitasaidia kuweka kumbukumbu za matukio ya uhalifu katika daftari la kumbukumbu la kielektroniki.
5. Vitawezesha kumtambua mtu anapofanya biashara au shughuli nyingine kwa kutumia majina tofauti.
6. Vitafanikisha kuhakikisha kuwa mtu anapata stahili zake za jamii. Kwa mfano, kupata malipo ya pensheni, haki za matibabu, haki za kujiunga na masomo ikiwa ni pamoja na stahili zozote ambazo raia wa Rwanda anastahili kupata kwa urahisi kwani kupitia kitambulisho mtu atatambulika kwa urahisi (fulani ni nani?, yuko wapi?, na anafanya nini? katika taifa hili.
7. Vitasaidia kuondoa watumishi hewa kwenye mfumo wa malipo ya mishahara ya Serikali.
8. Vitaimarisha utendajikazi Serikalini kwa kuwa na kumbukumbu sahihi za watumishi na malipo ya stahili zao, hasa pale wanapostaafu.
9. Vitarahisisha zoezi la kuhesabu watu (sensa).
10. Vitarahisisha zoezi la kusajili wapigakura

## 18.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Kazi ya 10:**

Zungumzia umuhimu wa kuwa na kitambulisho cha taifa na hasara za kutokuwa nacho.

## 18.6. Kuandika

**Kazi ya 11:**

Andika umuhimu wa vitambulisho vya kitaifa. Kwa kutumia maneno yasiyopungua 100

## Tathmini ya mada

Jibu maswali yafuatayo:

1. Jamhuri ya Rwanda inaongozwa na nani?
2. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia vivumishi vilivyotolewa mabanoni:

   a. Ukuta ………………..ulioanguka ulikuwa haukujengwa vizuri (moja,mmoja,mbili).

   b. Habimana hakuvunja ufunguo……………….(ndogo, mdogo, wadogo).

   c. Nyuzi…………………..ni nyeusi na nyekundu, pia (zao, wangu, yake).
3. Taja majina ya kiutawala yanayotumiwa kwa viongozi wa ngazi zifuatazo:

   a. Wilaya b. Kijiji c. Tarafa
4. Andika aina tano za vitambulisho vya kitaifa.
5. Ni nini kinachowanufaisha viongozi wakati wa kusherehekea sikukuu za kitaifa?
6. Taja mifano minne ya umuhimu wa vitambulisho kwa jamii ya Wanyarwanda.

# MADA YA 5

# KISWAHILI KATIKA SHUGHULI ZA KIBIASHARA

**Uwezo mahususi wa mada:** Kuzungumza na kuandika kwa ufasaha matini fupifupi kwa kutumia msamiati unaofaa katika shughuli za kibiashara.

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kufanya mazungumzo kati ya mfanyabiashara na mteja,
- Kutumia kwa ufasaha mizani au vipimo katika hesabu,
- Kuainisha pesa zitumiwazo katika shughuli za kibiashara,
- Kuainisha bidhaa mbalimbali zipatikazo sokoni,
- Kutumia kwa ufasaha ngeli ya I-ZI katika sentensi sahihi,

### Kidokezo

**Taja baadhi ya msamiati maalumu unaotumiwa katika mazingira ya biashara**

## SOMO LA 19: MAWASILIANO SOKONI



**Kazi ya 1:**

Tazama mchoro hapa juu na kueleza kinachofanyika hapo.

## 19.1. Kusoma na ufahamu: Safari ya Niwemwiza na Kayigi sokoni





Siku moja nilitembea sokoni na kaka yangu Kayigi ili kununua vifaa vya shule. Soko hilo linaloitwa Gatare lilikuwa katika kilomita kumi na tano kutoka kwetu. Mama alitupatia pesa za nauli na nyingine za kununua vifaa tofauti vya shule na bidhaa nyingine za kutumia nyumbani.

Tulitoka nyumbani saa tatu za asubuhi na kufika sokoni saa nne. Tulipokuwa garini, Kayigi aliniuliza kama ninakumbuka vifaa ambavyo mama alituambia kununua. Nilimkumbusha kwamba alituambia kununua vifaa vifuatavyo: shati, jaketi, jozi ya viatu, sidiria, madaftari kumi, kalamu nane, soksi mbili na sabuni vilevile.

Kayigi aliniuliza kama hakuna vitu vingine amabavyo nimesahau ili anikumbushe tusije tukasahau na vile vilivyokuwa vinahusu matumizi ya nyumbani. Kwa kusema hayo nilianza kuangalia kulia na kushoto, mbele na nyuma kwa ajili ya kuchunguza aina mbalimbali za bidhaa tofauti ili nisije nikasahau chochote nilichoambiwa na mama.

Nilikumbuka kuwa, mama alikuwa ameniambia kununua nyama, viazi vitamu, maharagwe na sukari.

Tulipofika sokoni, tulishangaa kuona watu wengi wa marika tofauti wakijaa sehemu zote. Kelele nyingi za watu sokoni zilikuwa zimehanikiza si huku si kule.

Kayigi alinishika mkono na kunielekeza pahali panapouzwa bidhaa tofauti. Sauti hizo zilikuwa za wauzaji wakisema: Mia bei! Mia bei! ….karibu mteja… bei rahisi…..chagua….chagua…..kaptula hii ni mia tatu, jaketi hii ni mia tano. Karibu mteja wangu. Karibu katika kibanda changu. Bidhaa ni nyingi utachagua zile utakazo. Tulianzia sehemu panapouzwa nguo.

Kayigi nami tulifika mbele ya kibanda cha nguo tukaanza kuuliza bei ya vile tulivyokuwa tunataka. Kwanza niliuliza bei ya jaketi niliyokuwa nimechagua. Muuzaji alinijibu kuwa jaketi ilikuwa elfu moja. Nilimwambia apunguze kidogo kwa kuwa bei ilikuwa ghali. Tulijadiliana bei mpaka akakubali mia tisa.

Baada ya kununua nguo, tuliendelea kutembea sokoni tukanunua vifaa vya shule. Kwenye kibanda cha vifaa vya shule, tulinunua madaftari na kalamu. Bei za kila bidhaa zilikuwa ni bei nafuu. Daftari moja tulilinunua kwa mia moja na hamsini na kalamu kwa mia tu.

Kabla ya kurudi nyumbani, tulikumbuka kuwa mama alitutuma kununua nyama kwenye bucha. Nilichunguza mfukoni mwangu pesa nilizokuwa nabaki nazo nikaona mnabaki dola mia tano za Marekani tu. Niliuliza dada yangu jambo la kufanya akanishauri kwenda kwenye duka la kubadilisha pesa za kigeni. Tulikwenda mbio na kufika kwenye nyumba ya ghorofa kubwa ambapo pamekuwa maduka mengi ya kubadilisha pesa.

Tuliingia duka moja ambamo tulikaribishwa na kijana mmoja aliyetubadilishia pesa zetu katika pesa za Rwanda tukarudi sokoni.

Kwenye bucha, bei ilikuwa ghali pia kwani kilo moja ya nyama ilikuwa mbili elfu mia tano. Kayigi alijaribu kupunguzisha bei. Muuza nyama alikataa kuipunguza akisema kuwa hawezi kupata faida akipunguza. Je, mnataka nipate hasara? Muuza nyama aliuliza. Nilimwomba kupunguza bei kidogo kufika mbili elfu mia tatu.

Aidha, tulinunua kifungu kimoja cha mboga za sukumawiki, vifungu viwili vya nyanya na kilo moja ya chumvi.

Ilipofika saa saba za mchana tulichukua basi tukarudi nyumbani. Tulipofika nyumbani mama alitushukuru kwa kuwa hatukukawia kurudi na kuwa tulitumia pesa vizuri. Kila mmoja alimwahidi kumpa tuzo ya peremende mbili.

**Kazi ya 2:**

**Maswali ya ufahamu**

a. Taja aina mbili za bidhaa ambazo mama aliwatuma wanawe sokoni.

b. Ni kwenye sehemu gani ya soko ambapo Kayigi na Niwemwiza walinunua madaftari na kalamu?

c. Nini kilichosababisha Kayigi na Niwemwiza kushangaa walipofika sokoni?

d. Kwa sababu gani mchinjaji alikataa kupunguza bei ya kilo moja ya nyama?

e. Ni kwa sababu gani mama aliwapongeza wanawe walipotoka sokoni?

## 19.2. Matumizi ya msamiati

**Kazi ya 3:**

**Toa maana ya msamiati ufuatao:**

a. Faida

b. Bei ghali

c. Kununua

d. Kuuza

e. Bucha

f. Hasara

## 19.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya I-ZI

**Kazi ya 4:**

**Tazama sentensi zifuatazo na kujadili mabadiliko ya kisarufi yanayojitokeza.**

a. Biashara imetajirisha watu wengi duniani na kuendeleza hali yao ya maisha (Umoja).

- Biashara zimetajirisha watu wengi duniani na kuendeleza hali yao ya maisha (Wingi).

b. Nguo ambayo imechafuka imemuambukiza magonjwa (Umoja).

- Nguo ambazo zimechafuka zimewaambukiza magonjwa (Wingi).

**Maelezo muhimu**

Ngeli hii ya I-ZI inajumuisha nomino za vitu visivyo na uhai. Nomino hizi umoja na wingi wake huwa ni sawa. Isitoshe, nomino hizi ni za vitu ambavyo vinaweza kuhesabika k.m kalamu, meza, sahani, rafu, linga, saa, rula, soksi, nyumba, karatasi, kamusi, wiki, siku, chaki, chupa, ndizi, kamba, bawaba, pete, n.k.

Majina ya ngeli hii hutumia kiambishi nafsi "I" katika umoja na kiambishi nafsi "ZI" katika wingi kufuatana na upatanisho wa kisarufi.

**Matumizi ya majina ya ngeli ya I-ZI na vivumishi vya sifa**

- Vivumishi **"-baya"** na"**-pya**" huchukua kiambishi **"m-"** badala ya **"n-".**

**Mfano:**

**Umoja:** Barabara mpya ilijengwa Kiramuruzi na kurahisisha mawasiliano baina ya raia huko.

**Wingi**: Barabara mpya zilijengwa Kiramuruzi na kurahisisha mawasiliano baina ya raia huko.

**Umoja**:Tabia mbaya inakemewa na wengi

**Wingi**: Tabia mbaya zinakemewa na wengi

Vivumishi vinavyoanza na **"r"** herufi hiyo hugeuka **"nd"** inapotanguliwa na kiambishi **"n"**.

**Mfano:**

**Umoja**: Ndoo ndefu imewekwa bafuni ili kuogea mikono.

**Wingi:** Ndoo ndefu zimewekwa bafuni ili kuogea mikono.

- Vivumishi vinavyoanza na **"ch, f, p, k, t"** havipachikwi viambishi katika umoja wala wingi.

**Mfano:**

**Umoja:** Meza chafu imetupwa nje.

**Wingi**: Meza chafu zimetupwa nje.

**Umoja**: Nyumba kubwa na ya kisasa inahitajika mjini.

**Wingi**: Nyumba kubwa na za kisasa zinahitajika mjini.

**Umoja**: Sketi fupi inakatazwa shuleni.

**Wingi**: Sketi fupi zinakatazwa shuleni.

**Umoja**: Meza kubwa imewatosha watu wengi harusini.

**Wingi:** Meza kubwa zimewatosha watu wengi harusini.

**Umoja**: Ndizi tamu imenunuliwa sana sokoni.

**Wingi**: Ndizi tamu zimenunuliwa sana sokoni.

**Umoja**: Nyumba pana iliwatosha wageni wote wakati wa mkutano wa kimataifa.

**Wingi**: Nyumba pana ziliwatosha wageni wote wakati wa mkutano wa kimataifa.

**Kazi ya 5:**

**Chagua neno linalofaa na kuliandika katika nafasi iliyoachwa wazi.**

1. Barabara hii ni ……….lakini imepasuka kwa sababu haikujengwa vizuri. (Zipya, kipya, mpya)
2. Tafadhari nipe Kamusi ya Kiswahili **………** kuna msamiati mgumu ninaotaka kuchunguza ( kisanifu, jisanifu, sanifu)
3. Karatasi …………zimetupwa jalalani ( mchafu, wachafu, chafu).
4. Meza …………imewekewa bidhaa nyingi sokoni (vipana, pana, kipana)
5. Pombe ………iliwalevya watoto na kusababisha kutohudhuria masomo (mtamu, litamu, tamu)

**Kazi ya 6:**

**Kwa kutumia vivumishi vya sifa, tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

a. Nyumba

b. Shule

c. Karatasi

d. Baiskeli

e. Nyumba

## 19.4. Matumizi ya lugha: Msamiati maalumu katika uwanja wa kibiashara

**Kazi ya 7:**

**Taja istilahi tano zitumiwazo katika shughuli za kibiashara na kueleza maana yake.**

**Maelezo muhimu kuhusu msamiati unaotumiwa katika shughuli za kibiashara.**

- Biashara: ununuzi na uuzaji wa bidhaa na/au huduma.

- Faida/tijara/kivuno/chumo/ziada - Pato libakialo baada ya kuondoa gharama za kufanya biashara k.v. ununuzi na usafirishaji.
- Hasara: Ukosefu wa faida; hali ya kupoteza pato au mali katika biashara.
- Bei: Kiwango cha pesa kununulia au kuuzia bidhaa au huduma fulani.
- Bei: Kiwango cha pesa kununulia au kuuzia bidhaa au huduma fulani.
- Uuzaji wa rejareja: Uuzaji wa kiasi kidogo kidogo.
- Uuzaji wa jumla: Uuzaji wa kwa pamoja
- Bei rafi: Bei ambayo haipunguzwi.
- Kipimo rafi: Kipimo ambacho hakipunguzwi.
- Bei ya kuruka: Bei isiyokubalika kisheria/haramu.
- Rasilimali: Jumla ya mali inayomilikiwa na mtu au nchi.
- Malighafi: Mali inayotumika kutengeneza vitu vingine k.m. pamba ni malighafi ya kutengenezea nguo.
- Maliasili: Utajiri kama vile madini, misitu, maziwa, mito, anga vinavyopatikana katika mazingira.
- Uwekezaji: Kutumia pesa / mali ili kuzalisha fedha/mali zaidi (ilikupata faida).
- Kitegauchumi: Rasilimali k.v. kiwanda inayotumika kuzalisha mali.
- Ujasiriamali: Uwekezaji mtaji katika biashara.
- Mtaji: Mali ya kuanzisha biashara au kuipanulia.
- Ulanguzi: Ufichaji wa bidhaa ili bei yake iruke.
- Magendo: Upigaji biashara kwa njia haramu/isiyo halali.
- Chenji: pesa inayobaki baada ya kununua kitu
- Maduhuli: Bidhaa ambazo hununuliwa kutoka nchi za nje.
- Mahuruji: Bidhaa zinazouzwa nchi za nje.
- Ushuru: Kodi ya kuingiza bidhaa nchini au kuziuza/Ada ya forodha.
- Ruzuku: Pesa inayotolewa na serikali kwa idara mbalimbali ili kujiendeleza.
- Mshitiri: Mnunuzi.
- Mteja: Mtu aendaye kununua bidhaa au huduma.
- Wakala: Ajenti.

- Utandawazi: Utaratibu wa mataifa kushirikiana katika nyanja mbalimbali k.v. biashara.
- Ubinafsishaji: Hali ya kusababisha mali ya umma imilikiwe na watu binafsi.
- Ubia: Ushirikiano wa watu wawili au zaidi katika shughuli k.v. ya biashara.
- Hawala: Hundi/ cheki yaani cheti maalumu cha benki kinachotumiwa kuidhinisha aliyetajwa kwenye cheti hicho apewe fedha za mwenye hesabu.
- Amana: Kitu unachomwekea mwenzako hadi atakapokihitaji.
- Turuhani: Kiwango kinachotolewa kutoka katika bei iliyotangazwa.
- Iktisadi: Uangalifu katika kutumia fedha/mali.
- Ubepari: Mfumo wa uchumi ambao unawawezesha watu wachache kumiliki rasilimali na vitegauchumi.
- Ukiritimba: Hali ya kuzuia wengine kufanya biashara au kushindana katika biashara.
- Dukakuu: Duka kubwa ambapo wateja hujichukulia bidhaa watakazo kutoka rafuni.
- Hisa: Sehemu ya mtaji katika biashara.

**Kazi ya 8:**

**Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo**

a. Hundi

b. Mteja

c. Ruzuku

d. Magendo

e. Rasilimali

## 19.5. Kusikiliza na kuzungumza

**Kazi ya 9:**

**Tega sikio habari inayosimuliwa na mwanafunzi mwenzako kuhusu safari yake sokoni na kusimulia hali ya safari hiyo mbele ya darasa.**

## 19. 6. Kuandika

**Kazi ya 10:**

**Tunga kifungu cha habari chenye aya tatu kuhusu safari yako sokoni.**


# SOMO LA 20: MAJADILIANO DUKANI

**Kazi ya 1:**

**Taja mahali fulani panapofanyiwa biashara na huduma zinazotolewa hapo.**

## 20.1. Kusoma na ufahamu: Muuzaji na mteja



*Mazungumzo yafuatayo yanahusu Kalisa ambaye ni mteja na Uwera ambaye ni muuzaji. Wanajadiliana bei dukani.*

**Kalisa :** Habari za asubuhi bibi !

**Uwera** *:* Nzuri. Nikusaidie nini ?

**Kalisa** : Nataka kununua bidhaa tofauti tofauti katika duka lako. Naona duka lako lina bidhaa mbali mbali zinazovutia macho.

**Uwera** : Ndiyo. Mimi ninaagiza bidhaa kufuatana na mahitaji ya wateja ili waweze kufaidika na kile wanachokinunua.

**Kalisa** *:* Mimi nahitaji sabuni, kilo moja ya chumvi, kilo mbili za sukari, nusu ya vitunguu, lita ya mafuta ya kupikia na sufuria moja.

**Uwera** : Vyote hapa Kalisa.

**Kalisa** :Kila bidhaa ambayo nimekutajia inauzwa kwa bei gani ?

**Uwera :** Bidhaa hizi zote zinauzwa kwa bei nafuu. Sabuni moja ni faranga mia moja, kilo moja ya chumvi ni faranga mia tatu, nusu ya vitunguu ni faranga mia moja hamsini, lita ya mafuta ya kupikia ni mia tano na sufuria hii ni moja elfu.

**Kalisa :** Mbona sufuria ni bei ghali ? Je, unaweza kupunguza kidogo ?

**Uwera** : Hiyo ni bei rafi bwana. Ungenunua sufuria mbili ningekupunguzia.

**Kalisa :** Nipunguzie faranga mia moja nitaendelea kununulia hapa.

**Uwera :** Ninakupunguzia faranga hamsini tu kwa sababu sufuria hii ni kubwa.

**Kalisa :** Asante. lakini chukua mizani unipimie kilo ya chumvi na nusu ya vitunguu.

**Uwera** : Ndiyo. Angalia hapa vipimo vinaenea. Kwa uhakika mizani yangu ni mpya sikunyang'anyi.

**Kalisa :** Hakuna nyongeza bibi ?

**Uwera** : Nitakupatia nyongeza ya kutosha siku ijayo.

**Kalisa** : Ni pesa ngapi ya kulipa kwa jumla?

**Uwera** : Mbili elfu kwa jumla.

**Kalisa** *:* Ahsante sana bibi.

**Uwera** : Asante kwa kushukuru. Karibu tena.

**Kalisa** :Kwaheri !

### Kazi ya 2:

**Maswali ya ufahamu**

1. Taja bidhaa zinazozungumziwa katika mazungumzo haya.
2. Kalisa alinunua nini dukani ?
3. Nini umuhimu wa mizani ?
4. Ni kwa sababu gani Uwera huuza bidhaa zinazovutia macho ya watu ?
5. Uwera alimwahidi Kalisa kumfanyia nini siku ijayo ?

## 20.2. Matumizi ya msamiati

### Kazi ya 3:

**Toa maelezo ya bidhaa zifuatazo:**

a. Kekee

b. Patasi

c. Chungu

d. Jiko la mkaa

e. Almasi

f. Dhahabu

g. Maziwa

h. Kuku

i. Maparachichi

j. Tikitimaji

## 20.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya I-ZI na vivumishi vya a-unganifu

## Kazi ya 4:

**Tazama sentensi katika sehemu A na sentensi katika sehemu B na kueleza mabadiliko ya kisarufi yanayojitokeza.**

| | |
|---|---|
| Ndege ya Rais wetu imetua Kanombe. | Ndege za Rais wetu zimetua Kanombe. |
| Nyumba ya Mahoro iliyojengwa mabondeni ilibomolewa na wezi. | Nyumba ya Mahoro liyojengwa mabondeni ilibomolewa na wezi. |
| Baiskeli ya baba ilichangia katika kuongeza mapato ya familia yetu. | Baiskeli za baba zilichangia katika kuongeza mapato ya familia yetu. |

**Maelezo muhimu kuhusu matumizi ya vivumishi vya a-unganifu**

Majina ya ngeli ya **I-ZI** yakitumiwa pamoja na vivumishi vya a-Unganifu, umoja wake huchukua **ya** na wingi huchukua **za.**

**Mfano:**

**Umoja:** Runinga ya Gakire ilinipasha habari kuhusu nanma ya kuleta umoja na maridhiano kwetu

**Wingi:** Runinga za Gakire zilinipasha habari kuhusu nanma ya kuleta umoja na maridhiano kwetu.

**Umoja**: Rafu ya mama inajaa bidha nyingi.

**Wingi**: Rafu za mama zinajaa bidha nyingi.

## Kazi ya 5:

**Tunga sentensi 5 kwa kutumia majina ya ngeli ya I-ZI na kiambishi cha -a unganifu**

## 20.4. Matumizi ya lugha: Aina za bidhaa zinazopatikana sokoni

## Kazi ya 6

**Bainisha aina kumi za bidhaa zinazopatikana sokoni.**

**Maelezo muhimu**

Kuna aina mbalimbali za bidhaa zinazouzwa na kununuliwa sokoni. Baadhi ya bidhaa hizo hutokana na kilimo, ufugaji, vifaa vya ufundi na vile ambavyo hutengenezewa viwandani.

**Kazi ya 7:**

**Toa mifano miwili miwili ya bidhaa zinazoweza kupatikana katika mazingira ya sokoni (Bidhaa zitokanazo na viwanda, mazao, ufugaji, madini)**

## 20.5. Kusikiliza na kuzungumza

**Kazi ya 8:**

**Buni mazungumzo kati yako na mwenzako kuhusu majadiliano kati ya muuzaji na mnunuzi. Majadiliano haya yafanyike sokoni na yaonyeshe kutokubaliana kwenye bei ya bidhaa zinazouzwa.**

## 20.6. Kuandika

**Kazi ya 9:**

**Tunga mazungumzo yasiyopungua ukurasa mmoja kuhusu majadiliano ya bei dukani.**

# SOMO LA 21: MATUMIZI BORA YA MIZANI



**Kazi ya 1:**

**Tazama mchoro hapo juu na kueleza kinachofanyika.**

## 21.1. Kusoma na ufahamu: Matumizi bora ya mizani



Bwana Muhire ni mfanyabiashara katika soko linaloitwa Maridadi. Biashara yake inahusu uuzaji wa matunda, bidha za kula, na mafuta ya kupikia. Mara nyingi raia humlalamikia wakisema kuwa yeye hatumii vipimo sahihi.

Siku moja, Amina alikwenda sokoni kununua bidhaa tofauti za matumizi ya nyumbani. Soko hilo lilikuwa kwenye umbali wa kilomita mbili kutoka kwake. Alipofika sokoni, alikaribishwa na muuzaji aitwae Muhire. Muhire anajulikana sana katika soko hili la Maridadi. Muhire alimwomba kutaja vitu vyote alivyokuwa anataka kununua.

Baadhi ya bidhaa alizokuwa anahitaji kulikuwa kilo kumi za maharage, kilo moja na nusu ya chumvi, lita tano za mafuta ya kupikia, gramu mia mbili hamsini ya nyama za kupikia ndugu yake mdogo, mafungu mawili ya sukumawiki na fungu moja la nyanya.

Baada ya kuorodhesha bidhaa hizo zote, aliomba Muhire kuchukua mizani na kupima ili kuhakikisha kwamba hamnyang'anyi. Muhire alichukua mizani na kuanza kupima maharagwe. Alipomaliza kupima, Amina aliona kuwa maharagwe yaliyokuwa yamepimwa yalikuwa machache akaanza kumlalamikia. Mbona unanipa maharagwe kidogo? “Mizani yako si sahihi,” Amina alisema. Amina alienda nyuma ya kibanda akapigia simu mfanyakazi katika Bodi ya Mapato Rwanda.

Katika dakika thelathini viongozi wanaohusika na ushuru nchini walitembelea soko hilo na kuwakagua wafanyabiashara halamu. Walitembelea watu ishirini na kukagua jumla ya mizani ishirini na miwili. Baadhi ya mizani hiyo, iliyokutwa sahihi ni ishirini na jumla ya mizani miwili ilikutwa na kasoro. Tokea hapo, mizani hii haikuruhusiwa katika biashara mpaka itengenezwe na mafundi na kuhakikiwa upya na wakala wa Vipimo ili iweze kuruhusiwa kutumiwa katika biashara.

Wafanyabiashara waliotuhumiwa ni Muhire na Kazimoto  ambao walikubali kosa lao la kutaka faida nyingi mno kwa njia isiyo halali. Bila kusita , viongozi waliwashawishi  raia na wafanyabiashara kutumia mizani iliyopimwa tu yaani iliyo sahihi.

Katika hatua nyingine, kiongozi mkuu aliwaonya wafanyabiashara wanaolalamikiwa kuweka mawe, kokoto pamoja na mchanga,vipande vya vyuma na aina nyingine za vitu kwenye mizani  kwa ajili ya kuongeza uzito waache tabia mbaya hiyo mara moja kwani wakikamatwa watapata hasara. Alieleza kwamba sheria ya vipimo ipo na inafanyakazi kwa pande zote mbili yaani kwa muuzaji na mnunuzi.

Wote hawatakiwi kufanya udanganyifu wowote katika biashara. Alisisitiza kuwa wale watakaobainika kuchezea mizani kwa ajili ya kuwaiba wananchi adhabu ni kubwa sana kwawo kama vile kifungo au kutozwa faini au vyote kwa pamoja ; shabaha ikiwa ni kumlinda mlaji ili apate faida na thamani ya kile alichozalisha ama kukinunua na siyo tu kupunjwa na wafanyabiashara wajanjawajanja.

Baada ya mkutano, mbele ya watu wote waliokuwa wamekusanyika hapo sokoni, viongozi walitoa tuzo ya mizani nne kwa wafanyabiashara ambao hawakuwa na makosa yoyote katika shughuli zao za kibiashara. Hii ilikuwa ni kutoa mfano kwa watu wote ili kusipatikane tena kosa lile la kuiba watu.

Watu waliokuwepo walifurahi na kuwapigia makofi viongozi wao.  Viongozi nao waliwapongeza kwa kuwa waliwajulisha hali ya makosa yanayofanywa na wafanyabiashara wakiwanyonya raia.

**Kazi ya 2:**

**Maswali ya ufahamu**

1. Nani ambaye alilalamikiwa kuwa na matumizi ya mizani isiyo sahihi?
2. Bainisha aina mbili za adhabu ambazo hupewa mtuhumiwa anayehusika na matumizi ya mizani isiyo sahihi.
3. Ni onyo gani lililotolewa na kiongozi mkuu kwa wafanyabiashara wanaotumia mizani kinyume na sheria?
4. Eleza lengo la ziara ya viongozi wanaohusika na ushuru katika soko la Maridadi.
5. Afanyaye vizuri hutuzwa. Eleza kauli hii kwa kutoa mfano kutoka katika kifungu hiki cha habari.

## 21.2. Matumizi ya msamiati

**Kazi ya 3:**

**Oanisha maneno katika sehemu A na maana yake katika sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1.Mizani | a.Mahali pa wazi penye watu wengi ambapo watu huuza na kununua bidhaa. |
| 2.Mfanyabiashara | b.Mtu anayepata kitu kinachouzwa kwa kulipa fedha. |
| 3.Miligramu | c.Kipimo cha umbali. |
| 4.Mnunuzi | d.Kifaa kitumikacho kupima uzito wa vitu. |
| 5.Soko | e. Mtu anayetoa bidhaa na kulipwa fedha |
| 6.Muuzaji | f. Vipimo vya tungamo. |
| 7.Kilomita | g.Mtu anayejishughulisha na ununuaji wa bidhaa na kuziuza kwa faida. |

## 21.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya I-ZI na vivumishi vya kurejesha

### Kazi ya 4

**Soma sentensi katika sehemu A na kujadili mabadiliko ya kisarufi yanayojitokeza katika sehemu B:**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| Nguo ambayo inamfaa mtoto ni ile ambayo inamkaa. | Nguo ambazo zinawafaa watoto ni zile ambazo zinawakaa. |
| Karatasi ambayo imechafuka imetupwa jalalani. | Karatasi ambazo zimechafuka zimetupwa jalalani. |

**Maelezo muhimu**

Majina ya ngeli ya **I-ZI**, katika sentensi hutumia kirejeshi **-yo** katika umoja na kirejeshi **-zo** katika wingi. Vivumishi hivi kuwa vinarejelea nomino.

**Mfano:**

**Umoja:** Pikipiki amba**yo** amenunua imemtajirisha.

**Wingi**: Pikipiki amba**zo** wamenunua zimewatajirisha.

### Kazi ya 5

**Kwa kutumia kirejeshi amba-, tunga sentensi katika umoja na wingi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

a. Klabu

b. Chupa

c. Redio

d. kaptula

e. suruali

## 21.4. Matumizi ya lugha: Matumizi ya mizani katika hesabu na aina za pesa

### Kazi ya 6

**Taja aina za mizani au vipimo unavyovijua**

**Maelezo muhimu**

**A. Matumizi ya mizani au vipimo**

Kipimo ni kiasi au kadiri. Kuna vipimo vya aina tofauti.

**Jedwali lifuatalo linaonyesha aina mbalimbali za vipimo.**

| AINA YA KIPIMO | MFANO |
|---|---|
| Vipimo vya umbali au urefu | • Kilomita (km)<br>• Mita (m)<br>• Sentimita (sm)<br>• Milimita (mm) |
| Vipimo vya ujazo | • Lita (l)<br>• Mililita (ml) |
| Vipimo vya tungamo | • Tani (tn)<br>• Kilogramu (kg)<br>• Miligramu (mg) |

**B. Hesabu**

Mifano ya hesabu kwa tarakimu na kwa maneno kutoka 1-1,000,000

| TARAKIMU | Kwa maneno |
|---|---|
| 1 | Moja |
| 2 | Mbili |
| 3 | Tatu |
| 4 | Nne |
| 5 | Tano |
| 6 | Sita |
| 7 | Saba |
| 8 | Nane |
| 9 | Tisa |

| | |
|---|---|
| 10 | Kumi |
| 11 | Kumi na moja |
| 12 | Kumi na mbili |
| 19 | Kumi na tisa |
| 20 | Ishirini |
| 21 | Ishirini na moja |
| 22 | Ishirini na mbili |
| 30 | Thelathini |
| 31 | Thelathini na moja |
| 40 | Arobaini |
| 50 | Hamsini |
| 60 | Sitini |
| 70 | Sabini |
| 80 | Themanini |
| 90 | Tisini |
| 100 | Mia moja |
| 101 | Mia moja na moja |
| 200 | Mia mbili |
| 500 | Mia tano |
| 900 | Mia tisa |
| 909 | Mia tisa na tisa |
| 1000 | Moja elfu |
| 100,000 | Laki moja |
| 10,001 | Laki moja na moja |
| 500,000 | Laki tano |
| 1,000,000 | Moja miliyoni |

## Kazi ya 7:

**Andika kwa tarakimu**

a. Kumi na sita
b. Thelathini na moja
c. Sabini na saba
d. Mia tatu hamsini
e. Moja elfu mia mbili na saba
f. Laki tano
g. Moja elfu mia mbili ishirini na sita

### C. Alama za hesabu

Alama ni mchoro wa kutambulisha kitu (Ishara)

**Jedwali lifuatalo linaonyesha alama za hesabu na maana zake.**

| ALAMA | MAAANA | MIFANO | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| × | Kuzidisha/ mara | 5×2=10 | Tano mara mbili ni sawa na kumi. |
| / | Kugawanya | 9 /3=3 | Tisa gawanya kwa tatu ni sawa na tatu. |
| + | Kujumlisha | 4+4=8 | Nne jumlisha nne ni sawa na nane. |
| - | Kutoa | 10-2=8 | Kumi toa mbili ni sawa na nane. |
| < | Ndogo kuliko | 11<50 | Kumi na moja ni ndogo kuliko hamsini. |
| > | Kubwa kuliko | 50>11 | Hamsini ni kubwa kuliko kumi na moja. |

## Kazi ya 8:

**Andika kwa tarakimu**

a. Sitini jumlisha kumi ni sawa na sabini.

b. Mia moja arobaini toa ishirini na saba ni sawa na mia moja na kumi na tatu.

c. Mia nane na themanini gawanya kwa nane ni sawa na mia moja na kumi.

d. Sabini na moja ni kubwa kuliko kumi na nne.

e. Mia moja ni ndogo kuliko laki moja.

f. Tisini mara tatu ni sawa na mia mbili na sabini.

### D. Aina za pesa zitumiwazo katika shughuli za kibiashara

## Kazi ya 9:

**Tazama mchoro ufuatao na kueleza shughuli zinazofanyiwa hapo.**



**Maelezo muhimu**

Pesa ni nini?

Pesa ni chombo cha kubadilishana bidhaa na huduma kati ya watu. Pesa zenyewe hazina faida na hazitoshelezi mahitaji ya binadamu ila zimekubalika katika jamii kama njia ya kujipatia mahitaji mengine. Kuna majina mengine ya pesa katika Kiswahili, kama kwa mfano: hela, fedha, dirhamu, darahima, fulusi au sarafu, n.k.

Pesa hutolewa na serikali ya nchi au na taasisi kama vile benki kuu inayofanya kazi hii kwa niaba ya serikali.

Kuna aina nyingi za pesa zinazotumiwa duniani katika biashara. Jedwali lifuatalo linatuonyesha baadi ya aina tofauti za pesa na nchi au bara zinakotumiwa.

| NCHI/ BARA | AINA YA PESA | KIFUPI / ALAMA |
|---|---|---|
| Marekani | Dola ya Marekani | USD($) |
| Kanada | Dola ya Kanada | CAD ($) |
| Ulaya | Euro | EUR (€) |
| Ujapani | yeni | JPY (¥) |
| Uingereza | Pauni | GBP (£) |
| Rwanda | Faranga | RFW |
| Burundi | Faranga | RFW |
| Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | Faranga | RFW |
| Tanzania | Shilingi | SH |
| Uganda | Shilingi | SH |
| Kenya | Shilingi | SH |

### Kazi ya 10:

**Kamilisha sentensi hizi kwa kutumia aina ya pesa zinazotumiwa katika nchi au bara husika.**

a. Wanyarwanda wengi hutumia ……………………katika shughuli nyingi za biashara ya ndani.

b. Mjomba wangu alikwenda kumtembelea rafiki yake anayeishi Uganda. Kabla ya kuvuka mpaka alikwenda kwenye duka la kubadilisha pesa ili wampe ………..za Uganda.

c. Mama aliniahidi kwamba nikishika nafasi ya kwanza katika kidato cha kwanza atanitembeza Marekani. Katika safari yetu tutatumia ………………… mia nne za kimarekani.

d. Shughuli za biashara anazozifanya mama yangu huhusisha uagizaji wa bidhaa kutoka Japani. Kila wiki hulipa ……..elfu tano.

e. Je, uliwahi kufika katika duka la kubadilisha pesa? Mimi nilifikapo nikaona faranga za Rwanda, Shilingi za Kenya, Dola za Marekani na Kanada na ………..za Uingereza.

### Kazi ya 11:

**Tafuta aina tofauti za pesa zinazotumiwa katika nchi nyingine ambazo hazikushughulikiwa katika somo hili.**

## 21.5. Kusikiliza na kuzungumza

### Kazi ya 12:

**Katika jozi, simulia mwenzako sifa za soko fulani uliyoitembelea na kueleza bidhaa ulizoziona.**

## 21.6. Kuandika

### Kazi ya 13:

**Tunga kifungu cha habari kifupi kuhusu umuhimu wa biashara**

### Tathmini ya mada

1. Taja angalau vifaa kumi vinavyouzwa sokoni.
2. Chagua neno linalofaa katika mabano na kukamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Mwalimu wetu huvaa suti nzuri sana. Wanafunzi wote hufikiri kwamba suti zake hununuliwa kwa bei ………. (ghali, rahisi, rafi).

b. Dada yangu amekwenda sokoni ……………………sare ya shule ili arudi shuleni kesho kuanza masomo ya muhula wa tatu( kununua, kuuza).

c. Uwantege anauza matunda katika soko la Nyagasambu. Kwenye kibanda chake kuna ,…………,……..,……… na …………( maembe, ndizi mbivu, machungwa, viazi vitamu, tikitimaji, mchele, madaftari, mananasi).

d. Mwenye duka la vitabu alitoa ……………………………. ya kitabu kimoja cha hadithi za Kiswahili kwa wateja wote ambao hununua kwake kila wiki (nyongeza, mtaji).

e. Wakati wa uhaba wa ………….. sokoni, bei hupanda sana (wateja, wanunuzi, bidhaa).

3. Kwa kuzingatia matumizi ya ngeli ya I-ZI, tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo:
   a. Nchi
   b. Tarafa
   c. Serikali
   d. Barabara
   e. Shule

4. Kamilisha kifungu cha habari hiki kwa kutumia maneno sahihi.

Mama Mutoni ni mfanyabiashara katika soko la Nyarugenge. Mara nyingi huagiza bidhaa kutoka nchi zinazopakana na Rwanda. Anapoagiza bidhaa kutoka Uganda inambidi abadilishe …………za Rwanda katika ……………..za Uganda. Ni sawa na kuagiza bidhaa kutoka Tanzania na Kenya.

Ikiwa Mama anahitaji bidhaa zinazotengenezewa katika nchi za Ulaya kama Vile Uingereza, inambidi kutumia ………………Mwezi uliopita rafiki yake ambaye anaishi Marekani alimwambia kuwa kuna bidhaa nzuri zinazoweza kumletea faida nyingi anapoziuza kwa Wanyarwanda. Mama aliamua kumtumia …………elfu tatu za Marekani ili amnunulie bidhaa hizo.

Kazi ya biashara naipenda sana. Kuna wakati amabapo naenda pamoja na mama yangu Zambia na Libya kufanya biashara huko nikaona namna anavyobadilisha faranga zake katika …………….. Libya au ……….za Zambia nikawa na motisha ya kufanya biashara ya kubadilisha pesa siku moja. Mimi nafikiri kwamba aina hii ya biashara itachangia kuongeza mapato yetu nyumbani.

5. Buni mazungumzo yenye ukurasa mmoja kati ya muuzaji na mnunuzi katika duka la vitabu.

# MADA YA 6 UIGIZAJI WA MAZUNGUMZO

**Uwezo mahususi katika mada hii:** Kuigiza mazungumzo mbalimbali kwa kutumia Kiswahili sanifu.

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kuzungumza Kiswahili Sanifu kwa ufasaha;
- Kujiamini katika mazungumzo ya hadharani au jukwaani;
- Kukuza stadi za kusikiliza, kukariri na kuzungumza hadharani;
- Kuendeleza weledi wa kubuni mazungumzo mbalimbali.

### Kidokezo

1. Nini maana ya mazungumzo?
2. Ni faida gani zinazopatikana kutoka mazungumzo?
3. Mazungumzo hujadili mada gani?
4. Katika mazungumzo, inawabidi wahusika kuwa na sifa gani?
5. Mazungumzo huweza kutokea wapi?

## SOMO LA 22: KUIGIZA MAZUNGUMZO



**Kazi ya 1:**

**Unaona nini kwenye mchoro huu?**

## 22.1. Kusoma na ufahamu: Mazungumzo kati ya mwalimu mkuu wa shule na mzazi



**Mwalimu mkuu wa shule:** Karibu bibi! Habari za asubuhi?

**Bibi:** Si nzuri hedimasta! Ahsante sana kwa kunikaribisha.

**Mwalimu mkuu wa shule:** Shida gani bibi? Nikusaidieje?

**Bibi:** Labda ni makosa ya mwanangu kutumwa mzazi.

**Mwalimu mkuu wa shule:** Jina lake ni nani?

**Bibi:** Gasagara Peter, mwanafunzi wa mwaka wa kwanza.

**Mwalimu mkuu wa shule:** Kwa nini umeitwa na shule?

**Bibi:** Kwa sababu ya utovu wa nidhamu wa mtoto wangu. Sababu hii niliisoma kwenye barua aliyopewa na shule ya kuniita mimi mzazi wake nije hapa shuleni haraka.

**Mwalimu mkuu wa shule:** Ndiyo! Mtoto huyo namkumbuka. Ni yapi yaliyomsibu? Je, alikuelezea kilichotokea?

**Bibi:** Alikuwa na makosa! Aliyakiri makosa matatu hivi: Kosa la kuchelewa shuleni, kuja shuleni bila vifaa vya shule na kukosa usafi mwilini.

**Mwalimu mkuu wa shule**: Ni kweli. Ilitubidi tumwite mzazi wake aje shuleni kwa sababu ya mwenendo wa mtoto wako ulikuwa unaendelea kuzorota sana. Bibi, unaweza kunielezea kwa nini mtoto wako hufanya kinyume na wenzake?

**Bibi:** Ushahidi ni kwamba sisi wazazi ndisi tuliokuwa chanzo cha matatizo haya yote. Kulingana na shughuli za kimaisha, tulidharau fursa ya kumchunga mwanetu na kuongea naye kila siku. Maana yake tulisahau jukumu letu kama wazazi. Kwa hiyo, naomba msamaha. Toka leo nimeahidi kurekebisha mienendo yetu na ya mtoto ili kuimarisha sura ya familia yetu.

**Mwalimu mkuu wa shule**: Ahsante sana kwa uamuzi mzuri huu. Kwa mujibu wa shule, tutashirikiana bega kwa bega kwa njia ya mawasiliano ya kila siku.

**Bibi:** Asante sana kwa makubaliano haya.

**Mwalimu mkuu wa shule**: Kumbuka kuwa ahadi ni deni.

**Bibi:** Ndiyo, usijali yote yatatimizwa.

### Kazi ya 2:

**Jibu maswali ya ufahamu yafuatayo:**

1. Kifungu cha habari cha hapo juu kinazungumzia nini?
2. Habari hii imetokea wapi?
3. Kwa nini mzazi ameitwa shuleni?
4. Ni makosa yapi yanayojitokeza katika kifungu cha habari?
5. Ni makubaliano gani yaliyofikiwa kati ya wahusika wawili?
6. “Harakati za maisha ya leo ni changamoto kubwa kwa elimu ya watoto katika jamii.” Husisha maoni haya na kifungu cha habari.

## 22.2. Matumizi ya msamiati

### Kazi ya 3:

**Kwa kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu au njia nyingine tofauti, toa maana ya msamiati ufuatao na kuutungia sentensi sahihi.**

a. Utovu wa nidhamu

b. Kuja

c. Kukiri

d. Kuzorota

e. Chanzo

f. Kuahidi

g. Kurekebisha

h. Kuimarisha

i. Uamuzi

j. Kushirikiana bega kwa bega

### Kazi ya 4:

**Jaza nafasi iliyoachwa wazi kwa kutumia msamiati unaofaa kutoka kifungu cha habari**

*i.* **.............** kosa ni njia ya kusamehewa.

ii. Ukosefu wa mwenendo mzuri ni ..........................cha kushindwa masomo shuleni.

iii. Ni lazima kuepuka vita kwa sababu bila usalama amani na utulivu .................................

iv. Tunaombwa .....................tabia mbaya ili tujenge jamii nzuri.

v. Tumechukua ................huu shuleni kwa ajili ya kugombana dhidi ya uvivu miongoni mwa wanafunzi

**Kazi ya 5:**

**Toa kinyume cha msamiati ufuatao**

a. Kumkaribisha mtu

b. Utovu wa nidhamu

c. Kushirikiana bega kwa bega

d. Kuzungumza

e. Kuheshimu

## 22.3. Sarufi: Matumizi ya “nini”, “nani” na “lini’ katika kuuliza maswali

**Kazi ya 6:**

**Soma sentensi zifuatazo na kuzungumzia matumizi ya maneno yaliyopigiwa mstari**

i. Jina lako ni <u>nani</u>?

ii. Kifungu cha habari kinazungumzia <u>nini</u>?

iii. Nchi yetu ilijinyakulia uhuru <u>lini</u>?

**Maelezo muhimu**

Maneno yaliyopigiwa mstari huitwa viulizi, yaani maneno yanayotumiwa kuulizia swali.

Viulizi huweza kutumiwa mwanzoni mwa sentensi au mwishoni mwake.

**Kwa mfano:**

- **Nani** amepiga hodi?
- Umesema bwana huyo anaitwa **nani**?

**Matumizi maalum ya viulizi**

**a. Nani**

Neno hili hutumiwa kuulizia mtu, Mwenyezi Mungu, mnyama, ndege au wadudu.

**Mfano:**

- **Nani** amezungumziwa hapa?
- Jina lake ni **nani**?
- **Nani** aliyeumba binadamu?
- Baadhi ya sungura na fisi, **nani** mjanja kuliko mwingine?

**b. Nini**

Hutumiwa kwa kuulizia kitu.

Mfano: Mmejifunza nini leo?

**c. Lini**

Neno hili hutumiwa kuuliza majira, kipindi cha muda (tarehe au mwaka)

Mfano: Ulizaliwa **lini**?

Wageni wako waliwasili nyumbani **lini**?

**Kazi ya 7:**

**Uliza swali linalofaa kwa kila sentensi kulingana na maneno yaliyopigiwa mstari**

a. Shule yetu ilijengwa miaka thelathini iliyopita.

b. Ukosefu wa usafi huweza kusababisha magonjwa.

c. Mgeni amewasili nyumbani.

## 22.4. Matumizi ya lugha: Mazungumzo na uigizaji wake

**Kazi ya 8:**

**Kwa kuzingatia mfano wa mazungumzo hapo juu, eleza maana ya neno 'mazungumzo' pamoja na aina zake.**

**Maelezo muhimu ya kuzingatia**

**Maana ya mazungumzo**

Mazungumzo au dayolojia ni utanzu mojawapo wa fasihi simulizi. Ni utaratibu wa kuongea baina ya watu wawili au miongoni mwa watu zaidi ya mmoja au pande mbili tofauti kuhusu mada mbalimbali zinazobadilikabadilika.

Baadhi ya vipera vya mazungumzo, vipera vitatu vifuatavyo ndivyo vinavyojulikana na kutumiwa sana.

**Malumbano ya utani:** Ni mashindano ya kuongea jukwaani baina ya watu wa makundi au jamii mbili ambayo hutumia kejeli na chuku kukejeli tabia mbaya katika jamii au kundi fulani. Watu husimama jukwaani na kushindana kwa maneno. Mazungumzo haya hutumia mzaha na vichekesho pamoja na kejeli ili kuangazia ukweli fulani katika jamii.

**Ulumbi:** Ni uwezo wa kipekee wa kuzungumza mbele ya hadhira. Mtu mwenye uwezo huo wa kipekee wa kuzungumza jukwaani huitwa mlumbi. Walumbi husifika sana kwa kuzungumzia mambo yanayoathiri jamii.

**Soga:** Ni mazungumzo baina ya watu wawili au zaidi ambayo aghalabu huwa hayana mada maalum. Aghalabu soga huwa na vichekesho vingi, mzaha na kejeli. Nia yake huwa kuburudisha na kupitisha wakati. Soga huwa na vichekesho na mzaha mwingi. Mada hubadilikabadilika kutoka wakati mmoja hadi mwingine. Haihitaji taaluma yoyote ya kisanaa na inaweza kufanyika pahali popote - njiani, sebuleni, katika vyumba vya burudani, n.k.

## 22.5. Kusikiliza na kuzungumza

**Kazi ya 9**

**Sikiliza mazungumzo kutoka video zifuatazo na kusimulia mbele ya darasa mambo yafuatayo:**

https=//www.youtube.com/watch?v=NK4MyrYIJI

https=//www.youtube.com/watch?v=G91GtbgdZKA

a. Dhamira kuu iliyozungumziwa

b. Maudhui

**Kazi ya 10**

**Kwa kushirikiana na wenzako, igiza mazungumzo kati ya mwalimu mkuu wa shule na mzazi wa mwanafunzi**

## 22.6. Kuandika

**Kazi ya11:**

**Buni mazungumzo (yenye ukurasa mmoja) kati ya mwalimu na mwanafunzi.**

**Kazi ya12:**

**Tunga sentensi sita kwa kuzingatia viulizi “nani” na “nini”.**

## SOMO LA 23: UMUHIMU WA UIGIZAJI WA MAZUNGUMZO



**Kazi ya1:**

**Unaona nini kwenye mchoro huu?**

### 23.1. Kusoma na ufahamu: Tujivunie lugha yetu

*Kamana na Zaninka ni wanafunzi wanaosomea darasa moja kwenye Shule ya Sekondari ya Tarubwenge. Wanazungumzia faida za kujizoeza uigizaji wa mazungumzo kama mojawapo ya njia za kupata weledi na umahiri wa lugha fulani.*

**Kamana:** Dada, unakumbuka jinsi tulivyokuwa miaka mitatu iliyopita?

**Zaninka:** Unataka kumaanisha nini? Unadhani nilihifadhi matukio yote katika miezi thelathini na sita yote?

**Kamana:** Nimetaka kuzungumzia mchakato wa kukuza ujuzi wetu katika stadi nne za lugha ya Kiswahili.

**Zaninka:** Aa! Kuna mambo tele ya kuongea kuhusu mafanikio tuliyonayo leo.

**Kamana:** Kiwango cha matumizi ya Kiswahili leo ni cha juu mithili ya Waswahili wenyewe.

**Zaninka:** Acha! Haya ni majivuno! Nakubali tumepiga hatua kubwa lakini hatujashindana na wale wakazi wa pwani.

**Kamana:** Mimi nina ushahidi mkubwa sana.

**Zaninka**: Ushahidi wako unautoa wapi?

**Kamana**: Weledi wangu katika kuizungumza kwa ufasaha lugha ya Kiswahili ulitokana na mazoezi darasani kwa kuigiza mazungumzo mbalimbali.

**Zaninka:** Si hayo tu. Kwa nini huzungumzii faida nyingine?

**Kamana**: Kwa mfano?

**Zaninka**: Kama kujiamini katika masimulizi hadharani.

**Kamana:** Huo ni ukweli mtupu. Wiki iliyopita niliingia katika mashindano ya mdahalo pamoja na wanafunzi kutoka shule tofauti za mjini ambao nilikuwa ninawaogopa kulingana na tajriba yao ya kuitumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha.

**Zaninka**: Matokeo ya mashindano yalikuwaje?

**Kamana**:Bila shaka nilijinyakulia ushindi na kutunukiwa kombe la almasi!

**Zaninka**: Mimi nimeishafanya maajabu kijijini kwetu! Wakati wa sherehe mbalimbali watu hunialika kwa ajili ya kuwaburudisha kupitia uigizaji wa mazungumzo. Mwishowe hunipatia zawadi ya pesa zaidi ya elfu kumi.

**Kamana**: Hatuwezi kuorodhesha faida zote, ndiyo sababu tunapaswa kujivunia lugha yetu tukufu.

## Kazi ya 2:

**Jibu maswali ya ufahamu yafuatayo:**

1. Kifungu cha habari kinazungumzia nini?
2. Ni wahusika gani wanaozungumziwa kifunguni?
3. Mafanikio ya wanafunzi hawa yalisababishwa na nini?
4. Je, majivuno ya wanafunzi hawa yana sababu ya kuwepo? Eleza.

## 23.2. Matumizi ya msamiati

**Kazi ya3:**

**Kwa kutumia kamusi ya Kiswahili sanifu au njia nyingine uzipendazo, toa maana ya msamiati ufuatao:**

a. Kujivunia

b. Mchakato

c. Tele

d. Mafanikio

e. Kujiamini

**Kazi ya4:**

**Jaza nafasi iliyoachwa wazi kwa kutumia msamiati huu:** *majivuno, pwani, ushahidi, tajriba, kujinyakulia*

i. Zaninka na Kamana wametoa.............................kwamba uigizaji wa mazungumzo ulikuwa chanzo cha mafanikio yao.

ii. Inahakikishwa kuwa asili ya Kiswali ni sehemu za.................. au mwambao wote wa Afrika Mashariki.

iii. .......................ni tabia ya kujisikia bora kuliko wengine; maringo.

iv. Baada ya kuishambulia timu B, timu A iliweza ........................ ushindi wa mabao mawili kwa nunge.

## 23.3. Sarufi: Matumizi ya "nini", "wapi" na "kwa nini' katika kuuliza maswali

**Kazi ya 5:**

**Soma sentensi zifuatazo na kuzungumzia matumizi ya maneno yaliyopigiwa mstari**

i. Je, miti itapandwa <u>wapi</u>?

ii. <u>Kwa nini</u> vijana hawajaelewa hasara ya kutumia dawa za kulevya?

**Maelezo muhimu**

**a. Wapi**

**Tu**natumia neno hili kuulizia mahali au sehemu fulani

**Mfano:** Unaishi wapi? ; Umesema uliniona juzi. Je, uliniona wapi?

**Tanbihi:** Matumizi ya neno '***pahali***', kiulizi '***wapi***' hugeuka '***papi***'

**Mfano:** Pahali **papi** panapotembelewa sana nchini humu?

**b. Kwa nini/ mbona**

Kiulizi hiki hutumiwa kuulizia sababu.

**Mfano: Kwa nini/ mbona** mmechelewa kufika shuleni?

**c. Namna gani**

Neno hili hutumiwa kuulizia namna au jinsi jambo lilivyotendeka

**Kwa mfano:**

Mlifanya kazi hii **namna gani**?

**Kazi ya 6:**

**Toa swali sahihi kutegemea maneno au kundi la maneno yaliyopigiwa mstari**

i. Sokwe mtu hupatikana katika mbuga ya wanyama iliyoko kaskazini mwa Rwanda.

ii. Taka zote hutupwa jalalani.

iii. Hali ya hewa ilikuwa nzuri mwaka huu kwani raia walipanda miti pahali pengi.

iv. Mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi yaliwezekana nchini Rwanda kwa sababu ya itikadi ya ubaguzi wa kikabila iliyofundishwa miaka mingi.

## 23.4. Matumizi ya lugha: Mazungumzo na uigizaji wake

**Kazi ya 7:**

**Jadili maswali yafuatayo:**

a. Nini maana ya uigizaji wa mazungumzo?

b. Uigizaji wa mazungumzo una umuhimu gani?

**Maelezo muhimu**

a. Kuigiza mazungumzo ni nini?

Ni kuyakariri mazungumzo yaliyosimuliwa na mtu mwingine na kuyarudia kwa kumwiga mtu huyo kimatendo kwa njia au namna ya mchezo; yaani kuvaa uhalisia wa mtu huyo. Ni karibu na maigizo au michezo ya kuigiza.

b. Umuhimu wa kuigiza mazungumzo

- Huunganisha watu katika jamii
- Hutumiwa kama chombo cha kuburudisha katika jamii.
- Vilevile huelimisha kuhusu mambo fulani
- Pia huleta umoja na utangamano
- Hutumiwa kuonya dhidi ya matendo mabaya.
- Hutumiwa kupitisha wakati.
- Hukuza stadi za kuzungumza lugha kwa ufasaha

## 23.5. Kusikiliza na kuzungumza

**Kazi ya 8:**

**Kwa ushirikiano na wenzako, igiza mazungumzo kati ya Zaninka na Kamana.**

## 23.6. Kuandika

**Kazi ya 9:**

**Buni kifungu cha habari kwa kutilia mkazo juu ya umuhimu wa uigizaji wa mazungumzo.**

**Kazi ya 10:**

Tunga sentensi nne kwa kutumia viulizi ‘’wapi’’ na ‘’kwa nini’’.

## SOMO LA 24: VIFAA KATIKA UIGIZAJI WA MAZUNGUMZO



**Kazi ya 1:**

Unaona nini kwenye mchoro huu?

### 24.1. Kusoma na ufahamu: Majukumu yetu katika uigizaji wa mazungumzo

**Egide na Liliane ni wanafunzi wanaosomea kidato kimoja kwenye Shule ya Sekondari ya Mazungumzo. Wanazungumzia vifaa vinavyowasaidia katika uigizaji wa mazungumzo pamoja na sifa za mwigizaji bora.**

**Egide:** Liliane, unayakumbuka mashindano tutakayoshuhudia wiki ijayo?

**Liliane:** Bila shaka nayakumbuka na nilazima tuanze maandalizi yake

**Egide:** Hayo ni kweli. Je, ni vifaa gani tutakavyohitaji ili tuliambulie kombe?

**Liliane:** Baadhi ya vifaa muhimu ni lazima kuwepo na simu ya mkononi, kofia, aina tofauti za pesa, chupa, tarumbeta, n.k.

**Egide:** Usisahau aina za mavazi mbalimbali kama suti, kimono, tarubushi pamoja na bombo.

**Liliane:** Aa! Hatukutaja vuvuzela, barakoa za ucheshi, mkongojo pamoja na miwani.

**Egide:** Asante sana kwa nyongeza. Sasa ni wakati wa kuzungumzia sifa zinazofaa kwa kila mwigizaji wa mazungumzo.

**Liliane:** Hizo ni mboga! Kwanza, mwigizaji bora ni lazima ajiamini katika mazungumzo yake.

Pili, anapaswa kutumia lugha ya ishara kama vile kusugua mikono, kutikisa kichwa, kugusa pua, kupiga vidole, kuinua nyushi, n.k.

Tatu, kuwa na ucheshi wa kutosha

Nne, kutumia vihisishi ili kufanya mazungumzo yawe ya kusisimua.

**Egide**: Si hayo tu, sifa zifuatazo sharti zizingatiwe pia:

Kutumia matamshi au lafudhi bora

Kuzungumza kwa ufasaha

Kuonyesha moyo wenye huruma

Kuwa na mazungumzo ya mkato na yasiyozidiana sana kati ya wahusika. Mhusika mmoja asitawale mazungumzo kupita wengine.

**Liliane:** Naam! Egide, tujipigie makofi kabisa! Ushindi ni wetu bila shaka.

**Egide**: Lakini kumbuka lililosemwa na wahenga kwamba chelewa chelewa utamkuta mtoto si wako.

**Liliane**: Usijali kaka yangu! Nimekupata wazi, ni lazima maandalizi yaanze leo bila kungoja kesho.

**Egide**: Naam, liwezekanalo leo lisingoje kesho.

**Maswali ya ufahamu**

**Kazi ya 2:**

**Jibu maswali ya ufahamu yafuatayo:**

1. Kifungu cha habari kinazungumzia nini?
2. Ni wahusika gani wanaozungumza?
3. Ni vifaa gani vilivyotajwa?
4. Onyesha angalau sifa tatu muhimu anazostahili mwigizaji bora.
5. Bila shaka wanafunzi hawa watajinyakulia ushindi. Tetea ukweli huu kulingana na ushahidi kutoka mazungumzo.

## 24.2. Matumizi ya msamiati

**Kazi ya 3:**

**Kwa kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu au njia nyingine tofauti, toa maana ya msamiati ufuatao na kuutungia sentensi sahihi.**

a. Kombe
b. Kujali
c. Maandalizi
d. Mkongojo
e. Ucheshi
f. Kimono
g. Tarubushi
h. Bombo
i. Barakoa

## Kazi ya 4:

**Oanisha michoro hii na majina yake, kisha eleza umuhimu wa kila aina: tarumbeta, vuvuzela, suti, miwani, barakoa.**

| Picha | Msamiati |
|---|---|
|  | |
|  | |
|  | |
|  | |
|  | |

## 24.3. Sarufi: Matumizi ya “gani” na “-ngapi’ katika kuuliza maswali

**Kazi ya 5:**

**Soma sentensi zifuatazo na kuzungumzia matumizi ya maneno yaliyopigiwa mstari**

i. Swali gani ambalo halikutolewa jibu?

ii. Miti mingapi mliyoipanda nyumbani kwenu?

**Maelezo muhimu**

**a. Gani**

Neno hili hutumiwa kuulizia aina ya mtu au vitu.

**Mfano:** Tatizo gani linalojitokeza hapa?

**Tanbihi:**

1. Kiulizi **gani** huweza kuwakilishwa na kiwakilishi -***pi***

**Mfano:**

- Tatizo **lipi** ambalo halijatatuliwa?
- Vitambulisho **vipi** vinavyotakiwa kwa kila mwanafunzi?
- Darasani **mpi** mnapatikana uchafu?

2. Viulizi mbalimbali huweza kuchukua nafasi ya viwakilishi viulizi.

**Mfano:**

- **Zipi** zimenunuliwa?
- **Papi** pamesafishwa?
- **Mpi** mmesafishwa?

**b. -ngapi**

Hiki ni kiulizi cha kuulizia idadi ya watu au vitu.

**Kwa mfano:**

- Ng’ombe **wangapi** walitolewa kwa raia kwa ajili ya kujitegemea?
- Ni wanafunzi **wangapi** wanaoomba mahitaji maalum ya ujifunzaji?

**Tanbihi:** Kiulizi hiki huweza kuchukua nafasi ya viwakilishi viulizi.

**Mfano: Vingapi** vinahitajika?

**Kazi ya 6:**

**Toa swali sahihi kulingana na maneno au kundi la maneno linalopigiwa mstari**

i. Tumetumia vifaa vya aina nyingi katika maigizo yetu

ii. Sabuni kadhaa zimewekwa nje ya choo kwa ajili ya usafi.

iii. Wanafunzi kumi wamezawadiwa kwa sababu ya kuimarisha amani na umoja darasani mwao.

iv. Mwigizaji bora anapaswa kuwa na sifa kama vile kujiamini, kuzungumza kwa ufasaha, kuzungumza kwa kutoa sauti, n.k.

## 24.4. Matumizi ya lugha

**Kazi ya 7:**

**Jadili mada zifuatazo:**

a. Umuhimu wa uigizaji wa mazungumzo

b. Wahusika wanaoshiriki katika uigizaji wa mazungumzo

c. Maigizo na aina zake

**Maelezo muhimu**

a. Kuigiza mazungumzo ni nini?

Ni kuyakariri mazungumzo yaliyosimuliwa na mtu mwingine na kuyarudia kwa kumwiga mtu huyo kimatendo kwa njia au namna ya mchezo; yaani, kuvaa uhalisia wa mtu huyo. Ni karibu sawa na maigizo au michezo ya kuigiza

b. Wahusika katika uigizaji wa mazungumzo

Kwa kawaida wahusika huwa ni binadamu. Wahusika ndio wanaozungumza katika sehemu zao mbalimbali. Kulingana na aina ya mazungumzo, wahusika wanaweza kuwa wawili au zaidi. Katika uigizaji wa mazungumzo, majukumu ya watu wa marika au viwango mbalimbali huigizwa kama vile wazee, rais, waziri, askari jeshi, mbunge, mwalimu, mfanyabiashara, mfalme, daktari, hakimu, n.k.

Maigizo ni sanaa katika fasihi simulizi ambayo watendaji huwa ndio wahusika. Maigizo hayasimuliwi kama mbinu nyingine za fasihi. Wahusika ndio huzungumza katika sehemu zao mbalimbali. Ifuatayo ni mifano ya maigizo.

1. **Michezo ya kuigiza** ( agh. huletwa jukwaani): Haya ni maigizo ya jukwaani ambapo watendaji huiga maneno na matendo ya wahusika mbele ya hadhira.
2. **Miviga**: Sherehe mbalimbali katika jamii fulani. Watu hujumuika na sherehe hizi kulingana na tamaduni zao
3. **Ngomezi:** Ni sanaa ya ngoma. Midundo mbalimbali ya ngoma hutumika kuwasilisha jumbe mbalimbali.
4. **Malumbano ya utani**: Mashindano ya kuongea jukwaani baina ya watu wa makundi au jamii mbili ambayo hutumia kejeli na chuku kukejeli tabia mbaya katika jamii au kundi fulani
5. **Ulumbi**: Uwezo wa kipekee wa kuzungumza mbele ya hadhira. Mtu mwenye uwezo huo wa kipekee wa kuzungumza jukwaani huitwa mlumbi.
6. **Soga** : Mazungumzo baina ya watu wawili au zaidi ambayo aghalabu huwa hayana mada maalum.
7. **Vichekesho**: Aina ya sanaa ya fasihi simulizi ambayo watu hutoa vihadithi vifupi au sentensi zenye uwezo wa kuwafanya wasikilizaji wacheke.
8. **Maonyesho ya sanaa**: Maonyesho huhusisha watu wa jamii au kundi fulani wanaoonesha taaluma, ujuzi au sanaa yao kwa watazamaji.

## 24.5. Kusikiliza na kuzungumza

**Kazi ya 8:**

**Kwa ushirikiano na wenzako, igiza mazungumzo kati ya Egide na Liliane.**

## 24.6. Kuandika

**Kazi ya 9:**

**Buni kifungu cha habari ambapo vifaa tofauti pamoja na sifa mbalimbali zimeonekana kwa wahusika wanaoigiza mazungumzo.**

**Kazi ya 10:**

**Tunga sentensi nne kwa kutumia viulizi “gani” na “-ngapi”.**

## Tathmini ya mada

1. Taja aina tatu za mazungumzo na kuzieleza
2. Nini umuhimu wa uigizaji wa mazungumzo?
3. Mwigizaji wa mazunguzo anastahili kuwa na sifa gani? Toa angalau tano
4. Kwa kutegemea mifano mitatu, onyesha mandhari au pahali panapoweza kuigiziwa mazungumzo.
5. Toa maswali sahihi kwa sentensi zifuatazo:
   i. Barabara hii ilijengwa kabla ya Wazungu kufika nchini humu.
   ii. Mtoto wangu hakuweza kufika shuleni jana kwani alikuwa mgonjwa.
   iii. Tunakuja shuleni kwa miguu.
   iv. Maswali kumi yametolewa na washiriki.
   v. Wazazi pamoja na walimu ndio watu muhimu katika jitihada za kuimarisha elimu bora.
   vi. Mgeni amepiga hodi.

# MADA YA 7 UTUNGAJI WA INSHA

**Uwezo mahususi wa mada** : Kutunga insha fupifupi kwa kuzingatia kanuni za utungaji na masimulizi.

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kueleza maana ya insha,
- Kutofautisha aina za insha,
- Kujadili umuhimu wa insha,
- Kutunga insha kwa kuzingatia kanuni za utungaji wa insha,
- Kutumia kwa usahihi alama za vituo husika.

**Kidokezo**

**Zungumzia aina mbalimbali za maandishi au masimulizi unazozijua.**

## SOMO LA 25: DHANA YA INSHA

### 25.1. Kusoma na ufahamu: Mchuano wa fainali



Wiki iliyopita nilibahatika kutazama mchuano wa fainali ya kuwania kombe la Agaciro kati ya shule ya wasichana ya Elimu Bora na Tusonge Mbele kwenye uwanja wa michezo Amahoro.

Nilipofika nyumbani, wazazi wangu waliniuliza kwa mapana na marefu kuhusu mchezo huo kwa sababu mmoja kati ya wachezaji ni dada yangu, jina lake Umutesi Marie Alice.

Nilianza kuelezea wazazi kwanza historia ya timu hizo. Timu hizi mbili ni wapinzani sugu tangu jadi na jadi. Elimu Bora inajivunia historia nzuri kwa kushinda kombe hili mara kumi. Wao ndio mabingwa watetezi. Tusonge Mbele imeshinda kombe hili mara tatu. Mwaka jana walitimuliwa katika nusu fainali. Katika awamu hii, wana rekodi ya kutoshindwa katika mechi zote hadi kufikia fainali.

Timu zote mbili ziliingia uwanjani tayari kwa mapambano. Kwa ufupi, kila timu ilikuwa na golikipa mmoja. Elimu Bora waliweka wachezaji watatu katika safu ya ulinzi wao Wakati ambapo tusone mbele walichezesha wachezaji wanne katika safu hiyo hiyo. Timu ya Elimu Bora walitia wachezaji watano katika kiungo cha kati nao Tusonge Mbele waliwachezesha wachezaji watatu. Elimu Bora walikuwa na washambulizi wawili nao wakati ambapo tusonge mbere walikuwa na washambulizi watatu katika safu ya mashambulizi. Timu zote mbili zilikuwa na wachezaji wa akiba watano. Refa mkuu alipuliza kipenga nao wasaidizi wake wawili walikimbia pembeni mwa uwanja kuinua kijibendera. Mmoja alikimbia kushoto naye mwingine alikimbia kulia.

Manahodha wa timu zote mbili walisimama katikati ya uwanja kurusha sarafu ili kuamua timu inayoanzisha mpira. Mashabiki wa timu zote mbili walikuwa wanaimba nyimbo za kushangilia timu zao. Makochi wao walikaa pembeni mwa uwanja kushuhudia wasichana wao wakimenyana.

Naam, refa alipuliza kipenga. Mpira ulianzishwa pale na Ikirezi na Umutesi Marie Alice wa timu ya Elimu Bora. Elimu Bora walianza mchuano huo kwa kasi mno. Walitafuta bao la mapema. Tusonge Mbele nao walifanya shambulizi la kujibu. Kipindi cha kwanza kilimalizika bila goli kwa timu zote.

Katika kipindi cha pili, kila timu ilicheza vizuri. Kwenye dakika ya sabini kulikuwa hatari katika lango la Tusonge Mbele. Kayitesi alinawa mpira. Naam, kipenga kilipulizwa. Refa aliwapa Elimu Bora penalti. Shangwe na vifijo vikahanikiza huku na huko kutoka kwa mashabiki wa Elimu Bora. Kayitesi alionyeshwa kadi ya manjano. Ikirezi alisimama nyuma ya mpira ule tayari kufyatua mkwaju wa penalti. Kabatesi akaruka na kuupiga mpira ule ukapitia juu ya mtambaapanya wa goli hadi nje. Ilikuwa konakiki.

Konakiki hiyo ilipigwa na Umulisa. Uwamwiza alikimbilia mpira ule. Alipiga kichwa! Hatimaye Elimu Bora walipata goli la kwanza. Mashabiki wote wa Elimu Bora na makochi wao waliacha viti vyao huku wakijirusharusha kwa nderemo kama kulungu. Mashabiki wa Tusonge Mbele waliviinamisha vichwa

vyao mithili ya kondoo. Wachezaji wa Tusonge Mbele walipandwa na mori kwa goli walilofungwa. Walimzingira refa mkuu. Walidai kuwa Uwamwiza alikuwa ameotea. Nahodha wao, Mutoni, ambaye ni beki wa kupanda na kushuka alimiminia refa maneno makali. Refa alitia mkono katika mfuko wa nyuma ya kaptula na kuchomoa kadi nyekundu. Mutoni alionyeshwa kadi nyekundu kwa kukosa adabu. Alisindikizwa nje ya uwanja. Timu ya Tusonge Mbele walibaki na wachezaji kumi pekee.

Mchezo ulimalizika ikiwa ni goli moja la Elimu Bora kwa bila.

**Kazi ya 1:**

**Maswali ya ufahamu**

1. Timu hizi mbili ni zipi?
2. Timu hizo mbili zinagombania kombe gani?
3. Timu hizo zilikuwa marafiki? Eleza.
4. Historia ya timu hizo ilikuwa namna gani katika mchezo wa kandanda?
5. Mchezo ulimalizika vyema? Eleza.
6. Kwa sababu gani wazazi walitaka kusikiliza matokeo ya mchezo huo?
7. Kwa sababu gani Mutoni alipewa kadi nyekundu?
8. Kwa maoni yako, michezo ina umuhimu gani?
9. Ni vizuri kwa wasichana kucheza mchezo wa kandanda?

## 25.2. Matumizi ya msamiati kuhusu kifungu cha habari

**Kazi ya 2:**

**Eleza maana ya maneno yafuatayo kutoka katika kifungu cha habari ulichokisoma hapo juu kuhusu "Mchuano wa fainali"**

Kabumbu

Mchuano

Fainali

Kuwania kombe

Wapinzani

Bingwa tetezi

Nusu fainali

Safu ya ulinzi

Kiungo cha kati

Washambulizi

**Kazi ya 3:**

**Kamilisha sentensi kwa kutumia maneno yanayofaa kati ya haya yafuatayo:** *kabumbu, mchuano, fainali, kuwania kombe, washambulizi, kuinua kijibendela, mabingwa watetezi, refa, mashabiki, penalti.*

1. Elimu Bora ndiyo **...............** kwa sababu walishinda mara nyingi.
2. **.........**anachomoa kadi nyekundu na kumuonyesha Mutoni.
3. Kulikuwepo mashabiki wengi katika mchezo wa **..............**la Agaciro nchini Rwanda
4. **..............** ndio wanaofungia timu yao magoli mengi.
5. Mara nyingi **............**husababisha goli.
6. Wasaidizi wa refa wanamsaidia katika mchezo kwa**...................**
7. Timu ya Arsenal ina ……….. wengi nchini Rwanda.
8. Siku hizi wachezaji wa **.............**hulipwa hela nyingi.
9. Nchini Rwanda, **............**wa APR FC na Rayon Sport unatazamwa na watu wengi sana.
10. Katika mchezo wa **.............**kila timu hutakiwa kuwa bingwa.

## 25.3. Sarufi: Matumizi ya herufi kubwa

**Kazi ya 4:**

**Tazama herufi zinazopigiwa mstari na kueleza sababu ya kutumia herufi kubwa**

a. <u>M</u>jini <u>K</u>igali panajulikana kuwa na usalama pamoja na usafi.

b. <u>S</u>hule ya <u>M</u>takatifu <u>Y</u>ohana inawapokea wasichana na wavulana.

c. <u>J</u>ina lako ni nani? <u>N</u>inaitwa Peter. <u>J</u>ina jingine ?

**Maelezo ya matumizi ya herufi kubwa**

a. Hutumiwa kuanzishia sentensi: Tazama mfano ufuatao:

*Nilikuona jana.*

b. Herufi kubwa hutumiwa mwanzoni mwa majina au nomino pekee kama vile: majina ya watu, mahali, milima, mito, maziwa, nchi, mabara, siku za wiki, miezi ya kalenda, sikukuu, dini mbalimali, barabara, majina ya vitabu, visiwa, n.k.

c. Hutumiwa kuandikia anwani:

**Mfano:**

JINSI YA KUPANDA MITI

**Kazi ya 5:**

**Chunguza makosa ya kisarufi katika sentensi zifuatazo na kuyasahihisha.**

1. musanze ni mji mkubwa.
2. kalisa na uwineza ni wanafunzi wenye bidii.
3. miti hutupatia kivuli cha kupumzikia.
4. mwalimu anafundisha.
5. berwa anacheza mpira.

## 25.4. Matumizi ya Lugha: Dhana ya insha na utungaji wake

**Kazi ya 6:**

**Jadili maswali yafuatayo:**

a. Insha ni nini?

b. Toa umuhimu wa kujifunza insha.

c. Insha nzuri inastahili kuwa na sifa gani?

d. Kifungu hiki cha habari ni cha aina gani ya insha ?

**Maelezo muhimu kuhusu insha.**

**Maana ya insha:**

**Insha** ni mtungo wa kinathari unaozungumzia suala au kusimulia kisa fulani. Utungo huu huwa na urefu wa wastani. Kisa hicho au suala hilo ndilo mada ya utungo huo. Insha hutumiwa kueleza maoni ya mwandishi kuhusu masuala au mambo tofauti. Utungaji ni neno linalotokana na kitenzi **"tunga".** Kitenzi hiki kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004: 414) kinamaanisha "***Kutoa mawazo kutoka ubongoni na kuyakusanya, kisha kuyadhihirisha kwa maandishi, kwa kusimulia, kwa kuyaimba au kwa muziki.»***

Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa utungaji ni utoaji wa mawazo binafsi kutoka akilini mwa mtu kuhusiana na mambo mbalimbali katika jamii, kisha kuyaweka wazi kwa njia ya mdomo au maandishi.

**Sehemu kuu za insha:** Insha hugawika katika sehemu kuu tatu ambazo ni pamoja na:

- **Utangulizi (mwanzo)**

Katika sehemu hii inampasa mwandishi/ mtungaji atoe maelezo mafupimafupi na maana ya habari aliyopewa.

- **Kiini cha insha (Kati au mwili)**

Inamlazimu mwandishi afafanue kwa mapana na marefu mada anayoishughulikia huku akitoa mifano hai inayoendana na hali halisi ya maisha ya mtu kijamii. Kwa kawaida sehemu hii hueleza kwa ukamilifu kila hoja iliyodokezwa katika utangulizi.

- **Hitimisho na mwisho**

Inampasa mwandishi kutoa mapendekezo (maoni) ya msingi au kusisitiza kwa ufupi yale aliyoyaeleza katika habari yenyewe. Mwisho wa insha huonesha uhusiano uliopo kati ya utangulizi na maelezo yaliyomo katika mwili.

## 25.5. Kusikiliza na kuzungumza

**Kazi ya 7:**

**Fikiria juu ya insha moja uliyoisikiliza au kusoma na kuisimulia mbele ya darasa**

## 25.6. Kuandika: Utungaji wa insha


**Kazi ya 8:**

**Kutokana na mfano wa insha uliotolewa hapo juu, andika insha kuhusu mada ifuatayo:**

"Umoja wa Afrika ni Msingi Muhimu kwa Maendeleo ya Afrika"

## SOMO LA 26: AINA ZA INSHA







**Kazi ya 1:**

**Jadili michoro hii kwa kuelekea kwenye insha**

## 26.1. Kusoma na ufahamu: Usafi wa mavazi yetu



Vazi ni nguo ya aina yoyote inayovaliwa mwilini. Binadamu huhitaji mavazi kujikinga dhidi ya hali ya hewa ya aina mbalimbali. Wakati wa joto huhitaji vazi jepesi na wakati wa baridi huhitaji vazi linaloweza kumtilia joto mwilini. Hii ndiyo sababu wakati wa baridi watu hujifunika mavazi kama migolole, makoti, makabuti, kaniki, vikoi, na sweta .

Mavazi ni pambo kwa binadamu. Vazi humfanya mtu aonekane maridadi na apendeze zaidi. Labda, hii ndiyo sababu ya kuwepo kwa aina mbalimbali za mavazi na mitindo tofauti inayomfanya mtu avutie.

Mavazi huonesha utamaduni wa watu. Kusema kwamba mtu akivaa nguo ya mtindo fulani mara nyingi utamaduni wake au asili yake hutambulika waziwazi. Hata mtu awe mweupe anayetoka Ulaya au Marekani, akivaa mgolole, kanga, kitenge, atakuwa akiiga vazi la utamaduni wa Afrika kwa ujumla. Hadi leo, kuna mavazi unayoweza kusema kuwa ni ya Kichina, Kihindi, Kiarabu, Kizungu, Kinyarwanda, Kiganda, Kimasai na kadhalika.

Tena mtu anaweza kuvaa nguo kwa mtindo wa aina fulani akafikiriwa kuwa ni Mkongomani, Mganda, Mmasai, raia kutoka Afrika Magharibi na kadhalika.

Mavazi ni ya aina nyingi na mitindo tofauti. Lakini mavazi hayo yote huweza kupangwa katika aina kuu tatu: mavazi ya kike, ya kiume na mavazi mahususi.

Kwa upande wa kwanza, mavazi ya kike ni mavazi ambayo kwa kawaida

huvaliwa na watu wa jinsia ya kike. Kuna mavazi au nguo za ndani, ambazo huvaliwa na wanawake na hazipaswi kuonekana ovyo. Na hizo ni kama chupi, fulana, sidiria na shimizi.

Tena, kuna nguo za nje ambazo ndizo zionekanazo mara nyingi. Hizo ni kama sketi, blauzi, shati, jaketi, gauni, kanga, kaniki, kitenge, kaptula, suruali na kadhalika.

Kwa upande mwingine, wanaume nao huwa na nguo za staha yaani nguo za ndani kama chupi na fulana. Pia, wana nguo zinazoonekana nje kama kaptula, suruali, shati, koti, tai, suti, kanzu na kadhalika.

Zaidi ya hayo, kuna mavazi mahususi ambayo ni mavazi rasmi kwa ajili ya shughuli maalum au kazi maalum. Mfano wa mavazi haya ni kama mavazi ya viongozi wa kidini, masista, makasisi, mapadri na mashehe. Kundi la aina hii huwa na nguo zao maalum kwa ajili ya kazi zao na pia huwasaidia kujitambulisha kwa urahisi kwa umma au jamii. Baadhi ya nguo hizo ni kama kasiki, joho, kanzu, kilemba na nguo zinazofanana na hizo.

Mfano mwingine ni mavazi rasmi kama ya askari jeshi, askari polisi, askari magereza, wafanyakazi wa forodha, walinda usalama wa mashirika ya kujitegemea, waganga na wauguzi, wafanyakazi wa mashirika ya ndege, wachezaji na hata wanafunzi. Hawa wote wana mavazi yao rasmi kwa ajili ya shughuli zao. Mtu akivaa nguo ya aina fulani, hujitokeza kuwa yeye ni mtu wa namna fulani au kazi fulani.

Mavazi yetu yote ni lazima yawe na usafi. Usafi wa mavazi yetu ni muhimu sana kwa sababu jambo hili husaidia mambo mengi maishani mwetu. Kwanza tunaposafisha nguo zetu, tunajiepusha na magonjwa yanayotokana na wadudu wanaoweza kuishi katika nguo chafu.

Wadudu hawa ni kama chawa, viroboto na kadhalika.

Nguo chafu hasa zile za ndani huweza kusababisha madhara katika sehemu za uzazi na kuleta magonjwa mbalimbali kutokana na vidudu ambavyo vinaweza kusababishwa na uchafu.

Pili, mtu akiwa na nguo chafu hutoa harufu mbaya ambayo husumbua wenzake wanapomsogelea.

Kwa ujumla, mavazi yetu ni ya aina nyingi na mitindo tofauti. Mavazi haya yana umuhimu sana katika maisha yetu. Ndiyo maana tunalazimika kuyatunza vizuri na kuyasafisha ili tuwe na usafi wa kutosha. Usafi huu lazima uende bega kwa bega na usafi wa miili yetu.

(Kifungu hiki msingi wake ni kutoka: Ndalu A. (1997) Mwangaza wa Kiswahili, East African Educational Publishers Ltd, Nairobi, Kenya.

## Kazi ya 2:

**Maswali ya Ufahamu:**

1. Vazi ni nini ?
2. Kwa sababu gani vazi ni kifaa muhimu sana kwa binadamu?
3. Taja aina kuu tatu za mavazi.
4. Ni kwa namna gani vazi linavyoweza kutambulisha utamaduni wa anayevaa vazi hilo? Eleza kwa kutoa mifano ya kutosha.
5. Taja mifano mitatu ya nguo mahususi.
6. Veli linaweza kutambulika kama vazi la aina gani miongoni mwa aina za mavazi tulizotaja hapo juu?
7. Eleza jinsi ambavyo mavazi hutegemea sana utamaduni wa jamii husika?
8. Taja majina ya wadudu wanaoishi ndani ya mavazi machafu.
9. Kwa sababu gani nguo zilizofuliwa ni lazima zipigwe pasi baada ya kukaushwa na jua?
10. Ni ushauri gani unaoweza kutoa kulingana na kifungu hiki?

## 26.2. Msamiati kuhusu kifungu cha hatari

## Kazi ya 3:

**Tazama kwa makini jedwali hili. Bainisha msamiati mbalimbali na kueleza maana yake.**

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | C | V | K | I | T | E | N | G | E |
| S | H | I | I | A | Z | A | P | A | L |
| K | U | R | K | F | N | M | I | U | U |
| T | P | A | O | F | U | I | E | N | B |
| S | I | D | I | R | I | A | K | I | E |
| O | S | H | A | T | I | K | A | I | G |
| K | A | B | U | T | I | U | S | N | A |
| S | U | R | U | A | L | I | I | U | N |
| I | S | U | K | I | L | O | K | B | N |
| V | E | L | I | S | U | T | I | Y | P |

## Kazi ya 4:

**Unganisha msamiati kutoka sehemu A na maana yake kutoka sehemu B.**

| A | B |
|---|---|
| 1. Kimono | a. aina ya kofia kubwa na pana. |
| 2. Chupi | b. soksi ndefu za wanawake zinazofika kiunoni |
| 3. Bwelasuti | c. kanzu ya kasisi. |
| 4. Pajama | d. Si aina ya vazi. |
| 5. Shumburere | e. Nguo nyepesi ya wanawake yenye maandishi. |
| 6. Stokingi | f. Hutumiwa kwa kuchezea mchezo wa kung'fu |
| 7. Tarbushi | g. sawa na surupwenye |
| 8. Kanga | h. nguo ndogo inayovaliwa ndani ya kufunika uchi. |
| 9. Kasula | i. mavazi ya kulalia. |
| 10. Kalavati | j. kofia yenye shada la nyuzi ndefu. |

## 26.3. Sarufi: Matumizi ya alama za vituo

**a. Matumizi ya nukta ( . )**

## Kazi ya 5:

**Tazama sentensi zifuatazo na kuzungumzia matumizi ya alama yanayojitokeza.**

i. Usafi ni muhimu sana kwa maisha ya binadamu.
ii. Kalisa alienda sokoni. Alikutana na rafiki yake sokoni.
iii. Tunasoma ili tupate elimu.

**Maelezo muhimu**

**Nukta**

a. Huwekwa mwishoni mwa sentensi sahili sahihi. Kwa mfano

i. Tunakula mboga kwa ajili ya afya nzuri
ii. Inatubidi kusafisha mahali tunapoishi.

b. .Hutumiwa kuonyesha ufupisho wa maneno. Kwa mfano:

i. S.L.P. – Sanduku la Posta
ii. Bi. – Bibi

c. Hutumika kubainisha saa na dakika au tarehe. Kwa mfano:

i. 3.20 – saa tisa na dakika ishirini

ii. 14.5.2016- tarehe kumi na nne, mwezi wa tano, mwaka wa mbili elfu kumi na sita

d. Hutumiwa kuonyesha vipashio vya pesa. Kwa mfano:

sh.10.50- shilingi kumi na thumuni hamsini

e. Zikitumiwa mara tatu mfululizo (…) huonyesha kutokamilika kwa sehemu husika

Kwa mfano: Nitakupa lakini ni sharti...

**Kazi ya 6:**

**Chunguza sentensi hizi na kusahihisha makosa ya kisarufi.**

1. mwalimu anaandika ubaoni
2. mifano ya ndege ni kv kuku, mwewe na bata
3. tulianza mitihani yetu tarehe 12122017
4. bi mutoni anaendesha gari
5. wanafunzi wanasoma darasani

**b. Matumizi ya koma / mkato ( , )**

**Kazi ya 7:**

**Tazama sentensi zifuatazo na kuzungumzia matumizi ya alama yanayojitokeza.**

1. Nimemkuta mzee, nikamwuliza shida zake, nikamsaidia kupata gari la kumpeleka nyumbani.
2. Tumekuja kwa ajili ya akili, si kwa ajili ya pesa.
3. Baadhi ya maadili na thamani Mnyarwanda anatakiwa kuwa na zo ni kama vile utu, unyarwanda, ushirikiano na ushujaa.

**Maelezo muhimu**

**Mkato / koma**

a. Hutumiwa kuonyesha pa kutua kwa muda mfupi katika sentensi. Kwa mfano:

ii. Nilipowasili nyumbani, nilienda kuteka maji kisimani.

iii. Kwa kuwa tulijiandaa vilivyo kwa mtihani wa kitaifa, tulipita.

b. Hutumiwa kutenga maneno yaliyo katika orodha:

i. Nenda sokoni ununue mboga, nyama, mafuta, na unga.

ii. Mwanafunzi huyu ni mtiifu, mwerevu, mtanashati, na mwenye bidii.

c. Hutumiwa kubainisha sehemu mbili za sentensi zilizo kinyume:

i. Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.

ii. Aliniambia atakuja, hakuja.

d. Hutumiwa kabla ya alama za mtajo.

**Kwa mfano:**

Mama akasema, “Niletee chumvi.”

e. Hutumiwa wakati sentensi inapoanza kwa kiunganishi.

**Kwa mfano:**

Kweli, alikuwa mtu mwovu.

f. Hutumiwa unapoita mtu ili kupata usikivu wake kabla hujamwambia chochote. Kwa mfano:

Nkusi, niletee kalamu.

g.Hutumiwa unapokubali au unapokataa kitu. Mfano:

i. Ndiyo, nitakuja.

ii. Hapana, sitakulipa.

**Kazi ya 8:**

**Sahihisha makosa ya kisarufi katika sentensi zifuatazo**

1. Baba alinunua daftari kalamu rula na kifutio
2. Mama alipofika sokoni alinunua nanasi mkate chungwa na parachichi
3. Familia yetu ina watoto wafuatao: Kabanda Kabalisa na Mukandoli
4. Mwalimu wetu anatufundisha masomo ya Kiswahili Kiingereza na Historia
5. Katika lugha ya Kiswahili kuna alama za uandishi kama vile: nukta mkato alama ya kuuliza ….

## 26.4. Matumizi ya lugha: Ainaza insha

**Kazi ya 9:**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Kifungu " Usafi wa mavazi" ni aina gani ya insha?
2. Kifungu ***"Mchuano wa fainali"*** ni aina gani ya insha?

**Maelezo muhimu kuhusu aina za insha**

Insha ni za aina nyingi kulingana na namna zilivyoandikwa au kufuatana na kusudi lake. Katika utungaji wa insha kuna :

**1. Insha za wasifu**

Insha za wasifu ni aina ya utungaji ambao huchora picha ya kitu kinachozungumziwa. Huonyesha waziwazi hisia za msanii. Aghalabu, kuna vitu vingi ambavyo tunaviona kila siku kama vya kawaida lakini mtungaji anaweza akavitungia insha za wasifu na tukaviona katika mtazamo tofauti kabisa. Katika insha za wasifu kuna usanii wa kueleza sifa za mtu, mahali au kitu fulani.

**2. Insha ya mjadala au ya mdahalo**

Inalenga mara nyingi kulieleza jambo na vile vile kuhimiza mtazamo fulani. Hata hivyo, jambo lililo muhimu zaidi si kueleza bali ni kujibidiisha kushawishi. Katika mdahalo shawishi, mwandishi hulenga katika kuathiri hisia na maoni ya msomaji kwa njia ya kumfanya achukue hatua. Insha hii huhusisha mada ambayo mwanafunzi anapaswa kuitetea au kuipinga katika kisa chake. Hoja nyingi na nzito hutolewa kwenye upande anaounga mkono.

### 3. Insha fafanuzi

Katika aina hii ya insha, mwandishi hutumia mifano kufafanua au kutilia mkazo hoja yake. Anaweza kutumia mfano mmoja wenye uzito au mifano mingi yenye kuhusiana.

**Mfano: Rushwa imepigwa marufuku nchini Rwanda.**

### 4. Insha ya methali

Insha ya methali ni utungo unaoandikwa kwa kuzingatia methali. Kisa au maelezo yatolewayo huwa yanaongozwa na maana iliyomo katika methali husika. Kabla ya kuanza kuandika insha, ni bora kwanza kuielewa vyema maana ya methali au maudhui yake. Mbali na kufahamu maana ya kijuujuu ya methali, inambidi mtunzi wa insha kuelewa mazingira (miktadha mingine ambapo methali husika inaweza kutumiwa). Kwa mfano: Akili ni nywele kila mtu ana zake. Hapa, anayetunga insha hii lazima aeleze maana ya juu na ya ndani ya methali. Pia, msamiati uliotumiwa hufafanuliwa.

### 5. Insha ya mdokezo

Insha ya mdokezo ni aina ya utungo ambao huandikwa kwa kuongozwa na maneno aliyopewa mtunzi wake. Maneno hayo yaliyotolewa ndiyo mwongozo wa kumwelekeza mwandishi kuhusu maudhui atakayoandika. Lililo muhimu ni kuhakikisha kuwa mtungo utakaoandikwa unaoana vizuri na maneno yaliyotolewa kama mwongozo.

**Mfano:** Nilipofika katika eneo la tukio hilo, sikuamini niliyoyaona .................

Hapa, unaweza kuendeleza kidokezi hiki kwa kukitungia kisa mwafaka.

### 6. Insha za picha

Insha za picha ni zile ambazo msingi wake wa kuzitunga ni picha ambazo huwa zimechorwa na ambazo humwongoza mwandishi kubuni hadithi au kisa kinachooana na picha hizo. Kimsingi, huhitaji ufasiri wa picha zilizo kwenye ukurasa na kuibuni hadithi kuzihusu.

Hivyo basi huwa ni insha za kusimulia.

### 7. Insha ya mawazo au ya kubuni

Insha hizi zinahusu jambo la kufikiriwa. Jambo linalojadiliwa katika aina hii ya insha huwa halitokani na hali au tukio halisi katika maisha. Vipengele vyote vinavyoijenga hubuniwa na mtunzi wake. Maudhui, wahusika, mandhari vya mtungo wa aina hii vyote hubuniwa katika fikra ya mtunzi.

8. **Insha ya kitawasifu (Insha elezi/ ya maelezo)**

Insha hii huwasilisha sifa za vitu, watu, hali, matendo, mahali au hata sherehe uliyohudhuria. Inalenga kutoa picha ya kitu katika akili zetu jinsi ambavyo kinamdhihirikia anayekiona. Ili kuandika insha ya maelezo, mwandishi wake anahitaji kwanza kabisa kukusanya habari za kina kuhusu jambo analoliandikia. Hategemei tu yale ambayo yanaonekana kwa macho bali pia aina nyingine za hisi kama vile kugusa, kuonja, kunusa, kusikia na kadhalika. Hali hii humwezesha msomaji kupata taswira kamilifu kuhusu jambo linaloelezewa kupitia viungo vya kuona, kuonja, kugusa na kusikia.

9. **Insha ya masimulizi**

Insha ya masimulizi ni insha yenye kuhadhiria tukio au hali fulani. Ni utungo ambao husimulia au kueleza kisa. Dhima yake ni kuburudisha au kuteka umakini wa msomaji. Kwa kuwa inalenga hadhira ni muhimu kufahamu na kuitambua hadhira yako kabla ya kuandika utungo wako

## 26.5. Kusikiliza na kuzungumza

**Kazi ya 10:**

**Jadili mada zifuatazo**

1. Mavazi ya kigeni yana athari kubwa katika utamaduni wa Wanyarwanda
2. Matumizi ya mtumba (mavazi) huleta hasara kwa Wanyarwanda.

## 26.6. Kuandika

**Kazi ya 11:**

**Tunga insha ya wasifu unayotaka yenye ukurasa mmoja.**

# SOMO LA 27: INSHA YA MASIMULIZI



**Kazi ya 1:**

**Unaona nini kwenye mchoro hapa juu?**

## 27.1. Kusoma na ufahamu: Mafanikio ya kudumu

Ilikuwa tafrija ya kijiji kizima, tuliposherehekea siku ya kupata tuzo kwa kijana hodari ambaye aliyamudu maisha yake kiasi cha kuigwa na vijana wengine. Kabatesi, kijana aliyezaliwa mwanapekee katika familia yake hakubahatika kulelewa na wazazi wake kwani walifariki angali mdogo akachukuliwa na kulelewa na shangazi yake.

Alipomaliza masomo yake katika shule za sekondari, Kabatesi alipata cheti cha kuhitimu masomo ya sekondari huku akiwa na alama nzuri. Jambo hili liliwafurahisha watu wengi: walimu na majirani zake. Alikuwa mwanafunzi mwenye bidii tangu shule za chekechea hadi kiwango alichofikia. Muda mfupi baadaye, alijiunga na vijana wenzake kufuata masomo ya muda mfupi yaliyokuwa yakitolewa kijijini mwake. Masomo hayo ni kuandaa miradi midogo midogo ya kujiendeleza na jinsi ya kuifanikisha.

Alipokubaliwa kufuata mafunzo pamoja na vijana wengine alielewa kwamba hiyo ilikuwa njia nzuri ya kupata suluhisho na ufumbuzi wa tatizo lililokuwa likimkera kwa muda mrefu. Mafunzo yalifanyika kwa muda wa mwaka mzima, akapewa cheti katika fani ya maandalizi na utekelezaji wa miradi ya kimaendeleo.

Mwezi mmoja uliofuata, Bodi ya Maendeleo Rwanda ilihitaji kuajiri vijana waliokuwa wamemaliza masomo yao katika mkondo wa lugha ili wasaidie katika kazi za ukalimani na uongozaji wa watalii kwenye vivutio vya utalii.

Kabatesi alipeleka ombi lake na baada ya muda mfupi akaitwa kwa mtihani. Hili lilikuwa jambo jepesi kwake kwani aliufaulu vizuri mtihani na hivyo akaajiriwa na bodi hiyo. Alifanya kazi yake kwa bidii kiasi kwamba watalii wengi walifurahia huduma yake, wakampenda kwa uwezo wake wa kuzungumza lugha nyingi tofauti na bidii aliyoonesha kazini.

Kabatesi alifungua akaunti kwenye benki moja na kuanza kuhifadhi sehemu ya mshahara wake. Kwa kweli, alikuwa msichana asiyekata tamaa na kila aliposhikilia jambo alilifuatilia mpaka lilipokamilika. Kwa hivyo, alipoona akaunti yake imeshakua na pesa za kutosha, aliamua kuomba mkopo ili aweze kutekeleza mengi aliyokuwa amejifunza katika maandalizi na utekelezaji wa miradi ya kimaendeleo. Mawazo yake yalikuwa kwenye shamba lake kubwa aliloachiwa na wazazi ambalo mpaka wakati huo lilikuwa halijatumiwa vizuri. Aliandaa vizuri mradi wa kilimo na ufugaji, akajenga vibanda vya mifugo yake, akawaajiri baadhi ya vijana waliokuwa pamoja katika mafunzo ya muda ule mfupi, kila mmoja akapewa jukumu lake.

Pamoja na kazi yake ya ukalimani, Kabatesi alifuata vizuri mradi wake akanunua vifaa vilivyohitajika. Ninakumbuka kuwa mwaka jana, serikali yetu ilipotoa tuzo kwa watu waliochangia kubadilisha maisha ya watu wengine, Kabatesi alikuwa miongoni mwa watu waliochangia kuyaboresha maisha ya majirani zake. Kwa sasa ameanza kuendelea na masomo yake katika Chuo kikuu cha Rwanda.

Kabatesi amekuwa mfano mzuri kwa vijana wengine wengi ambao wanayakumbuka maisha yake, huyaamini yaliyosemwa na wahenga kwamba” Mchumia juani hulia kivulini” na “mvumilivu hula mbivu”.

Wema kwa kila mtu, utulivu na upendo ni baadhi ya sifa zinazomtambulisha kijana huyu ambaye amewashangaza wengi wanaofahamu alipotoka.

## Kazi ya 2:

**Maswali ya ufahamu**

1. Eleza hali ya maisha ya Kabatesi alipokuwa mtoto mdogo.
2. Kwa nini Kabatesi alipewa zawadi nyingi baada ya kumaliza masomo yake ya shule za Sekondari?
3. Masomo ya muda mfupi aliyoyafuata yalikuwa yanahusu nini?
4. Eleza jinsi ambavyo Kabatesi aliweza kufaidika kutokana na masomo ya muda mfupi.
5. Eleza jinsi ambavyo Kabatesi aliweza kufaidika kutokana na masomo yake ya Sekondari.
6. Ni mambo gani yanayokudhihirishia kwamba Kabatesi alikuwa kijana asiyekata tamaa?
7. Eleza jinsi ambavyo Kabatesi aliweza kuboresha maisha ya watu wengine.
8. Kwa nini Kabatesi alipewa tuzo?
9. Kwa kifupi, eleza tabia na mienendo ya Kabatesi.
10. Kwa nini Kabatesi anachukuliwa kuwa mfano kwa vijana wengine?
11. Umepata funzo gani kutokana na kifungu hiki?
12. .Kulingana na kifungu hiki, eleza maana ya methali hizi:
    a. Mvumilivu hula mbivu.
    b. Mchumia juani hulia kivulini.

## 27.2. Matumizi ya msamiati kuhusu kifungu

**Kazi ya 3:**

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. Kuandaa
2. Karo
3. Tafrija
4. Ajira
5. Hodari
6. Kukata tamaa
7. Akaunti
8. Tuzo
9. Mradi

**Kazi ya 4:**

**Husisha maneno kutoka sehemu A na maana yake kwenye sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Mkalimani | a. Malipo ya mwezi anayopewa mwajiriwa kwa kazi aliyofanya; janguo |
| 2. Utalii | b. Cheti maalumu chenye hadhi ya chini kuliko shahada. |
| 3. Shahada | c. Mali inayotumika kuanzishia au kupanulia biashara au shughuli yoyote ya kuzalisha mali. |
| 4. Mshahara | d. Matendo ambayo mtu amezoea kuyafanya mara kwa mara; mwenendo; mazoea; desturi |
| 5. Yatima | e. Mwito wa kumtaka mtu au watu kuhudhuria mahali |
| 6. Stashahada | f. Mtu afasiriye papo kwa papo mazungumzo kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine |
| 7. Mtaji | g. Kuendelea kuishi au kuwepo kwa muda wote. |
| 8. Mwaliko | h. Cheti au karatasi maalumu anayopewa mtu baada ya kupata mafunzo fulani katika chuo kikuu. |

| | |
|---|---|
| 9. Tabia | i. Mtoto ambaye mzazi wake au wazazi wote wamekufa. |
| 10. Kudumu | j. Hali ya kusafiri mbali au kuvinjari huku na huko ili kuyafurahia mandhari |

**Kazi ya 5:**

**Kamilisha sentensi kwa kutumia maneno unayoona yanafaa kati ya yafuatayo**: *Bidii, inawapongeza, utulivu, majukumu, vibanda, shule za chekechea, ukalimani*

1. Nchini Rwanda watoto wengi wanaanzia masomo yao katika……
2. Wanafunzi wanalazimishwa kusoma kwa ............ ili waweze kufaulu mtihani wa taifa.
3. Kuna uhusiano wa karibu wa kazi ya .......... na tafsiri.
4. Wanafunzi wenye tabia ya ........ wanapata alama nzuri katika masomo yao.
5. Serikali ya Rwanda .......... na kuwahimiza wasichana wanaosoma sayansi na teknolojia.
6. Wazazi wana ....... ya kuwalisha na kulipa karo za watoto wao.
7. Mjomba wangu alijenga ......... vitatu vya kuku wake

## 27.3. Sarufi: Matumizi ya alama za vituo

### a. Matumizi ya alama ya kuuliza/ ulizo ( ? )

**Kazi ya 6:**

**Tazama sentensi zifuatazo na kuzungumzia matumizi ya alama inayojitokeza.**

i. Unasema nini?

ii. Mnafanya nini hapa ?

iii. Je, jina lako nani ?

iv. Kwa sababu gani wototo wanapaswa kuheshimu wazazi wao ?

**Maelezo muhimu**

Alama ya kuuliza au ulizo hutumiwa mwishoni mwa sentensi kuonyesha kuwa sentensi hiyo ni swali.

**Kwa mfano:** Unaitwa nani?

### Kazi ya 7:

**Sahihisha sentensi zifuatazo:**

1. Unasoma kitabu kipi
2. Mwalimu wako wa Kiswahili anaitwa nani
3. Je, unakunywa chai
4. Kwa nini unapiga kelele darasani
5. Unachora nini

**b. Matumizi ya alama ya mshangao ( ! )**

### Kazi ya 8:

**Tazama sentensi zifuatazo na kuzungumzia matumizi ya alama inayojitokeza.**

i. O lalala! Baba yako amekufa!

ii. Gooooo ! Amefunga goli!

**Maelezo muhimu**

Alama ya mshangao hutumiwa kuashiria mahangaiko ya moyo kama vile hasira, hofu, mshangao na kadhalika.

i. Lo! Mwanafunzi ameangusha kitabu cha mwalimu matopeni.

ii. Wamefungwa mabao kumi kwa nunge!

### Kazi ya 9:

**Chunguza sentensi zifuatazo na kuzisahihisha**

1. Ala umebeba mzigo huo pekee yako
2. Hoyee wanariadha wametunzwa medali
3. Pesa zangu zimeibiwa
4. Nimepita mtihani wangu wa kitaifa
5. Lo Akimana ameanguka chini

## 27.4. Matumizi ya lugha: Sifa za inshe ya masimulizi

**Kazi ya 10:**

**Je, kifungu "Mafanikio ya kudumu" ni aina gani ya insha? Toa maelezo.**

**Maelezo muhimu**

**Sifa kuu za aina hii ya insha:**

- Matamshi na lafudhi ni lazima yawe sahihi.
- Ni lazima mazungumzo haya yagawanyike katika sehemu kuu tatu: ***mwanzo, kati,*** na ***mwisho***.
- Utungaji wa masimulizi ni lazima uzungumzie ukweli wa jambo linalozungumziwa.
- Uwasilishaji wa hali, matukio, na mazingira yanayodhihirika waziwazi.
- Mtiririko wa mawazo wenye mshikamano.
- Msimuliaji ni lazima azungumze kwa nidhamu na kwa lugha sanifu inayoeleweka kwa watu wote.

Mfululizo wa matukio ya haraka haraka.

- Masimulizi yawe ya kupendeza sana, pengine ya kuchekesha na yenye kuteka hisia kwa maelezo ya kushangaza au yenye kujaa taharuki.
- Kutoa funzo maalumu kutokana na hadithi yenyewe, yaani maadili fulani kuhusu maisha kwa ujumla.

## 27.5. Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

**Kazi ya 11:**

**Serikali ya Rwanda inawahimiza wananchi kujitafutia ajira kutokana na uhaba wa kazi. Jadili kuhusu namna ya kujitafutia kazi.**

## 27.6. Kuandika: Utangazaji wa insha ya masimulizi

**Kazi ya 12:**

**Baada ya kusoma kifungu kuhusu insha za masimulizi "Mafanikio ya kudumu," tunga insha ya masimulizi kuhusu tukio fulani, kisa au tukio la kweli au la kubuni kwa kuheshimu vipengele muhimu vya insha ya msimulizi na taratibu zake.**

## SOMO LA 28: MWONGOZO WA KUTUNGA INSHA




**Kazi ya 1:**

**Unaona nini kwenye mchoro hapa juu?**

### 28.1. Kusoma na kufahamu: Siku yangu ya kwanza katika shule za mabweni



Mwanzo wa masomo yetu ulipokaribia kufika, wazazi wote walianza kujiandaa kwa kutimiza wajibu wao wa kuwanunulia watoto wao mahitaji kwa ajili ya masomo yao katika shule za sekondari. Wazazi wangu nao waliwajibika kuninunulia mahitaji yote muhimu yaliyohitajika.

Ulikuwa wakati wa mwanzo wa mwaka, shule za msingi na za sekondari zilifungua tayari kwa kuanza masomo. Mimi niliamka asubuhi na mapema nikatoka nyumbani saa kumi na mbili kamili. Baba, mama, dada na kaka zangu wawili walinisindikiza umbali wa takribani kilomita mbili toka nyumbani kabla ya wengine kurudi nyumbani isipokuwa baba. Baba yangu alichukua begi langu lililokuwa zito nami nikachukua ndoo na godoro langu tukaendelea mpaka kituo cha basi.

Tulipofika njiani, baba yangu aliniambia kwa sauti ya upole akisema: “Mwanangu, nenda ukasome kwa bidii. Wakati ni mali, kamwe usiuatili. Kumbuka kuwa tumewauza mbuzi wetu wawili ili tuweze kukutafutia vifaa vyote unavyohitaji. Huko shuleni utakutana na vijana wengi wenye tabia tofauti. Tafadhali, usishabihiane na wanafunzi wabaya ambao hawazingatii maonyo na mawaidha ya wazazi wao na walimu”. Nami nilifikiria kidogo ili niweze kumpa baba yangu jibu kutokana na yale aliyoniambia. Hatimaye nilipata cha kumuambia baba. “Baba! Sitakusaliti kamwe! Malezi uliyonipa tangu utotoni mwangu nitayatilia maanani; nitajifunza kwa bidii kama unavyonitakia. Sitalandana na vijana hao wasio na maadlili mema.” Baada ya kusikia hayo, baba yangu alitikisa kichwa kuonyesha kukubaliana nami kuhusu mwelekeo wangu wa maisha katika mazingira niliyokuwa natarajia kuingia.

Tuliendelea na safari mpaka tulipofika kwenye kituo cha basi. Huo ulikuwa mwendo wa saa moja tu kwa miguu.

Kwenye kituo cha basi, kulikuwa na wanafunzi wengi lakini mabasi yalikuwa machache. Baada ya dakika thelathini, basi lilikuja tukaingia sote. Mimi nilikaa upande wa dirisha na baba alikaa karibu nami.Tuliendelea na safari yetu mpaka shuleni. Kufika hapo, tulielekea kwenye ofisi ya mwalimu mkuu wa shule ili tujitambulishe na kujisajilisha. Hapo nje palikuwa na umati wa wanafunzi waliokuwa wakielekezwa kwenye mabweni yao na wengine wakifanya shughuli za usafi. Labda hao walikuwa wenyeji wa shule hiyo kwani walikuwa wakizungumza na kucheka kwa furaha kubwa pasipo wasiwasi wowote.

Tulipiga hodi ofisini tukapokelewa vyema. Hedimasta alituuliza habari kamili, tukamwelezea yote halafu nilielekezwa kwa katibu ambaye alinisajili baada ya kuonyesha stakabadhi ya malipo ya karo ya shule. Mfanyakazi huyu alimwita afisa wa nidhamu ili anipeleke bwenini na kunionyesha kitanda changu. Hapo hapo nilimuaga baba yangu, naye akarudi nyumbani baada ya kunitakia kila heri na fanaka katika masomo yangu.

Nilipofika bwenini nilishangaa sana kuona vitanda vingi katika ukumbi mkubwa ambapo kila kitanda kilikuwa na sehemu mbili za kulala, moja chini na nyingine juu yake. Nilitandika godoro langu kwenye sehemu ya chini ya kitanda. Hata hivyo, nilikuwa na hofu kubwa moyoni kuwa yule atakayelala juu yangu siku moja anaweza kuniangukia. Lakini nilijikaza kiume nikafikiria kwamba hayo yalikuwa mazoea yao na kwamba shule haingekubali kuendeleza hali hiyo kama kungetokea tatizo kama hilo.

Baadaye, kengele ililia kuwaita wanafunzi wote kuingia bwaloni kupata chakula cha jioni. Chakula kilikuwa kizuri. Siku hiyo tulikula wali, maharagwe, mboga na matunda.

Tulipomaliza kula tuliambiwa kuingia madarasani mwetu kwa masomo ya kibinafsi. Sisi sote tuliingia darasani, kila mwanafunzi alichukua daftari fulani alilotaka na kuanza kujikumbusha yale tuliyokuwa tumesoma hapo awali. Mimi nilichukua daftari langu la somo la Kiswahili nikaanza kupitia masomo yote tuliyojifunza katika kidato cha tatu. Shughuli hii iliendelea mpaka saa tatu za jioni ambapo kengele ililia tena kuashiria kuenda mabwenini kulala. Mumo humo, tulilala kwa utulivu mpaka asubuhi tulipoamka kuanza masomo yetu.

Kwa hakika, siku hiyo ya kwanza ya masomo yangu katika shule za mabweni ilikuwa siku ya furaha na ugunduzi wa mambo mengi yanayohusu mazingira ya shule hizo ambayo sikuyajua. Nilifurahia maonyo niliyopewa na wazazi wangu na jinsi nilivyopokelewa na kuelekezwa na kila mmoja niliyemkuta katika shule yangu.

## Kazi ya 2:

**Maswali ya Ufahamu**

1. Eleza shughuli za wazazi kila wanapokaribia mwanzo wa masomo ya watoto wao.
2. Mwanafunzi anayezungumziwa katika kifungu hiki anakwenda kujifunza katika aina gani ya shule?
3. Nani ambaye alimsindikiza mwanafunzi hadi shuleni?
4. Ni mawaidha gani aliyompatia baba yake walipokuwa njiani?
5. Eleza sifa za mwanafunzi anayezungumziwa katika kifungu hiki.
6. Ni nini kinachokuonyesha kwamba mwanafunzi huyu alipokelewa vizuri mara tu alipofika shuleni?
7. Kwa nini alishangaa alipofika bwenini?
8. Wanafunzi walipewa chakula gani wakati wa jioni?
9. Walipoingia darasani mwanafunzi huyu alifanya nini?
10. Wanafunzi walitakiwa kulala saa ngapi?

## 28.2. Matumizi ya msamiati

## Kazi ya 3:

**Tunga sentensi fupi kwa kutumia maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu ulichokisoma hapo juu.**

1. kujiandaa
2. kusaliti
3. kuuza
4. bidii
5. tabia
6. maadili
7. heri na fanaka
8. ukumbi
9. kusajili
10. kuashiria

## Kazi ya 4:

**Tumia mshale kwa kuonyesha maana ya maneno yafuatayo:**

| Maneno | Maelezo |
|---|---|
| 1. hofu | a. ukumbi mkubwa unaotumiwa na wanafunzi au askari kulia chakula. |
| 2. mzazi | b. karatasi aliyopewa mtu baada ya kulipa |
| 3. sauti nyororo | c. hali ya kutokuwa na ushujaa, amani, kuwa na woga. |
| 4. mwenendo | d. madini yanayonata sana na hutumika kwa kujengea barabara. |
| 5. mawaidha | e. nyumba za kulala wanafunzi katika shule au chuo. |
| 6. bwalo | f. mtoto wa kwamba kuzaliwa na mama/ mwanambee. |
| 7. umati | g. mlio laini. |
| 8. bweni | h. watu wengi sana. |
| 9. stakabadhi ya malipo | i. maneno ya maonyo au mafunzo, aghalabu ya kidini, na yenye mwongozo. |
| 10. kifunguamimba | j. mama au baba wa mtu |
| 11. lami | k. matendo ya mtu yanayojirudiarudia |

## 28.3. Sarufi: matumizi ya alama za vituo

**a. Nuktambili / koloni ( : )**

## Kazi ya 5:

**Tazama sentensi zifuatazo na kuzungumzia matumizi ya alama nuktambili inayojitokeza.**

i. Tunaenda sokoni kununua vitu vifuatavyo: nyanya, mahindi,…

ii. Katika familia yetu kuna watoto kama: Karangwa, Mukamurenzi…

iii. Jimbo la kusini kuna wilaya kama: Ruhango, Kamonyi, Huye

**Maelezo muhimu**

**Nukta mbili**

a. Hutumiwa kutanguliza maneno yaliyo katika orodha.

**Kwa mfano:**

i. Nenda ukaniletee: kalamu, karatasi na kifutio.

ii. Amenunua: machungwa, sukari, na ndizi.

b. Hutumiwa kuashiria maneno ya msemaji badala ya alama za mtajo hasa katika uandishi wa mazungumzo au tamthilia.

i. Mama: Lazima uniambie ulikokuwa tangu jana.

ii. Mwalimu alisema: Ingieni darasani.

c. Hutenganisha nambari za saa (saa na dakika).

**Kwa mfano:**

4: 10 – saa kumi na dakika kumi

**Kazi ya 6:**

**Sahihisha sentensi zifuatazo**

1. Mifano ya ndege wanaofugwa ni kuku, bata, na njiwa
2. Baba yangu hutengeneza meza, kiti, kitanda na kabati.
3. Familia huwa na baba, mama, nyanya, babu na watoto
4. Mimi huamka saa 2: 00 asubuhi kila siku
5. Mchezo wa kandanda ulianza saa10: 00 jioni

**b. Nuktamkato / nukta na kituo / semikoloni ( ; )**

**Kazi ya 7:**

**Tazama sentensi zifuatazo na kuzungumzia matumizi ya alama nuktamkato inayojitokeza.**

a. Sikwenda Kayonza; nilienda Kirehe.

b. Usiwe na wasiwasi; nitakuwa pamoja nawe siku zote.

c. Harusi hiyo ilihudhuriwa na watu wengi: wanawake kwa wanaume; wadogo kwa wakubwa; wazee kwa vijana.

**Maelezo muhimu**

**Nukta na kituo**

a. Hutumiwa kuunganisha vishazi vikuu bila kutumia kiunganishi.

**Kwa mfano:**

- Tuliwasili darasani tukiwa tumechelewa; mwalimu alitukaribisha kwa kutuuliza tulipokuwepo.

b. Hutumiwa kumpumzisha msomaji katika sentensi iliyo ndefu ili apumzike zaidi kuliko pale inapotumiwa koma.

**Kwa mfano:**

Alipofikiri sana, alitanabahi kuwa hakikuwepo cha kutorokwa; yeye angeweza kuondoka nyumbani au kumwacha mumewe, aende popote kufanya lolote.

c. Kuorodhesha vitu hasa vinapokuwa na zaidi ya neno moja

**Mfano:**

Wakati wa likizo tulitembelea sehemu kadhaa: Mombasa, Kenya; Dodoma, Tanzania; Kampala, Uganda na tukamalizia hapa Nairobi, Kenya.

**Kazi ya 8:**

**Sahihisha sentensi zifuatazo:**

1. Kabla ya kupata chakula ni lazima kunawa mikono hii ni tabia nzuri
2. Akili ni mali kila mtu ana zake.

## 28.4. Matumizi ya lugha: Taratibu za kutunga insha

**Kazi ya 9:**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Kwa sababu gani utangulizi mzuri ni muhimu katika insha?
2. Jadili sehemu kuu za insha.
3. Jadili mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha.

**Maelezo muhimu: Taratibu za kutunga insha:**

- Soma kwa makini mada/ kichwa/ anwani uliyopewa zaidi ya mara moja, ili uielewe vizuri.

- Ifikirie mada/ kichwa/ anwani kwa muda.
- Yaandike mambo muhimu yatakayokuongoza katika kuiandika insha .
- Maelezo yote yatolewe kwa undani na kwa njia ya kuvutia.
- Kutumia vizuri alama za uakifishaji.
- Kupanga mawazo katika mtiririko wenye mantiki.
- Kutumia msamiati mwafaka kwa kutegemea mada.
- Lugha iwe ya adabu na isiyo ya matusi.
- Andika methali, misemo na nahau ambazo unadhania zinaweza kukufaa katika utungaji.

**Mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha**

Bila kujali ni aina gani ya insha mtu anayoiandika, yapo mambo kadhaa ya kuzingatia wakati wa uandishi wa insha. Mambo hayo ni pamoja na:

1. Kubaini ni mada gani ya kuandikia insha na kuielewa vyema,
2. Kupanga mawazo katika mtiririko wenye mantiki,
3. Kutumia mtindo unaoendana na kusudi la insha.

**Kwa mfano**: Mtindo wa masimulizi unafaa kwa hadithi au insha nyingine za kisanaa.

4. Kutumia lugha fasaha na inayoeleweka,
5. Kufuata kanuni za uandishi.

**Kwa mfano:**

Matumizi ya alama za uandishi, aya, herufi kubwa na herufi ndogo.

Kupanga insha katika muundo wake, yaani *kichwa, utangulizi, kiini* na *hitimisho.*

**1. Kichwa cha habari**

Kichwa cha habari cha insha ni maneno machache, takribani matano, ambayo ndiyo jina la insha. Kichwa cha habari huandikwa juu, katikati kwenye ukurasa wa kwanza wa insha. Mara nyingi, huandikwa kwa herufi kubwa na hubeba wazo kuu la insha.

**2. Utangulizi wa insha**

Utangulizi wa insha ni sehemu ya mwanzo yenye urefu usiozidi aya moja. Utangulizi hudondoa kwa ufupi kabisa kile kinachoelezwa kwenye insha.

### 3. Kiini cha insha / mwili

Hii ni sehemu tunayoweza kusema ndiyo insha yenyewe. Kwenye kiini ndipo ufafanuzi wote hutolewa. Ufafanuzi huu hupangwa katika aya moja au zaidi. Hapa ndipo mwandishi hubainisha mawazo yake, huthibitisha, hushawishi, huhimiza na hufafanua kiundani kabisa.

### 4. Hitimisho la insha

Hii ni sehemu ya mwisho ya insha ambayo nayo haizidi aya moja. Katika sehemu hii, mwandishi anaweza kurejelea kwa ufupi sana yale aliyozungumzia kwenye insha yake, anaweza kuonyesha msimamo wake, anaweza kutoa mapendekezo, au kuwahimiza walengwa wake kuchukua hatua fulani.

## 28.5. Kusikiliza na kuzungumza

**Kazi ya 10:**

**Chagua mada moja kati ya hizi, kisha uizungumzie kwa mapana na marefu na kuiwasilisha mbele ya darasa.**

1. Harusi uliyoihudhuria
2. Mchezo uliohudhuria

## 28.6. Kuandika: Utungaji wa insha

**Kazi ya 11:**

**Andika insha ya ukurasa mmoja kuhusu “Siku yangu ya kwanza shuleni.”**

## Tathmini ya mada

**A. Sahihisha makosa ya kimaandishi katika mazungumzo hapa chini**

**Mgonjwa:** hujambo daktari

**Daktari:** sijambo Karibu uketi.

**Mgonjwa:** asante daktari

**Daktari:** nikusaidie vipi

**Mgonjwa:** Jina langu ni kayitesi ninaumwa na tumbo sana.

**Daktari:** pole sana kayitesi tumbo lilianza kukuuma lini

**Mgonjwa:** Tangu jana usiku hata sijalala ninaendesha na kutapika sana

**Daktari:** pole sana Ulikula nini jana usiku

**Mgonjwa:** Nilikula wali kwa kitoweo cha samaki

**Daktari** Mmmmhh!Wewe hunywa maji yaliyochemshwa

**Mgonjwa** Si kila siku daktari Mimi hunywa maji yoyote bora yanaonekana kuwa safi.

**B. Andika insha ya masimulizi kuhusu mada zifuatazo:**

i. Siku ya kuadhimisha mwaka mpya.
ii. Safari yangu mjini Kigali.
iii. Utoto wangu.
iv. Likizo iliyopita.

# MADA YA 8 DHIMA YA LUGHA YA KISWAHILI KATIKA JAMII

**Uwezo mahususi katika mada hii:**

Kuonyesha dhima ya lugha ya Kiswahili kwa jamii ya nchi zinazozungumza lugha hii.

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kutoa maana na umuhimu wa lugha,
- Kusoma na kuelewa kifungu kuhusu lugha kama chombo cha mawasiliano,
- Kusikiliza kwa makini na kusimulia kwa ufasaha kifungu cha habari kinachohusika,
- Kujadili namna ya kuitunza lugha na mwenendo unaofaa.

**Kidokezo**

1. Taja lugha zote zinazozungumzwa nchini Rwanda.
2. Andika dhima nne za lugha ya Kiswahili.

## SOMO LA 29: TUONGEE KISWAHILI SANIFU



**Kazi ya 1:**

**Tazama mchoro hapa juu na kujadili kazi mbalimbali zinazoendelea.**

## 29.1. Kusoma na ufahamu: Kiswahili nchini Rwanda

**Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha ujibu maswali yanayoambatana nacho:**

Lugha ya Kiswahili ni mojawapo ya lugha nne zinazozungumzwa nchini Rwanda. Hizi ni Kinyarwanda, Kiingereza, Kifaransa na Kiswahili vilevile. Hapo mwanzo, lugha ya Kiswahili ilikuwa lugha ya kibiashara lakini polepole mambo yalibadilika kutokana na ushirikiano wa Rwanda pamoja na nchi jirani zake ambazo ni Kenya, Tanzania, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Burundi zinazotumia lugha ya Kiswahili katika shughuli mbalimbali.

Lugha ya Kiswahili ambayo ni chombo cha mawasiliano kwa kupashana habari, nchini Rwanda, imeshamiri na kupata nguvu nyingi baada ya Rwanda kuwa mwanachama wa Jumuiya ya nchi za Afrika Mashariki, Kiswahili kikiwemo lugha rasmi.

Lugha ya Kiswahili hufundishwa nchini katika shule za sekondari na vyuo vikuu. Vituo vya utangazaji habari kama vile redio na vituo vya televisheni pia hutumia Kiswahili katika baadhi ya matangazo vinavyorusha.

Aidha, lugha ya Kiswahili hutunza, hukuza, na huendeleza utamaduni wa jamii, bila ya kusahau kwamba ni alama ya utambulisho wa jamii au taifa fulani.

**Kazi ya 2:**

**Maswali ya ufahamu**

1. Ni lugha gani zinazozungumzwa nchini Rwanda ?
2. Kwa sababu gani, nchini Rwanda, lugha ya Kiswahili imekua sana siku hizi?
3. Onyesha dhima mbili za Kiswahili.
4. Taja shule zinazofundisha Kiswahili nchini Rwanda .
5. Je, lugha ya Kiswahili ni lugha ya mawasiliano nchini? Eleza jibu lako kwa kutumia mifano sahihi kutoka kifungu.

## 29.2. Matumizi ya msamiati

### Kazi ya 3:


**Toa maana ya maneno yafuatayo:**

1. Dhima
2. Ushirikiano
3. Kupashana
4. Maarifa
5. Utamaduni
6. Jamii
7. Mzawa

## 29.3. Sarufi: Matumizi ya hali ya kuamuru



**Mchoro wa 1**



**Mchoro wa 2**

## Kazi ya 4:

**Tazama michoro hapo juu na kueleza kinachofanyika pale.**

## Kazi ya 5:

**Tunga sentensi tano kwa kutumia hali ya kuamuru.**

**Maelezo muhimu**

- Katika hali ya kuamuru au ya kushurutisha, vitenzi vya silabi zaidi ya moja na vyenye kiambishi tamati -a, huondolewa tu kiambishi cha kitenzi ku- katika umoja hali yakinishi. Katika wingi, vitenzi hivi huondolewa kiambishi ku- pamoja na kiambishi tamati-a, halafu vikachukua kiambishi -eni badala ya kiambishi -a cha mwishoni.

**Mfano:Kitenzi: kusimama**

**Umoja:** (Wewe) Simama!

**Wingi:** (Nyinyi/ Ninyi) Simameni!

## Kazi ya 6:

**Zikamilishe sentensi zifuatazo kwa kutumia hali ya kushurutisha kwa vitenzi ambavyo vimo katika mabano.**

***Kwa mfano:*** *Swali: Mwalimu aliwaambia wanafunzi: "…….madaftari yenu". (kuchukua)*

*Jibu: Mwalimu aliwaambia wanafunzi: "Chukueni madaftari yenu."*

1. "…………… kazi yako ya shule kuhusu dhima ya Kiswahili." Mama alimwamrisha mtoto wake. (fanya)
2. Mwalimu alimwomba mwanafunzi akisema: "…………… ubao tufanye mazoezi!"(Kufuta)
3. Baada ya kujiunga na nchi nyingine za Afrika Mashariki viongozi wa Rwanda walituambia: "……… Kiswahili!" (kuzungumza).
4. Kwa kuwa wewe ni mkazi wa nchi ya Rwanda …………. vizuri lugha ya Kinyarwanda! (ongea)
5. Mwalimu ameniambia kuwa mtafanya jaribio la Kiswahili kesho; kwa hiyo……… (kurudia) masomo yenu.
6. Mwalimu aliwaambia wanafunzi: "…………..runinga kuna mchezo wa kuigiza uhusuo uhifadhi wa mazingira!" (kutazama).

7. Katibu aliombwa na mwenyekiti: "……………….mawazo yote yatakayotolewa mkutanoni!" (kuandika).
8. Kama unataka kukuza stadi zako za kuzungumza na kusikiliza lugha ya Kiswahili, ……………..matangazo ya redioni na utazame runinga! (kusikiliza)

## 29.4. Matumizi ya Lugha: Maana na umuhimu wa lugha katika jamii

**Kazi ya 7:**

**Panga maneno yafuatayo kwa utaratibu unaofaa ili yaweze kuleta maana kamili**

1. ni -ya -Kiswahili- Mashariki- muhimu -lugha -Jumuia -ya -Afrika -katika -sana
2. Kiswahili -mwanzoni -kama- lugha -ilikuwa -ya- hapo- biashara- lugha-ikitumiwa -ya.
3. Walifurahi- rasmi- Wanyarwanda- kusikia- sana- mojawapo- lugha ya- nchini- Kiswahili- kwamba- ni- Rwanda- ya- lugha.

**Kazi ya 8:**

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. Jumuiya
2. Utamaduni
3. Matangazo
4. Jamii

## 29.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika jamii

**Kazi ya 9:**

**Jadili kuhusu dhima za lugha ya Kiswahili**

## 29.6 Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari

**Kazi ya 10:**

**Tunga kifungu kifupi (mistari kumi) ukionyesha faida ya Rwanda kutumia lugha ya Kiswahili**

# SOMO LA 30: MAWASILIANO YETU.




**Kazi ya 1:**

**Eleza kinachofanyika kwenye mchoro wa hapo juu.**

## 30.1. Kusoma na ufahamu: Ziara ya mjini

**Soma kifungu cha habari hiki na kujibu maswali yanayokifuata:**

Siku moja Bwana Mugisha aliondoka zake kijijini Kirenge kuelekea mjini. Alichukua mkoba wake mweusi na kuujaza kila kitu cha kumsadia njiani na mjini vilevile. Alipofika mjini, aliwakuta jamaa wawili mmoja aitwaye Rukundo na mwingine Ruhara.Walisalimiana kwa hamu kubwa kwani siku zilikuwa nyingi bila ya kuonana.

Wakati huo huo wasichana watatu Ange, Lidia na Isimbi walipita karibu nao wakiwa wametoka kabisa. Lugha waliyokuwa wanaongea ilimshangaza Mugisha sana kwani ilikuwa mara yake ya kwanza kuisikia. « Mbona watu hawa siwaelewi hata kidogo, wametoka wapi ? » Alitamka haya akiwa na mshangao mkubwa sana. Ruhara ambaye alizoea maisha ya mjini

alimwambia, ''hii ni lugha ya Kiswahili, lugha nzuri yenye *asili ya upwa wote wa Afrika Mashariki.*'' Aliendelea kumsimulia yaliyompata alipokwenda sehemu za Arusha huko Tanzania. ''Miaka miwili iliyopita, nilikwenda mjini Arusha katika mkutano wa waumini wa dini moja huko, nilipoingia mjini lugha ilikuwa hiyo, mitaani na migahawani, misikitini na makanisani, kweli sikuwa na tamko lolote isipokuwa kimya tu na kutumia ishara. Kwa bahati nzuri, nilipata usaidizi kutoka kwa raia wa huko kwani baadhi yao walijua lugha nyingi ikiwemo yangu. Baada ya wiki moja, tulirudi kwetu nikiwa na fikra moja kichwani mwangu ya kujifunza Kiswahili na kukizungumza vizuri. Leo nina hatua nzuri. ''

Kuyasikia hayo, Mugisha aliunga mkono Ruhara na kusema kuwa naye angepata mwalimu angejifunza Kiswahili. Wote waliendelea na safari zao kwa makubaliano ya kujua lugha zaidi ya moja, msingi wa maendeleo na ushirikiano na wengine.

Punde si punde mabinti wale Ange, Lidia na Isimbi walimwita Mugisha ambaye alionekana kuwa mgeni mjini. Walisema '' Mzee njoo hapa, tunahitaji kuongea na wewe.'' Mugisha bila kusita alianza mbio kinyumenyume akihofia kuibiwa au usumbufu mwingine. Yeye aliona wasichana hao kama wakware ambao wanataka awape pesa zake alizokuwa ameficha mkobani chini ya nguo. Ange alimfuata kwa hatua ndefu na maneno ya upole, jambo lililopunguza wasiwasi wake Mugisha na kusimama.

Mazungumzo yalianza katika lugha ya Kinyarwanda Ange na wenzake wakimwonyesha umuhimu wa lugha kama chombo cha mawasiliano kati ya jamii fulani. Bwana Mugisha aliwajulisha uamuzi wake ili mara ijayo asije akakabiliana na shida hiyo tena. Walimfundisha maneno machache na kumshauri aendelee kuvifuata vipindi vya redio na televisheni katika Kiswahili. Mugisha aliwaomba namba zao za simu ili kila mara atakapopata shida au atahitaji msaada awapigie simu. Wasichana walimnunulia chakula na chai akala na kushiba. Baadaye, kundi la watatu lilimuaga Mugisha. Tangu siku hiyo, Mugisha hawezi kuidharau lugha na umuhimu wa mawasiliano.

**Kazi ya 2:**

**Maswali ya ufahamu**

1. Toa majina ya wahusika katika kifungu cha habari hiki.
2. Mgeni huyu alishangazwa na nini alipofika mjini?
3. Kwa sababu gani Ruhara alikuwa kimya na kutumia ishara tu alipokuwa mjini Arusha ? Alisaidiwa na nini ?
4. Je, mabinti waliokutana na Mugisha walizungumza lugha zaidi ya moja ? Fafanua jibu lako.
5. Kwa nini Mugisha alianza kukimbia alipoitwa na wasichana ?
6. Nini kilimridhisha Mugisha katika ziara yake mjini ?
7. Ingekuwa wewe ungefanya nini baada ya kupata shida ya kimawasiliano ? Jadili.

## 30.2. Matumizi ya msamiati kuhusu mawasiliano yetu

**Kazi ya 3:**

**Toa kinyume cha maneno haya:**

1. Mzee
2. Mji
3. Haraka
4. Lugha nzuri
5. Karibu

**Kazi ya 4:**

**Jaza sentensi hizi kwa kutumia msamiati unaofaa ulioko katika kifungu**

1. Bwana Mugisha alisaidiwa na………………………wawili waliomnunulia ………….akala akashiba.
2. Miaka miwili iliyopita ……………..alikwenda mjini…………….. katika …….wa waumini.
3. Ange na ……..waliongea lugha ya…………na lugha ya.....
4. Mugisha alidhani wasichana walikuwa ……………..na kukimbia.

## Kazi ya 5:

**Eleza maana ya maneno yanayofuata:**

a. Mkoba

b. Jamaa

c. Mkutano

d. Kutoka

e. Fikra

f. Binti

g. Mbio

h. Kuaga

## Kazi ya 6:

**Kamilisha sentensi zifuatazo ili zilete maana kamili kwa kutumia msamiati huu:** *lugha, jumuia, televisheni, simu, ishara.*

1. Kiswahili ni................................ambayo inatumiwa katika ……………………ya afrika Mashariki.
2. Jamila hufuata vipindi vya………………………kila siku.
3. Wasichana watapigiwa …………………….. na mzee Karinda.
4. Mtu asiye na ujuzi wa lugha lazima atumie……..…………………

## 30.3. Sarufi: Hali ya kuamuru

**Kazi ya 7:**

**Soma mazungumzo yafuatayo na kubainisha vitenzi vilivyotumiwa katika hali ya kuamuru**

**Baba:** Waambaje, Nikuze?

**Nikuze:** Salama babangu. Naona umechoka leo! Tafadhali nenda bafuni.

**Baba:** Ehee! Leo nimefanya kazi nyingi bila kupumuzika. Nenda ukaniletee maji na sabuni ya kuogea.

**Nikuze:** Ndiyo. Jitayarishe, uchukue taulo na kandambili halafu uende bafuni.

**Baba**: Asante sana binti yangu. Niandalie chakula haraka iwezekanavyo nina njaa.

**Nikuze:** Chakula kimeiva na ninakaribia kukiweka mezani. Nimekupikia ugali na kitoweo kitamu sana bila shaka utakifurahia. Karibu ndani mama.

**Mama**: Asante binti yangu. Habari za nyumbani?

**Nikuze:** Nzuri mama. Baba amekuja akiwa amechoka na hivi sasa yumo bafuni.

**Mama**: Ni kweli kabisa. Leo amefanya kazi isiyo rahisi.

**Nikuze** : Namwona baba anatoka bafuni usisahau kumpa pole kwa uchovu alio nao.

**Mama:** Wewe mwekee chakula na kinywaji mezani, mengine ni yangu. Fanya haraka binti yangu.

**Nikuze:** Barabara kabisa.

**Kazi ya 8:**

**Tunga sentensi tatu kwa kutumia hali ya kuamuru tungo yakinishi.**

**Kazi ya 9:**

**Tunga sentensi tatu zenye vitenzi vilivyoko katika hali ya kuamuru tungo kanushi.**

**Maelezo muhimu kuhusu hali ya kuamuru / hali ya amri**

Hali ya kuamuru ni  ya vitenzi ambavyo vimo katika hali shurutishi au ya kulazimisha yaani mtendaji wa tendo halitendi kwa hiari yake bali ni kwa sharti ya mtu mwingine.

Huonyesha kuwa mtu analazimishwa kufanya jambo fulani. Hutumiwa kwa nafsi ya pili tu (umoja na wingi).

Tunafuata kanuni zifuatazo :

- Vitenzi vyenye silabi nyingi, hupoteza ku- ya kitenzi. Kwa wingi, kitenzi huongezwa «-ni» mwishoni, katika hali yakinishi.

**Mfano:** Nyamaza! (Umoja)

Nyamazeni! (Wingi)

shukuru! (umoja)

shukuruni! (wingi)

- Katika hali kanushi, vitenzi huishia na «-e» isipokuwa vitenzi vya asili ya kigeni.

**Mfano:** Usinyamaze! (Umoja)

msinyamaze! (Wingi)

- Usirudi! (umoja)
- Msirudi! (wingi)

- Vitenzi vyenye silabi moja hubaki na «ku-» ya kitenzi (katika hali yakinishi) na huongezwa «-ni», kwa wingi.

**Mfano**: - Kunywa! (umoja)

- Usinywe!
- Kunyweni! (wingi)
- Msinywe!

- Vitenzi: kuja, kwenda (kuenda) na kuleta, havifuati kanuni hizi.

**Mifano:**

**a.** Kuja:

Njoo! (umoja hali yakinishi)

Usije! (hali yakinishi)

Njooni! (wingi hali yakinishi)

Msije! (wingi hali kanushi)

**b.** Kwenda/kuenda :

Nenda! (Umoja hali yakinishi)

Usiende! (Umujo hali kanushi)

Nendeni! (Wingi hali yakinishi)

Msiende! (Wingi hali kanushi)

**c.** Kuleta:

Lete! (Umoja hali yakinishi)

Usilete! (Umoja hali kamushi)

Leteni! (Wingi hali yakinishi)

Msilete! (Wingi hali kanushi)

**d.** Kupa:

Nipe! (Umoja hali yakinishi)

usinipe! (Umoja hali kanushi)

Nipeni! (Wingi hali yakinishi)

Msinipe! (Wingi hari kanushi)

**Kazi ya 10:**

**Badilisha sentensi zifuatazo ziwe katika hali ya kuamuru katika wingi.**

1. Njoo hapa utusalimu!
2. Kimbia ili usichelewe shuleni!

## 30.4. Matumizi ya lugha: Mawasiliano yetu

**Kazi ya 11:**

**Jadili maswali yafuatayo:**

Mawasiliano ni nini?

Je,ndege na wanyama huwasiliana kwa njia gani?

Mawasiliano yana umuhimu gani ?

**Maelezo muhimu**

Mawasiliano ni mchakato wa kuhawilisha taarifa kwa njia ya ubadilishanaji wa mawazo, hisia, malengo, tabia, matarajio, mitazamo kupitia mazungumzo, ishara na maandishi. Ni ubadilishanaji wa taarifa unaoleta maana baina ya pande mbili au zaidi ambazo zinaweza kuwa viumbe hai au kinyume chake.

Lugha ni chombo cha mawasiliano ambacho amejaliwa binadamu tu na kwamba hakuna kiumbe mwingine ambaye si binadamu mwenye uwezo wa kuzungumza na kutumia lugha. Hii ina maana kuwa kuna sifa fulani za lugha za binadamu ambazo hazipatikani kwa kiumbe mwingine yeyote yule isipokuwa mwanadamu.

Ingawa ndege, mbwa, nyuki, tumbili wanaweza kuwasiliana, mawasiliano yao huwa ni ya sauti au ishara ambazo kimsingi siyo lugha, pia huwa yanadhibitiwa na hisia tu kama hofu, njaa, na ishara za kutoa taarifa.

Binadamu ana uwezo wa kujifunza lugha mbalimbali na kuzitumia katika mazingira yake na kitu ambacho wanyama hawawezi. Kwa mfano, ukimchukua paka wa Uchina na kumleta Rwanda atatoa sauti ile ile sawa na paka wa Rwanda  kwa kueleza shida ile ile au kutoa ishara ile ile.

Ulishawahi kujiuliza kwamba mawasiliano yangekuwaje pasipokuwepo lugha? Mwalimu angekuwa anatumia mtindo gani kukufundisha darasani au wewe ungemwombaje kalamu rafiki yako? (Unasema ungewasiliana kama wanavyowasiliana watu wasiosikia au kuzungumza?) Hao pia wanawasiliana hivyo kwa sababu wana maarifa ya lugha. Watu wasiosikia au kuzungumza wanawasiliana kwa lugha ya ishara, lugha ambayo inafundishwa katika baadhi ya shule za sekondari na vyuo vikuu nchini Rwanda.

Ufumbuzi wa kisayansi na kiteknolojia usingewezekana pasipo kuitumia lugha, usingeweza kusogoa na marafiki zako kwenye fesibuku, usingeweza kumwandikia ujumbe rafiki yako kupitia simu yako na kadhalika. Kiswahili kinatarajiwa kutumika kama chombo cha mawasiliano katika taaluma mbalimbali kama vile utawala na taasisi mbalimbali kama vile bungeni, mahakamani na penginepo.

**Kazi ya 12:**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. watu wasiosikia au kuzungumza huwasiliana kwa njia ipi?
2. Ni tofauti gani kati ya mawasiliano ya binadamu na yale ya viumbe wengine?
3. Andika njia nne ambamo Kiswahili kinaweza kutumiwa na kurahisisha mawasiliano.

## Kazi ya 13:

**Pamoja na picha hizi, sema ikiwa kuna mawasiliano ya lugha, ya ishara au ya sauti na kujaza jedwali hapo chini:**



Chui



njiwa



Baba nawatoto



panzi



Msichana



chatu

| Mawasiliano ya lugha | Mawasiliano ya ishara au sauti |
|---|---|
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |

## 30.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

## Kazi ya 14:

**"Mawasiliano ya lugha ni bora kuliko mawasiliano ya ishara na sauti." jadili kauli hii.**

### 30.6. Kuandika: Utangaji wa insha

**Kazi ya 15:**

**Tunga insha fupifupi ukionyesha umuhimu wa lugha ya Kiswahili nchini Rwanda.**

**Kazi ya 16:**

**Andika aya mbili kuhusu "umuhimu wa mawasiliano."**

## SOMO LA 31: UMUHIMU WA LUGHA



**Kazi ya 1:**

**Eleza yale unayoyaona kwenye mchoro huu.**

### 31.1. Kusoma na ufahamu: Umuhimu wa lugha

***Soma kifungu kifuatacho kuhusu "Umuhimu wa lugha" kisha, jibu maswali uliyopewa hapo chini.***

Familia ya mzee Yakobo inaishi katika kijiji cha Nyamugari. Kila mara Mzee Yakobo huwahimiza watoto wake Maria na Maria kujifunza lugha mbalimbali kwa madhumuni ya maisha yao ya usoni. Yeye anajua kwamba lugha, kama mfumo wa ishara au sauti nasibu zinazowezesha jamii kuwasiliana, ina

umuhimu sana katika maisha ya kila siku. Tangu Maria alipoyasikia maneno ya baba yake aliyazingatia sana mawaidha aliyopewa na kujifunza vizuri lugha zote zilizopatikana kwenye ratiba yake ya masomo. Kwa sasa, yeye ni mkuu wa kitengo cha utalii katika taasisi inayoshughulikia masuala ya utalii na mazingira. Petro ni tofauti na ndugu yake Petro aliyeonyesha mtazamo hasi kuhusu ujifunzaji wa lugha. Yeye alipenda kusema: « Siwezi kupoteza muda wangu kujifunza lugha za watu wengine, lugha ninayozungumza inanitosha». Kwa kweli, alikuwa mtoto mtukutu asiyejali maonyo na mawaidha ya wazazi wake. Kwake, kujisomea hata sentensi fupi za Kiswahili lilikuwa jambo la ajabu! Alikuwa amesitisha masomo yake alipomaliza darasa la pili katika shule ya Sekondari ya Nyamugari ingawa baba yake hakuacha kumuonya kuhusu umuhimu wa elimu na nafasi ya lugha katika maisha ya binadamu.

Siku moja, Mzee Yakobo aliamua kwenda kumtembelea binti yake aliyeishi katika nchi jirani. Petro alimsihi waende pamoja kuwasalimia binamu zake ambao ni Kamugisha na Kana. Mzee Yakobo aliposikia maneno ya mtoto wake, hakusita kukubali wazo lake. Alifikiria kwamba mtoto wake angekutana na binamu zake wangemuuliza mengi kuhusiana na masomo yake. Kwa hivyo, Mzee Yakobo alimwomba mtoto wake Petro ajiandae kwa safari.

Gari lao lilitoka Nyabugogo saa kumi na moja alfajiri. Walipofika njiani, Petro alishindwa kuvumilia njaa iliyokuwa ikimuuma kutokana na safari ndefu. Kwa bahati nzuri, walipofika katika mji mmoja, dereva aliamua kusimamisha gari ili wasafiri waweze kwenda haja na wengine waweze kujinunulia chakula na kinywaji kabla hawajaendelea na safari yao. Baba yake Yakobo alimwonea huruma mtoto wake na kumpa shilingi mia mbili ili aweze kwenda kujinunulia chakula. Petro alifurahi sana. Alikuwa na hamu ya kula mkate na kunywa juisi ya matunda iliyotengenezewa katika nchi jirani. Alienda haraka na kuingia dukani. Dukani alimkuta Bi Hassani aliyemkaribisha na kumuuliza alichotaka kununua dukani humo.

Lo ! Petro alikosa neno. Alisimama akimkodolea macho kama aliyejiingiza baharini bila kujua kuogelea. Kweli alishindwa kuulizia kile kilichomleta pale. Alijitahidi kutumia ishara kumwonyesha sehemu palipowekwa mikate na vyakula vingine lakini mfanyabiashara hakuelewa alichokuwa anahitaji miongoni mwa vyakula vilivyokuwemo dukani. Petro aliposhindwa kusema alichukua shilingi zote alizokuwa nazo na kumkabidhi Bi. Hassani. Hapo ndipo alipewa mkate na maji. Petro alipokea kwa shingo upande alichopewa na mwenye duka na kurudi haraka na kuziacha shilingi mia moja zilizobaki kwenye jumla ya bei ya mkate na maji. Kama angekwenda shuleni asingefanyiwa hayo.

Mara moja, dereva alianza kugeuza gari ili waendelee na safari. Petro alikuwa ameketi kwenye kiti chake karibu na baba yake. “Salaalaa!” Yakobo alishikwa na bumbuazi alipoona mtoto wake ameleta chakula kilichokuwa kimepitisha tarehe ya kukila mwaka uliopita. “Wewe hujui kusoma wala kuhesabu! Tazama tarehe iliyoandikwa hapa! Huoni kuwa chakula hiki kingepaswa kuliwa kabla ya mwezi uliopita?” Kwa kweli, alianza kujiuliza mengi kuhusu maisha ya mtoto wake. Alisikitika sana na kumwomba asithubutu kula chakula hicho kwani kingeweza kuharibu afya yake. Petro alikunywa maji tu aliyoleta na kuvumilia njaa iliyokuwa ikimbana wakati huo. Alianza kujuta kwa kutofuata mawaidha aliyopewa na wazazi wake. Alifikiri, “Nisingepuuza mawaidha ya baba yangu, nisingekutana na matatizo haya”.

Walipofika Dar-es-salaam, walifurahi kuonana na shangazi na binamu zake. Walipokelewa vizuri na kupata muda wa kutembelea mazingira mazuri ya jiji hilo. Tangu alipofika, Petro alifuatana na binamu zake kila wakati walipotoka kununua vitu ili asikilize walivyoweza kuwasiliana na watu wengine katika lugha ya Kiswahili. Hapo, aliweza kuelewa umuhimu wa kujifunza lugha na aliamua kwamba angeanza kujifunza kwa bidii mara wakirudi nyumbani. Kwa sasa, Petro amemaliza kidato cha tatu katika shule ya Sekondari ya Museta ambapo walimu wake wanampenda kwa uwezo wake wa kuzungumza lugha ya Kiswahili na lugha nyingine anazojifunza.

## Kazi ya 2:

### Maswali ya Ufahamu

1. Taja majina ya watu wanaozungumziwa katika kifungu hiki.
2. Ni mawaidha gani mzee Yakobo aliyokuwa anawapa watoto wake ?
3. Maria amefaidika vipi kutokana na ujuzi wake wa lugha mbalimbali ?
4. Safari ya mzee Yakobo ilikuwa na lengo gani ?
5. Ni hasara gani aliyoipata Petro aliposhindwa kuwasiliana na mfanyabiashara ?
6. Eleza tabia za mfanyabiashara Bi Hassani mbele ya mteja wake.
7. Ni jambo lipi lingetokea ikiwa mzee Yakobo hakumkataza mtoto wake Petro kula chakula alichokinunua ?
8. Petro alikuwa na majuto gani? Kwa nini alijuta?
9. Aliporudi nyumbani alifanya nini?
10. Unajifunza nini kutokana na kifungu hiki cha habari?

## 31.2. Msamiati kuhusu umuhimu wa lugha

### Kazi ya 3:

**Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo huku ukizingatia matumizi yake katika kifungu cha habari ulichosoma hapo juu.**

1. Kuhimiza
2. Madhumuni
3. Mawaidha
4. Mtazamo
5. Mtukutu
6. Utalii
7. Kwenda haja
8. Kwa shingo upande
9. Bidii
10. Bumbuazi

### Kazi ya 4:

**Oanisha maneno katika sehemu A na maana zake zilizopo katika sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Inayoshughulikia | a. Enye kujulikana kila mahali, mashuhuri |
| 2. Mtazamo | c. Watu wanaokwenda au walio katika safari |
| 3. Madhumuni | d. Maneno ya maonyo au ya mafunzo yenye mwongozo na mashauri |
| 4. Alijitahidi | e. Kwenda choo kwa ajili ya haja kubwa au ndogo |
| 5. Aliyazingatia | f. Kuacha kutia maanani, kudharau |
| 6. Wasafiri | g. hamu ya kufanya jambo, juhudi |
| 7. Bumbuazi | h. Sababu ya kufanya jambo; kusudi; nia; lengo |
| 8. Bidii | i. Hali ya kuwa kimya na kutojua la kufanya au kutosikia lisemwalo |
| 9. Mazingira | j. Namna ya kuangalia au kutazama kitu au mtu |

**Kazi ya 5:**

**Jaza nafasi kwa kutumia maneno mwafaka yafuatayo: bidii, madhumuni, kupuuza, maarufu, mawaidha, mtazamo, bumbuazi, ratiba, kwenda haja, shingo upande**

1. Nilianzisha mradi huu kwa ...................................ya kuhifadhi mazingira yetu.
2. Kila mwanafunzi analazimishwa kuwa na .........................ya masomo yake ya kila siku.
3. Usipojifunza kwa............................ basi hutafaulu mitihani yako.
4. Aliposikia habari hiyo alipigwa na .............................. na kukosa la kufanya.
5. Anaanza kujuta kwa kutofuata ...................................ya baba yake.
6. Baada ya kufanya safari ndefu, wasafiri wamesimamisha dereva ili waweze ....................
7. Sikubaliani na ..............................wako kuhusu uhifadhi mwafaka wa mazingira.
8. Alipokea zawadi hiyo kwa..............................................
9. Amekuwa mchezaji...................................kutokana na ustadi wake wa kusakata mpira.
10. Si vizuri ..............................fikra za mwenzako kabla hujamsikiliza.

## 31.3. Sarufi: Matumizi ya hali ya kuamuru

**Kazi ya 6:**

**Soma kifungu cha habari kifuatacho na kubainisha vitenzi vilivyotumiwa katika hali ya kuamrisha**

Ona kwenye gazeti hili viongozi wa mataifa mbalimbali wamekusanyika mjini Kigali. Lengo lao ni maendeleo ya lugha yetu. Soma habari yote uelewe vizuri yanayoendelea pale na usiendelee kusimama kwenye barabara. Kimbia nyumbani uwashe runinga yako ili uweze kuwaona na uandike matangazo hayo kwa ufupi. Lakini jaribu kujifunza Kiswahili kitakuwezesha kushirikiana na jamii, nchi zote za kanda hii hasa hasa Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki kwani Kiswahili ni lugha rasmi.

## Kazi ya 7:


**Tunga sentensi tano zenye vitenzi mbalimbali katika hali ya kuamuru.**

## Kazi ya 8:

**Tazama picha hizi kisha utunge sentensi katika hali ya kuamuru kulingana na vitendo vinavyoendelea kwenye picha hizi:**











## Kazi ya 9:

**Andika vitenzi vilivyopigiwa msitari katika hali ya kuamuru tungo yakinishi na kanushi:**

Nchi yetu ni nzuri sana,ina milima na mabonde,viongozi bora na sehemu mbalimbali za utalii. Mutesi hutembelea maziwa mengi naye Bugingo husafisha kwake akipanda maua na miti ili kuhifadhi mazingira. Yeye huwazuru wenzake akiwashawishi watende mema kila siku. Benita aliamua kujenga nchi yake kwa kufanya kazi za umuganda, vilevile akiwajengea wasiojiweza na kutengeneza barabara.

**Kazi ya 10:**

**Weka sentensi zifuatazo katika hali ya kuamuru katika umoja na kuzingatia mabadiliko ya kisintaksia katika sentensi.**

a. Sauti ya pili,ingieni tuimbie Bwana.

b. Teteeni maendeleo ya lugha ya kiswahili.

c. Kuleni nyama yote pia osheni vyombo.

d. Lieni kwa sauti ndogo majambazi yasituvamie.

## 31.4. Matumizi ya lugha: Umuhimu wa lugha

**Kazi ya 11:**

**Soma maelezo yafuatayo, kisha ujibu maswali hapo chini.**

**Maelezo muhimu: Umuhimu wa lugha**

Lugha ni mojawapo ya vipengele vya utamaduni wa jamii na tena ni chombo cha utamaduni. Hili ni kwa sababu chombo hiki hutumiwa kuwasilisha amali, mila na desturi zote za jamii. Lugha ndio uti wa mgongo wa utamaduni. Lengo kuu la lugha katika jamii ni pamoja na kuwafanya watu wawasiliane kwa kupashana habari. Kujua lugha fulani kunamwezesha mtu kujipatia marafiki, kukuza ujuzi kwa kusoma maandishi mbalimbali au kwa kufuata vipindi mbalimbali kwenye redio, runinga na tovuti

Kutumia lugha moja katika jamii kunaweza kuwa na faida pamoja na hasara mbalimbali kutokana na mazingira ya jamii. Rwanda kama nchi inayozungukwa na nchi zinazotumia Kiswahili, itanufaika kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Vilevile, lugha ya Kiswahili ina umuhimu mkubwa sana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuwa lugha hii ndiyo lugha rasmi inayotumiwa katika Jumuiya hii.

**Maswali:**

1. "*Lugha ndio uti wa mgongo wa utamaduni.*" Eleza.
2. Lipi ni lengo kuu la kuijua lugha?
3. Jadili: "*Kutumia lugha moja katika jamii kunaweza kuwa na faida pamoja na hasara mbalimbali*".

## 31.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

**Kazi ya 12:**

**Jadili kuhusu mambo yafuatayo:**

1. Matatizo yawezayo kujitokeza baina ya watu wawili wanaposhindwa kusikilizana kimawasiliano
2. Umuhimu wa lugha katika jamii
3. Mambo mbalimbali yanayoweza kukwamisha mawasiliano yenye kutumia lugha

## 31.6. Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari

**Kazi ya 13:**

**Kwa kutoa hoja zenye mifano, tunga kifungu chako kwa kutumia mada ifuatayo:**

“Lugha inapotumiwa vizuri hujenga jamii na ikitumiwa vibaya huangamiza jamii”.

**Kazi ya 14:**

**Chagua mada moja kati ya hizi zifuatazo na kuzitungia insha isiyopungua maneno 100.**

- Lugha ni kitambulisho cha jamii
- Lugha hurahisisha mawasiliano katika jamii
- Lugha hukuza utamaduni
- Lugha huburudisha

## Tathmini ya mada

**Jibu maswali yote.**

1. Je, ushirikiano wa Rwanda pamoja na nchi nyingine za kikanda ulisaidia nini Kiswahili?
2. Toa lugha rasmi nchini Rwanda.
3. Ni vituo gani vya utangazaji habari vinavyotumia Kiswahili katika baadhi ya matangazo vinavyorusha?
4. Fafanua maneno haya: - Malighafi, chatu, mawaidha.
5. Jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia neno lililo mabanoni:

i. "…………… kazi yako ya shule kuhusu dhima ya kiswahili!". Mama alimuamrisha mtoto wake (kurekebisha).

ii. Mwalimu alimwomba mwanafunzi akisema: "…………… kurasa mbili za kifungu!"(Kuandika).

iii. Baada ya kujiunga na nchi nyingine za Afrika Mashariki viongozi wa Rwanda walituambia: "……… Kiswahili!" (jifunza)

6. Onyesha umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika jamii.

## MAREJEO


1. Ntawiyanga, S. na Wenzake (2016). *Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Kidato cha Kwanza.* Longhorn Publishers (K) Ltd.
2. Ndalu, A. E. (2016). *Masomo ya Kiswahili Sanifu, Kidato cha 2.* Moran (E.A.) Publishers Ltd.
3. Rwanda Education Board (2019). *Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Mchepuo wa Lugha, Kidato cha 4.* Rwanda Education Board.
4. Rwanda Education Board (2019). *Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Michepuo Mingine, Kidato cha 6*. Rwanda Education Board.
5. TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la Pili*. Oxford University Press.
6. NKWERA, F.M.V. (1979). *Sarufi na Fasihi, Sekondari na Vyuo*. Tanzania Publishing House Dar-es-salaam, Tanzania.
7. *https://sw.wikipedia.org/wiki/Kito_(madini)*
8. *https://www.youtube.com/watch?v=NK4M_yrYIJI*
9. *https://www.youtube.com/watch?v=G91GtbgdZKA*
10. *http://swa.gafkosoft.com/maigizo*
11. *https://www.facebook.com/1416762588414463/posts/hali-ya-kuamuru-hali-hii-ilichambuliwa-kwenye-tawi-la-mutanga-jumapili-hii-kidat/1823486384408746/*